

8 j CONSTITUTIONAL PUBLIC HEARING, ELDORET SOUTH CONSTITUENCY AT ELDORET ASK SHOW

GROUND ON 1ST JULY 2002

Present

Com. Riunga Raiji

Com. Salome Muigai

Com. Domiziano Ratanya

Secretariat staff in attendance

John Watibini Programme Officer

Lynne Sigei Asst. Programme Officer

Grace Gitu Verbatim Recorder

Gilbert Bor District Co-ordinator

The meeting started at 9.20 a.m. with Com. Salome Muigai in the chair

Com. Salome Muigai: Kwa niaba ya team ya Tume ya Marekebisho ya Katiba, ningetaka kuwakaribisha hapa leo na kukitangaza hiki kikao cha tume ya marekebisho ya Katiba na pia kusema hiki ni kikao cha dharura, hiyo ni kusema kila mtu amekaribishwa lakini kabla hatujaanza ningetaka kuomba mtu mmoja atufungulie kwa maombi. Helen, is that you Helen Rono?

Karibu

Helen Rono: Hebu tusimame na tuombe. Kwa jina la Baba, la Mwana na Roho Mtakatifu, Amen. Mungu Baba tunakushukuru kwa asubuhi njema umetuwezesha tufike hapa. Asante kwa wageni umetuletea. Tunapoanza huu mkutano ukue pamoja nasi, mpaka saa zile tutakapo maliza ukue pamoja nasi. Naomba haya machache kwa jina la Kristo Mwokozi wetu, AMEN

CONSTITUTIONAL PUBLIC HEARING, ELDORET SOUTH CONSTITUENCY AT ELDORET ASK SHOW

GROUND ON 1ST JULY 2002

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, ELDORET SOUTH CONSTITUTUENCY HELD AT ELDORET ASK SHOWGROUND ON 1ST JULY 2002.

PRESENT

Com. Riunga Raiji

Com. Salome Muigai

Com. Domiziano Ratanya

Secretariat staff in attendance

John Watibini Programme Officer

Lynne Sigei Asst. Programme Officer

Grace Gitu Verbatim Recorder

Gilbert Bor District Co-ordinator

The meeting started at 9.20 a.m. with Com. Salome Muigai in the chair

Com. Salome Muigai: Kwa niaba ya team ya Tume ya Marekebisho ya Katiba, ningetaka kuwakaribisha hapa leo na kukitangaza hiki kikao cha tume ya marekebisho ya Katiba na pia kusema hiki ni kikao cha dharura, hiyo ni kusema kila mtu amekaribishwa lakini kabla hatujaanza ningetaka kuomba mtu mmoja atufungulie kwa maombi. Helen, is that you Helen Rono?
Karibu

Helen Rono: Hebu tusimame na tuombe. Kwa jina la Baba, la Mwana na Roho Mtakatifu, Amen. Mungu Baba tunakushukuru kwa asubuhi njema umetuwezesha tufike hapa. Asante kwa wageni umetuletea. Tunapoanza huu mkutano ukue pamoja nasi, mpaka saa zile tutakapo maliza ukue pamoja nasi. Naomba haya machache kwa jina la Kristo Mwokozi wetu, AMEN

Com. Salome Muigai: Asante sana Bi. Rono. Sasa ningetaka kuwajulisha wanatume wenye wameandamana nasi, na nitaanza na mwanatume aliye upande wangu wa kushoto, na nitampa hichi chombo cha kupazia sauti ili nanyi mzikie sauti yake.

Com. Raiji: Hamjambo, kwa majina mimi naitwa Riunga Raiji na mimi ni mmoja wa ma-Commissioners, asante

Domiziano Ratanya: Hamjamboni wote. Mimi ninaitwa Domiziano Ratanya na ni mmoja wa Commissioners.

Com. Salome Muigai: Pia tuna wafanyi kazi kutoka kwenye ofisi za Tume na pia hao watajijulisha hao niwa kina nani.

John Watibini: Mimi naitwa John Watibini, mimi ni Program Officer, nasaidia ma-Commissioners wangu. Hamjambo?

Audience: Hatujambo

John Watibini: Hamjambo tena. Asanteni

Lynne Sigei: Hamjambo

Audience: Hatujambo

Lynne Sigei: Mimi ni Lynne Sigei, mimi ni Assistant Program Officer

Grace Gitu: Hamjambo

Audience: Hatujambo

Grace Gitu: Mimi naitwa Grace Gitu, mimi ni Verbatim Recorder wa ku-tape vile mnavyosema. Asante

Maingi: Hamjambo

Audience: Hatujambo

Maingi: Mimi naitwa Maingi na mimi ni Engineer wa hii mitambo

Gilbert Bor: Hamjambo nyote

Audience: Hatujambo

Gilbert Bor: Mimi ni Gilbert Bor, District Co-ordinator wenu. Karibuni

Com. Salome Muigai: Sasa mmewajua wa team ya kutoka kwa Tume ya Marekebisho ya Katiba. Mimi nitakua mwenye kiti wa kikao hiki na jina langu ni Salome Wairumu Muigai. Nilizaliwa hapa Mitianda, nikasoma hapa Township, kwa hivyo niko nyumbani kabisa na ninawakaribisha kwenye kikao hiki. Na sasa kabla hatujaanza, ningetaka kuwaeleza utaratibu tutakao fuata kwa kikao cha leo. Kwanza, unaweza kutumia lugha yeyote ukija kutuzungumzia. Sisi wenyewe tunatumia lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza kwani ndizo lugha rasmi, lakini ikikubidi kuzungumza lugha nyingine, tutatafuta mtu mwenye atafanya tafsiri ndio uweze kujisikia unaweza kujieleza. Hata ikiwa ni mtu ambaye hasikii, tutatafuta mtu mwenye kutueleza kwa ishara vile anavyosema.

Pia ningetaka kueleza kwamba kuna namna tatu ya kupeana maoni. Unaweza kuja ukawa una maandishi yako. Ukiwa una maandishi na ungetaka kutupatia tu, basi utaende kujiandikisha pale kwa Bwana Watibini na umpatie maandishi yako

(memorandum). Pia unaweza kuwa na maandishi na ukataka kueleza kidogo ili uangazie makubwa yale yenye umeeleza. Hapo nitakupatia dakika tano uweze kuelezea hayo maandishi yako. Tafadhali usisome, sisi tutayachukua maandishi yako, tutasoma neno kwa neno, kikomo kwa kikomo. Lakini wewe ukija hapa usitusomee, utuangazie yale makubwa yake. Ukiwa huna maandishi yeyote unakuja kutuzungumzia tu kutoka vile unavyo fikiria, basi nitakupa dakika kumi ili utueleze vile ungetaka. Ningetaka pia kuwaomba kutupa mapendekezo. Ukitueleza tu taabu peke yake vile ziko, wakati mwingine hazitusaidii sana kwenye kuandika Katiba lakini ukitupa mapendekezo yako, useme kama kungefanyika hivi tungesaidika, hiyo inatusaidia zaidi ya yale malalamishi peke yake.

Halafu, ningetaka pia kuwaeleza kuwa una uhuru wa kusema jambo lolote unalotaka kwa sababu hii marekebisho ya Katiba inafanywa kisheria. Ni mambo yenye imekubaliwa, imekubaliwa na Serikali kuwa wakati wetu wa kubadilisha Katiba yetu umefika na tujieleze wote. Kwa hivyo usiwe na hofu na usiogope. Lakini pia, ni lazima tupeane kila mtu heshima zake. Wakati mwenzako anapozungumza, hata kama hukubaliani naye, unyamaze tu umpe nafasi yake ya kuzungumza. Atakapomaliza, nami nitakupa nawe nafasi nawe uzungumze yako ya kukataana na yale yake naye pia atanyamaza akusikilize. Tunaelewana? Kwa hivyo sitaki upingamizi kwenye sakafu.

Na jambo la mwisho, ni kueleza kua usingoje mpaka nikukatishe mara kumi, nakueleza wakati wako umeisha bado unaanza pointi ya tano, nakueleza una dakika moja, uko kwa pointi ya sita, tusiwe na mapingamizi hayo, tupeane heshima kuwa mimi ni Mweye Kiti na kuna watu wengi wanaotaka kuzungumza. Kwa hivyo, tafadhali ukipata nafasi yako, heshimu zile dakika zako fulani na ujieleze ili umpe mtu mwingine naye nafasi ajieleze. Kama tumekubaliana hayo, basi sasa nina fursa ya kwanza ya kuita mzungumzaji wetu wa kwanza ambaye ni Helen Rono wa kutoka Kapsaret Leberio Women Group. Helen, Helen unaonekana una memorandum. Una dakika tano za kuangazia makubwa yalio kwenye memorandum yako.

Helen Rono: Constitution of Kenya Review Commission, wanakamati wengine, members' wenye wamefika hapa hamjamboni wote?

Audience: Hatujambo

Helen Rono: Hamjambo tena

Audience: Hatujambo

Helen Rono: Change tugul. Mbele yenu hapa nina present memorandum ya Leberio Women Group kutoka Kapsaret, that is Eldoret South Constitution, Uasin Gishu District. Majina yangu yamesemwa, naitwa Helen Rono. Kwa sababu ya saa, nimeandika hapa, maybe itakuwa tu points kidogo kidogo nielezee tu, nimeandika hapa majority of the points. Kwa kuongea kwangu nita-mix Kiswahili na English kidogo, sitataka interpretation. Sasa ya kwanza yenye wamama wa Leberio Women

Group waliona ya kwamba kwa Constitution Review wanataka wakue na majimbo type of government at the district level. Tunajua ya kwamba, wamama wengi hatujui Nairobi, sijui wamama wamechelewa wapi, wagenisaidia sana niki-Raise a point. Hawajui Nairobi ni wapi na unakuta vitu vingi vinafanywa Nairobi, ukitaka pengine umefungua business yako unataka kufuata, unaelezwa uende u-register Nairobi na hatujui huko so tungetaka kila kitu kifanywe kwa district level.

La pili, wamama wameonelea ya kwamba election ikifanywa ifanywe kwa secret ballot. Tunajua ya kwamba kwa familia, mzee pengine ameonelea hio nyumba fulani tunaenda kupigia kura na pengine kuna mama amesimama na mimi mama mwenzake nataka kupigia yeye kura. Sasa ingekuwa kwa secret ballot ndio nimpe huyo mama kwa sababu tukipiga na mzee kwa laini moja, mzee atanieleza usipigie huyo mama fulani, hatutaki mama apate nini, apate cheo. So tungeonelea ikue secret ballot during voting time. Lngine wamama wameonelea, point yenye wali-Raise ni violence against women. Tunajua wamama wengi sana kuna hii shida ya rape, sijui kufafanua hiyo kwa Kiswahili, raping

Speaker: (?)

Helen Rono: So, hiyo shida iko sana kwa wamama wengi. So tungeonelea watu wenye wanafanya ama wenye wanavunja hio sheria, wafungwe kabisa, wasiende cell pengine mwezi moja, miezi nne ama mwaka mmoja wamewachiliwa. Tunataka wakifungwa wafungwe kabisa kwa sababu, hata wewe jirani ukikosana na mtu, ukiona huyo mtu akija hapo, hutaki kuona sura yake. Kwa tradition ama kwa kimila, mtu aki –rape-iwa ni vibaya sana, na ukiona huyu mtu, hutaki kumuona mbele yako. Hata kama umemsamehe, ukimuona hutaki, sasa ni vizuri kama mtu akifanya hayo makosa afungwe kabisa, asiwachiliwe kwa cell tena.

Lngine wamama walionelea tena ni percentage. Saa zingine kwa ndoa, hiyo ina-deal na property, mama umeolewa na mzee, mumetafuta mali. Wengi wa wamama wakiolewa, especially kwa Wakalenjin, pengine utakuta tu hiyo kifuli ya nyumba, haitakuwa na kitu kingine, hakuna gari hakuna nyumba nzuri, pengine hata hakuna ng'ombe kwa hiyo boma. Sasa mtatafuta mali na mzee, mumezata mali vizuri, mumezata gari, pengine mumezata manyumba ya ku-rent. Baadaye, mzee unaona bibi wa pili analetwa, unashangaa huyu mzee amepata wapi huyu bibi na hii mali tumetafuta na yeye? Sasa tumeonelea kitu kama hicho kikifanyika, hiyo property igawanywe 75%, huyo mama apewe 75% halafu mzee achukue 25% na akienda kuoza bibi wa pili na aende na 25% property, wamama hawatalalamika sana. Hiyo ndio walionelea sana.

Lngine, wamama pia waliona ya kwamba kuna haya mambo ya property tena kwa nyumba kama title deed. Unakuta wengi wetu, especially kwa Nandis' tradition, title deed iko kwa jina la mzee peke yake. Mama hana mamlaka jina lake liwe kwa title deed ama mtoto yeyote. So tunaonelea ya kwamba kama kuna title deed ya shamba, ikue ina jina ya mama na mzee na pia ikiwezekana mtoto wa kwanza. Hii ni kwamba kuna shida saa zingine inapatikana kwa familia, pengine mzee afariki, mama kupewa hiyo title deed iingie jina lake ni vingumu sana, ama kijana a-inherit hivyo vitu vya wazazi wake hiyo title deed iwekwe jina lake ni vingumu sana. So, tungeonelea hiyo title deed ikuwe kwa majina yote kwa sababu hiyo mali ni yetu yote, ama iko

namna gani wazee?

Audience: (?)

Helen Rono: Hiyo mali ni yetu wote? Eh, kwa sababu kama mali ni yetu wote.....

Com. Salome Muigai: Helen, usigeuze hii kuwa mkutano wa siasa kwa hivyo usiwaulize wenye wanafanya, participants swali lolote. Wewe unazungumzia tume peke yake. You are addressing yourself to the Commission, so please don't have interaction.

Helen Rono: Thank you

Com. Salome Muigai: Yes, thank you very much

Helen Rono: So, tunataka hayo mambo ya title deed ikue kwa jina la mama na mzee, any property title deed kama ni ya gari ikue both ya mama na mzee, kama ni nyumba imejengwa ikue na majina zote. Halafu kuna ingine inaitwa maternity leave, nikisema hivo pengine mama ameenda kuzaa. Kwa kazi tunapewa 60 days, hizo ni siku sitini, uende upumzike unyonyeshe mtoto ndio urudi kazini. So tungeonelea iongezwe iwe 90 days, hiyo ni mieze tatu than 60 days ndio mama alishe huyu mtoto vizuri, anyonyeshe vizuru, akirudi kazini mtoto amepata afya ya kutosha atleast na nguvu ya kutosha. Na hapo pia tunataka wazee wapewe yenye inaitwa paternity leave kwa baba sasa, 30 days. Hizo ni siku thelathini pia hata mama akienda maternity leave pia mzee anaenda paternity leave mwezi moja, ndio saa zile mama anakula, mzee atajua chakula gani mama anatakikana apewe, shida gani mama ako nayo, ndio mama alishwe vizuri na akirudi kazini ama akifanya kazi ya nyumbani vizuri, amepata nguvu ya kutosha

Com. Salome Muigai: Una secondi 30 to wind up please

Helen Rono: Lingine lenye tulionelea pia pengine wamama wengi tunakuta wanapigwa na wazee na wamama wameonelea iwekwe kwa sheria wamama wasipigwe. So wamama walionelea ya kwamba tuwe na village elders halafu hao village elders walipwe mshahara kidogo ndio mama akienda hapo kusema ya kwamba mzee amenipiga, mzee asiende kwa huyu village elder amhonge. So tunataka haya mambo ya kupigwapigwa yakome, ama mzee amwambie mama enda kwenu halafu wataongea na wazazi wa mama kuliko mama apigwe. Kwa hivyo, bado kuna zingine lakini nitapeana, hiyo tu nimejaribu ku-explain kidogo yenye niko nayo. Asanteni sana

Com. Salome Muigai: Asante sana Bi Rono, kabla haujaundoka wacha niwaulize wanatume kama wana maswali kwako. Mimi nina swali moja kwako Bi. Rono, umesema wazee wa kijiji wapatiwe mshahara kidogo. Hawa wazee wa kijiji ni akina

mama ama ni akina baba, ama ni mchanganyiko?

Helen Rono: Ni mchanganyiko, unaweza kupata elder mama ama mzee

Com. Salome Muigai: Mmh?

Helen Rono: Inaweza kuwa mama ama mzee, bora ni village elder

Com. Salome Muigai: Vile wako sasa wamechanganyika?

Helen Rono: Majority ni wazee lakini tunataka wamama wakue pia

Com. Salome Muigai: Okay. Asante sana na asante kwa kuweka your time. Umekua mzuri kwa kutumia time yako. Sasa nataka kumwita Sammy Tarus, Kaptelton Youth. Una memorandum ya kutupatia? Kwa hivyo una dakika tano ya kufafanulia memorandum yako au kuangazia.

Sammy Tarus: Constitutional Review Team, the committee and the members at large, I thank you for this chance. I am going to present the points concerning Kaptelton Youth Catholic Church. The type of Government that we need is federal system-majimbo type. The youth have been having problems concerning their brothers and sisters; especially I am going to talk about alcohol. We find that the youth take alcohol when they are very young and they cannot manage their home. Therefore we give this Government that we would like to lead us, majimbo Government license urban centers to operate from 5 p.m. to 9 p.m. and to operate on weekends alone. Any youth is not allowed to take legal brews. Rural centers to operate at 5 pm to 9pm on the two days of weekends. Village elders be given powers to arrest anyone found drinking during the day.

We should outlaw early marriages and the youth should be given a chance to get married at least 25 years both for the men and for the ladies at 20 years old. The Government should also provide education to the highest level and guarantee employment after education or means to alleviate the youth. That is because most of the youth waste almost three quarters of their time in education and they are not employed. We would like also our Government to reduce the retirement age to at least 45 years to allow for the youth to work also. There should be one-man one-job hence giving chance to most people who are educated to get the chance to work also.

Voters should have power to recall members of Parliament who do not perform. That is we always elect members and MPs and when they enter Parliament they take much time there, not coming back home to help the youth in developing and maybe

support them. In addition, we have a complaint in the allocation of land especially in the forest. We would like the land allocated to individuals to be repossessed and given to the youth because you will find an MP with vast a land almost being given 100 acres and so many Kenyans are poor, which means land allocation goes to the wrong place. We are not allocating the land to the right, to the poor those people who do not have land.

Com. Salome Muigai: You have one minute, have you finished? You have half a minute.

Sammy Tarus: In this Government we would like to have nobody should be above the law, and also the public should review the salary of the MPs not the MPs to review their salary because we should not let a way that somebody will earn more salary while the others are poor. They should have little salary and the rest of the money goes to the public especially we would like to have at least free education and free medication that will.....

Com. Salome Muigai: Thank you very much; I have one question for you. I do not know whether my fellow Commissioners have a question. Okay, I have a question for you; you want people to retire at age 45. How old is the youth, what is the range of being a youth?

Sammy Tarus: At least when you get an ID you are 18 years old

Com. Salome Muigai: Yah

Sammy Tarus: And especially when you have finished school at university level

Com. Salome Muigai: Mnh

Sammy Tarus: At least 21 to 25 years

Com. Salome Muigai: So the youth is from 18 to what?

Sammy Tarus: At least 45

Com. Salome Muigai: At least 45. Therefore, you want them to retire when they are still youths?

Sammy Tarus: No, at least

Com. Salome Muigai: 35

Sammy Tarus: 35, yes

Com. Salome Muigai: So you want the youth to be able to work for ten years and then retire?

Sammy Tarus: No. Because we have the case whereby someone will work, is given 50 years to retirement not 55 but that person will cling to that job for almost even 70 years.

Com. Salome Muigai: Okay

Sammy Tarus: And there is somebody who would also like to work

Com. Salome Muigai: All right. Thank you very much Mr. Sammy Tarus on behalf of the youth. The next, mtu mwenye tutapatia nafasi hii sasa ni Joseph Malakwen for Handicapped Individuals. Joseph Malakwen yuko hapa na sisi? Huyu ni wewe mzee?

Speaker: (?)

Com. Salome Muigai: Ooh, nasome vile kumeandikwa. Lakini karibu Mzee Marakwen

Joseph Marakwen: *Alen tugul ochamegen en kainet ab Jeiso.*

Translator: Nawasalimu nyote kwa jina la Yesu

Joseph Marakwen: *Anendat komakase komie Kiswahili.t*

Translator: Anasema kuwa hafahamu au haelewi Kiswahili vizuri

Joseph Marakwen: *Ko anyu kiiton ne amwae.*

Translator: Sasa anasema

Joseph Marakwen: *ko nyalilda .*

Translator: Ni taabu

Joseph Marakwen: *Kong'eten minginatenyun komaro ng'ung'unyat.*

Translator: Tangu utotoni mwake hajapata ardhi

Joseph Marakwen: *Ko katinye ng'ali noton kong'eten. Kiasamate koyemaitinye tuguk alyajini injiniton niikoita ng'ungu'nyat.*

Translator: Anasema basi tangu wakati huo amekua akiomba na amepata shida nyingi sana

Joseph Marakwen: *Ko anyun kigo nyalilatan agoi.*

Translator: Anasema hiyo shida imemfuata hadi wasasa

Joseph Marakwen: *Ko kiang'eten Kapseret agoi tun awe Baraton.*

Translator: Anasema alitoka Kapseret mpaka Baraton

Joseph Marakwen: *Tuguk che kiatinye kiakwere.*

Translator: Mali alizokuwa nazo alienda zikaisha kule alipohama kutoka hapa Kapseret mpaka kule Baraton, mali yake ikaisha

Joseph Marakwen: *Bas aketuge Kaseret nyayaikasit Tanning.*

Translator: Akarudi hapa Kapseret akaajiriwa hapa tanning

Joseph Marakwen: *Aweke ekosiek tutukin eronon imbaret nekigoita en Turbo*

Translator: Akasema muda mfupi mashamba yakapeanwa kule Turbo

Joseph Marakwen: *Awe anyun oliniton kokikaba sibate imbarenik chatan komanyoru.*

Translator: Akaenda kule kujaribu kufanya pilka apate hio shamba lakini hakufaulu

Joseph Marakwen: *Amun kawe ak ewut puch,makachi che ikaito imbarenik komamuche kogonin.*

Translator: Kumbe ni kwa sababu kama haukupeana kitu kidogo kwa wanaopeana shamba hautapata shamba

Joseph Marakwen: *Anyoru nyalilda kounatan kot awe foresty.*

Translator: Alipata taabu hapo mpaka akaenda msituni

Joseph Marakwen: *Bas koyech kenyit age, kowalak Serikalit kole kakoyait oli ba Burnt foresty en kogoek, maekeba timin.*

Translator: Alipoona amepata shida akaenda Burnt Forest, Serikali ikaona basi shida imetokea kule Burnt Forest

Joseph Marakwen: *Kowalak Serikalit ingunon kole ngunon chitugul ne mi foresty, makemenye foresty age.*

Translator: Basi akatolewa kule msituni upande wa Burnt Forest, Anaibkoi Forest kule akatolewa kwa sababu ya amri ya Serikali

Joseph Marakwen: *Anyanyalilate agoi raini aketuge Kapseret ini kora.*

Translator: Akarudi tena mpaka hapa Kapseret

Joseph Marakwen: *Nguni anyon ami Kapseret aripchini chito tisok.*

Translator: Ako hapa sasa Kapseret akichungia mtu mali yake

Joseph Marakwen: *Amun ine ne ribbon ngunon ak konegit koalwan ingoraik, Lagok che kiatinye kigoyesta konyalilat.*

Translator: Basi yeye ako kwa mtu sasa, anafanyia mtu kazi amejiriwa, yeye ndie anamlisha. Watoto aliowazaa wote wameenda kwa sababu ya shida, wametapakaa

Joseph Marakwen: *Kianyoru nyalilatan arawet ab oeng' kenyit konye.*

Translator: Alipata shida hiyo mwezi wa pili mwaka jana

Joseph Marakwen: *Komian lakwet chepto.*

Translator: Mtoto wake akawa mgonjwa

Joseph Marakwen: *Komian any komapetyo che anyaan.*

Translator: Akawa mgonjwa akashindwa kumtibu

Joseph Marakwen: *kobetwon tuk chanyaen amuten sipitali.*

Translator: Akakosa pesa za kumtibu

Joseph Marakwen: *Kanam borwechu eb Ukimwi.*

Translator: Ugonjwa huu wa ukimwi ulimkamata

Joseph Marakwen: *kowendot agoi kobarchi Turbo.*

Translator: Akaenda mpaka huyo mtoto akaaga kule Turbo

Joseph Marakwen: *konam polis ingunoton koib Konyo Moi Referral Eldoret.*

Translator: Basi alipokufa kule, askari polisi wakaleta mpaka hapa Moi Referral

Joseph Marakwen: *Komakibarwon kele kagokeskei lakweng'ung' kakonyo Eldoret.*

Translator: Basi akafahamishwa kwamba mtoto wake ameaga na mwili uko hapa Moi University mortuary

Joseph Marakwen: *kokianyawe*

Translator: Basi alipoenda

Joseph Marakwen: *Ko kitebenon akichek kelenjon indei chi ngung' yu*

Translator: Akaambiwa basi utatafuta mahali pa kuzika huyu mtu wako

Joseph Marakwen: *kokibetwon olandai chichoton.*

Translator: Basi alikosa mahali pa kuzika

Joseph Marakwen: *Agoi awe kapkirwagik.*

Translator: Akaenda kwa ma-Chief

Joseph Marakwen: *Kogiib kosirwan baruet kole ib kowa olimba mortuary, Matinye chichon kiy age tugul.*

Translator: Hapo Chief akaandika barua kule mortuary akaambia huyu mtu hana mahali pa kuzika huyu aliyeaga

Joseph Marakwen: *Ako kiwekwon chumbechoton che mi mortuary kolenjon wui kapassistant chief sikosirun baruet ko konin permit.*

Translator: Basi akamuambia huyo mzungu aliyehudumu hapo katika chumba cha kuhifadhi maiti. Akamuandikia barua akamueleza “rudi kwa Assistant Chief akuandikie permit”.

Joseph Marakwen: *Kokin kegonon permit, anyokachi chumbek choton kaba mortuary.*

Translator: Alipopewa permit na huyu naibu mkuu, akaja akapeleka hiyo permit kwa yule mkurugenzi wa chumba hicho cha kuhifadhi maiti

Joseph Marakwen: *Ko kiit koyan bichoton ko zikan chichoton.*

Translator: Basi hao watu walikubali kuzika huyo

Joseph Marakwen: *Agot ingunon mang'en kaburinyin.*

Translator: Hadi wa sasa hajui mahali huyo mtoto wake alizikwa

Joseph Marakwen: *Ko nyalildanyun natinye kou natan*

Translator: Shida yake ni hiyo

Joseph Marakwen: *ne rubei neb a oeng'*

Translator: Ya pili

Joseph Marakwen: *Ko ane koma a Nandin i.*

Translator: Yeye ni Mnandi

Joseph Marakwen: *Konitan Katiba ne kamache anyun, ko a Nandin anyun kabisa.*

Translator: Basi kwa sababu Katiba imefika yeye ni Mnandi kabisa

Joseph Marakwen: *Kit ake tugul ne kiyae koyayagse kounatet mawalaksei.*

Translator: Kile Wanandi wanafanya ibaki hivyo na isibadilike, mila za Wanandi zibaki hivyo na zisibadilike

Joseph Marakwen: *Kounaton kong'eten keny agoi raini.*

Translator: Iendeleo vile ilivyokuwa tangu zamani hadi sasa.

Joseph Marakwen: *Kounata anyun matinye che chang'.*

Translator: Yeye hana mengi ni hayo tu

Joseph Marakwen: *Kongoi missing.*

Translator: Asante sana

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Marakwen,

Speaker: (?)

Com. Salome Muigai: Tafadhali msaidie Mzee kujiandikisha na ningetaka kueleza kila mtu, ukimaliza kutupa maoni yako, tafadhali jiidikishe pale ili tuwe na record yako kuwa ulikuja mbele ya tume na tulikusikiza. Sasa namuita Daniel Simoto, Citizens Common Forum

Daniel Simoto: Asante sana ma-Commissioners na wananchi wenzangu ambao tumekuja hapa kutoa mapendekezo. Jambo la kwanza ambalo nitaanzia kwa sababu nimetengeneza a written document ni kwamba nitasema tu zile tunaita salient features. Kwanza ninapendekeza tukuwe na Serikali ya uBunge ambayo tunaita Parliamentary system of Government. Na hii yangu si ile wanasema eti tuwe na hybrid kama vile tunasikia wanasema ili kujipatia mamlaka ya ku-divide, mimi napendekeza a pure Parliamentary form of Government ile inaitwa West Minister. Ya pili kuhusu hiyo ni kusema ya kwamba hata ingawaje tutakua

na hiyo pure Parliamentary form of Government, tuwe na a limited term of office kwa sababu tumeona hata Prime Minister wanaweza wakakaa kwa ofisi kwa muda mrefu kwa kutumia njia zisizofaa. Nina kwa mfano kama yule Prime Minister wa Malaysia, ni vizuri anaenda kwa retirement, lakini he has been in power for a very long time. Kwa hivyo mimi ninapendekeza awe na 2 terms of 5 years each na kwa sababu hio hali ya West Minister huwa Serikali inaweza anguka wakati wowote, kwa hivyo itakuwa ni aggregate, kama ameanguka halafu akapigania tena akachaguliwa, ikisha fika ile aggregate ya ten years, anaenda nyumbani.

Ya tatu kuhusu hiyo Serikali pia, unaweza pata ya kwamba inaweza kuanguka wakati wowote kwa hivyo itakuwa kila wakati Serikali ikianguka, Parliament wana-elect, sio ati kuenda kwa general elections. Hata kama imeanguka, Parliament wanaambiwa waende wa-elect, sio kusema eti yule leader of the largest group in Parliament ndio wata-form Government sio automatic namna hiyo, ni Parliament wanaenda wanaelect MPs wenyewe through secret ballot. Halafu ya pili ni kwamba hiyo Serikali itakua ni ile tunaita federal ama majimbo, watu wengine wanaita majimbo. Hiyo Serikali, kutakua na Serikali kuu halafu kutakua na Serikali kwenye mkoa, halafu viletunaona mikoa yetu bado ni kubwa sana na kuna makabila mengi, kwa hivyo bado tutakuwa na Serikali nyingine katika wilaya. Badala ya kuwa na PC ambaye anatumwa na Rais kutoka kule juu, tutakua na mtu ambaye amechaguliwa, an elected person to be in-charge of what is going on in the province. Halafu badala ya kuwa na DC ambaye hatujui ni nani tunashtukia tu tunaona DC na hatujaambiwa ndio huyu DC, basi tutakuwa na DC ambaye amechaguliwa na watu through direct voting kwenye District level. Yule sasa tunaita DC ambaye ni civil servant, sasa huyu anaweza kuwa ni District Secretary ambaye anatekeleza mambo ambayo ni matakwa ya watu wa sehemu hio.

Tutakuwa na, katika hio Serikali ya district, tutapata ya kwamba ma-councilor ambao wanatoka kwenye Serikali za wilaya kadhaa katika hio district, all the local authorities within a district ndio wata-constitute hiyo Bunge ya hiyo Serikali ya hiyo district. Kwa hivyo all the councillors ingawaje watakua kwenye council zao kama ni municipal, county council, town council, watakuja kuangalia mambo ya district ili tusiwe na Chief ambaye anasemekana ni Chief. Chief sasa atakua ni a civil servant ambaye anaweza kuwa transferred from here to there.

Katika the lowest unit ya Serikali tutakua na village elders ambao watachaguliwa, sio tena wale wamekua appointed kama tunavyo ona kwa sasa. Na mimi napendekeza kila polling station iwe na, it is considered to be a village so every polling station itakuwa considered ni village na wata-elect a village elder ambaye atakuwa na mshahara. Nafikiri hiyo nimesema, nimefafanua juu ya hiyo hali ya majimbo. Kuna kitu kingine ambacho watu wengi wanahofia juu ya majimbo, kwa hivyo tutasema ya kwamba, ingawaje kuna hizi autonomies lakini Serikali kuu itakua na uwezo wa kung'oa Serikali yoyote ya jimbo kama ita.....

Com. Salome Muigai: Daniel, una dakika nyingine moja

Daniel Simoto: Okay, halafu tena la pili, tutakua na Bunge ambayo tunaita bi-cameral Parliament. Tutakuwa na upper house

na lower house. Upper house itaangalia maneno ya makabila na madistrict na lower house itakuwa wanachaguliwa kutoka constituencies ambazo ziko sawa kwa wingi wa watu na wale wanaopiga kura. Judiciary tutakuwa na supreme Courts na kwenye kila mkoa kutakua na High Court.

Halafu ningependa kusema juu ya Constitutional supremacy. Hii Katiba itakuwa inabadilishwa, itakua ya watu wa kenya na njia ya kubadilisha ni kwamba lazima Bunge zote mbili zikubaliane kwa two thirds majority, a half of all the provinces itakubaliana kwa two thirds majority katika Legislature zao na districts. A half of all the districts in every province lazima wakubaliane namna hiyo. Katika hii wilaya yetu tuna specific demands, ya kwanza tunataka boundaries ya wilaya ya Uasin Gishu irudi mahali ilikuweco 1963 tukipata uhuru. Pili, tunataka sasa tukiwa na district Legislature ndio itachagua wale ambao watakua board members wa National Cereals and Produce Board, Kenya Dairy Board, Cotton and Lint and Seed marketing Board, we have textiles here, that is why I am saying that

Com. Salome Muigai: And your time is over sir

Daniel Simoto: Yes, asante sana, nafikiri mtapata all the details kwa hii proposal naleta hapa

Com. Salome Muigai: Kuna maswali kwa Bwana Daniel, Mr. Ratanya? Asante sana Bwana Daniel Simoto, mwenye atatuzungumzia sasa ni Bwana Francis Sitienei.

Francis Sitienei: Hamjamboni

Audience: Hatujambo

Francis Sitienei: Basi, maoni yangu inasema mambo ya Katiba. Kwa maoni yangu mimi nataka, mimi nasikia kuna mtu *Kiagas kele mi chito ne maname sheria.*

Translator: Anasema kwamba katika Katiba ya Kenya kuna mtu ambaye ako juu ya sheria

Francis Sitienei: *Ko kounatan koamune si manam sheria chito kongeten meto agoi ngweny.*

Translator: Basi anasema Katiba ya sasa isiwe na mtu ambaye ako juu ya sheria

Francis Sitienei: *Konoton ne kere kikoim ng'alek ab emet.*

Translator: Hiyo ndio imekua chanzo cha shida katika taifa hili

Francis Sitienei: *Amun ndakiganam chitugul ng'atutiet*

Translator: Kama sheria ingeweza kufikia kila mtu

Francis Sitienei: *ka kararan emet.t*

Translator: Nchi ingekuwa nzuri

Francis Sitienei: *Ko kounatan amwae alen ng'alek ab judges*

Translator: Anasema basi kwa upande wa mahakimu

Francis Sitienei: *Ko kiagas kele ngerinen.*

Translator: Anasema ni wachache

Francis Sitienei: *Amune sikong'erinitun oko kigosoman*

Translator: Anasema kwa nini mahakimu wakawa wachache na watu wamesoma?

Francis Sitienei: *Ko kounatan ko siokere ng'atutik makobendi koiku ma.*

Translator: Kwa hivyo anasema hiyo ndio inafanya kesi na hukumu zisiwe ni za haki katika taifa

Francis Sitienei: *Amun igere chito imuch koyai tuguk che yachen.*

Translator: Unapata wakati mwingine mtu anafanya maovu

Francis Sitienei: *Ak mutai kenam*

Translator: Kesho anashikwa

Francis Sitienei: *Kegere komi gaa.*

Translator: Muda mchache unamuona akiwa nyumbani

Francis Sitienei: *Kiwano ukweli neba emet.*

Translator: Ukweli wa nchi ulikwenda wapi?

Francis Sitienei: *Kimache keyaien ukweli kila kitu.*

Translator: Nasema ukweli na haki ufanywe katika mahakama

Francis Sitienei: *Konatan ne akere koimi bik.*

Translator: Hiyo ndio inatusumbua

Francis Sitienei: *Amache ng'alek ab chamaisiek amache ane kochang'a.*

Nandi dialect

Translator: Nasema basi kwa maneno ya viama, anakata viwe vingi

Francis Sitienei: *Sababu ingo chang'a,*

Translator: Vikiwa vingi

Francis Sitienei: *Kowa emet kokaranit.*

Translator: Nchi itaenda vizuri

Francis Sitienei: *Amun kikigere ngot ko akenge ko umisanech bik alak*

Translator: Na naona wakati wa chama kimoja, kilitatiza na kiligandamiza watu wengi

Francis Sitienei: *Ko ng'unon ko kararan ko chang'a.*

Translator: Yeye anasema kwamba anataka viama vya kisiasa viwe vingi

Francis Sitienei: *Asiko ribech.*

Translator: Ndio ipate kulinda

Francis Sitienei: *Ketinye tabut akenge ng'unon.*

Translator: Yeye akiongea hivi sasa anasema wako na shida moja

Francis Sitienei: *Amun kolul olniba KFA ole kitam kotareti wanainchi.*

Translator: Yeye ni mkulima lakini mahali walikua wakiuza mimea yao kama KFA iliokuwa ikiwasaidia

Francis Sitienei: *Koki keibech.*

Translator: Imeenda

Francis Sitienei: *Kou KCC*

Translator: KCC iliyokuwa ikinunua maziwa

Francis Sitienei: *kokikeibech.*

Translator: Ilienda

Francis Sitienei: *Ko kounatan ko kibano bik che kiribe yekinye.*

Translator: Basi wale watu walikuwa wakichunga walienda wapi?

Francis Sitienei: *Neba somok*

Translator: La tatu

Francis Sitienei: *ko ehek Nandiek.t*

Translator: Ndio hawa Wanandi

Francis Sitienei: *Ko ng'alekyok ko kichopyoso komatelejin kirwok.*

Translator: Kimila haikuruhusu mama kusimama mbele ya wazee

Francis Sitienei: *Oko kimakekanye muren.*

Translator: Na hio hakuwa hata ana hiyo roho ya kuweza kusimama mbele ya wanaume

Francis Sitienei: *Ke mache ketebi kou atkinye.*

Translator: Anataka basi hiyo amri ya zamani irudi

Francis Sitienei: *Amun ma baiwech chepyoso.*

Translator: Kwa sababu kimila hakuna wakati mama anaruhusiwa kutawala

Francis Sitienei: *Neb a ag'wan,*

Translator: La nne

Francis Sitienei: *Ko mila ne nyon komi*

Translator: Kulingana na mila za Kinandi, watu hupashwa tohara

Francis Sitienei: *Neba loo*

Translator: La sita

Francis Sitienei: *Komi ng'aliot nebunu Kanisa.*

Translator: Kuna jambo la dini au kanisa

Francis Sitienei: *Amun bik kotekse.*

Translator: Kwa sababu watu wanaendelea na ujenzi

Francis Sitienei: *Ko natekse ko sponsoreni kanisosiek*

Translator: Basi wakati wanazidi kujenga kuna sponsorship ya makanisa

Francis Sitienei: *Komi kaniset ne sponsoreni sukulit*

Translator: Unapata kanisa ambalo lina-sponsor shule lingine

Francis Sitienei: *komago kachin chit one kitech kocher rabinikyik*

Translator: Haipei nafasi mtu aliyejenga, aliyetoa pesa zake

Francis Sitienei: *kolenjin sis metinye kiy nekere ne ya*

Translator: Anasema wewe nyamaza usiongee hata kama kuna jambo mbaya hapo

Francis Sitienei: *ko ngunon komi ano ukweli.*

Translator: Anasema hapo basi haina ukweli

Francis Sitienei: *Ara anyun matinye che tian.*

Translator: Anasema yeye hana mengi

Francis Sitienei: *Kale maatinye che tain*

Translator: Hana mengi

Francis Sitienei: *Kagoyam choton.*

Translator: Yeye amemaliza hapo

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Francis Sitienei, umetueleza mila ya Kinandi haikubalishi mama kusimama mbele, lakini MP wangu wa kwanza kuona mama alitoka hapa Eldoret. Ni kweli?

Audience: Ndio

Com. Salome Muigai: Yes, kwa hivyo mila zetu zinaendelea kukua, sio kuwa zimekaa tu lakini zinakua. Lakini tutaendelea kwa kumuita Madam Everlyne Maiyo. Everlynne Maiyo

Evelynne Maiyo: Okay, kwa majina ni Evelynne Maiyo, I am from the Kenya Women Political Cocus, Uasin Gishu District. With me, I have a memorandum but I am just going to read through some few highlights then I will submit the copy. One of the key areas I am going to talk about is the health sector or the area of health. We find that in Uasin Gishu basically, we have dispensaries but they are very few. Most of the times we don't have medicine or even the personnel, we could be having only

one nurse and no doctor at all, so there is a problem in the health system in this district.

Secondly, education: in the area of education, we find that we advocate for a free and compulsory primary education for everyone because in this area most of the times because of the poverty we find that sometimes they opt to educate the boys. There is a gender bias there when it comes to the education system in this area. Another area is the issue of inheritance, we advocate that in future in this Constitution it could be impossible, yah that is our view, that the issue of inheritance be addressed equally. Men and women if there is any property, each should get an equal share whether it is a girl or a boy that is not an issue, it should be equal for all the gender.

The system of Governance, we would wish for a system in which there is equality for all and we propose that 35% of the seats be reserved for women because in the current system there are very few women. Women are not represented yet they are the majority of the population in the country. Another area is citizenship; we advocate for automatic citizenship whether you are born, there is usually bias for a woman married to a foreigner. We see the men are always given the upper hand when it comes to the issue of citizenship.

Employment, which is another key area where we have a problem. We advocate that there be guaranteed employment for each and every Kenyan. Then the issue of the vulnerable groups in society like women and children and the disabled, we find that most a times their problems are not addressed at all. We have no schools; like in this area, we have very few schools for the disabled. Okay, another area in the Constitution; we find that the current Constitution is basically in English. We want it demystified to be written in the local languages so that people can understand, and read, and get to know what is in the Constitution. I think that is all I have, thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you very much Everlynne Maiyo. Are there any questions? There are questions for you, just come back.

Com. Ratanya: Everlynne

Everlynne Maiyo: Yes

Com. Ratanya: There is one point for clarification. You have stated that we should have free and compulsory education. Do you indicate the level that is it from standard one to university or what levels?

Everlynne Maiyo: The primary level, primary school

Com. Ratanya: (?)

Everlynne Maiyo: I think that is the key area

Com. Ratanya: (?)

Everlynne Maiyo: To university I think

Com. Salome Muigai: Excuse me, while Everlynne Maiyo is talking, she is addressing the Commission, so the rest of us wait until we have a chance to address the Commission so I.....

.....*End of tape 1 Side A*

Com. Salome Muigai: Are recommendations and proposals. And there is something else again that you just told us that, just a moment, you also said that there are no schools for the disabled

Everlynne Maiyo: Yes

Com. Salome Muigai: But you did not give us a proposal. What would you like to see done.

Everlynne Maiyo: Okay, about the health sector, I propose that those (?) be managed by the locals. I think it should be managed by the locals where they train them, they have their own people trained and they work within the same environment. And then to do with the disabled I think there should be a Government directive, as in they should be assessed. Okay, I think it should be from the budget, be allocated some amount so as to build schools for such people. Because if we rely on NGOs and the religious community, I think it will not work. I think the Government should do something about it.

Com. Salome Muigai: Thank you very much Madam Maiyo. The next person, mtu mwingine mwenye nitasikiza sasa ni Bwana Gilbert Kimani Nyumu, Senior Citizen Welfare Association.

Gilbert Kimani Nyumu: Asante bwana Commissioners

Com. Salome Muigai: Na Bi Commissioner pia

Gilbert Kimani Nyumu: Na Bi. Commissioner

Com. Salome Muigai: Asante

Gilbert Kimani Nyumu: Asante. Yangu niko na memorandum na kwa hivyo nitachukua muda ile mtakuwa mumenipatia. Na mimi nitaendelea

Com. Salome Muigai: Kwa dakika tano

Gilbert Kimani Nyumu: Kwa dakika tano hizo.

Sasa ya kwanza, mimi nataka kupendekeza kwamba Katiba mpya wakati wa kuandikwa iwe na kile kitu kinaitwa utangulizi that is Preamble. Na hiki kitu ningependekeza kwamba mupate mfano wa Uganda pengine ufuatwe, sitaki ku-elaborate hapo.

Namba mbili ni kwamba political parites, vyama visiwe zaidi ya vitatu. Nikimbie?

Halafu ya tatu, katika High Court zote za Kenya tuwe na kile kitu kinaitwa legal aid kwa sababu watu wengi wanatatizwa katika kisheria, na ukienda kuchukua advocate inakua ni pesa nyingi kwa hivyo tunataka katika High Court zote za Kenya tuwe na pahali watu wanaweza kusaidiwa na mawakili bila kulipa pesa yoyote.

Kitu cha nne ni katika electoral system and process, ili tupate mtu ambaye ameshinda katika uchaguzi ama President ambaye ameshinda katika uchaguzi, napendekeza ya kwamba awe amepata 51% ya kura zote ambazo zimekuwa cast na awe na 25% kutoka kwa provinces tano.

Ya tano, napendekeza kwamba, kwa sababu Katiba ya sasa haina specific, haina tarehe kamili ya uchaguzi mkuu, napendekeza Katiba mpya iwe specific kwa kuweka tarehe ya uchaguzi. Kwa sasa Katiba inasema ni baada ya miaka tano, sasa inaweza kuwa ni mwezi wa pili ama ni mwezi wa December ama ni January. Sasa iwe specific.

Lingine ni kwamba katika uchaguzi wa mwaka huu, kura zihesabiwe katika kituo ambacho watu wametupa kura na hayo mambo yakwishie hapo. Pendekezo lingine ni kwamba kitu ambacho tumekwisha ona kwa campaign zilizokwisha ni kwamba the incumbent President na chama chake wanatumia mali ya Serikali. Katika Katiba mpya nimependekeza kwamba hiki kitu kisikubaliwe kutumia public funds wakati wa campaign ya chama. Kitu kingine napendekeza ni kwamba Katiba mpya isikubalie mtu yeyote awe na zaidi ya acre hamsini.

Kitu kingine ni kwamba there should be an expanded public service Commission of Kenya, na iwe ni moja tu kiliko sasa tuna Commission nyingi ambazo zimeleta mambo mengi sana, mambo ya strikes, kwa sababu kila Commission inapigania mambo ya mshahara wa watu wao. Tukiwa na hiyo Public Service Commission moja, we shall remove ambiguity, tuta-remove discrimination in remuneration awards, tuta-promote efficiency and order in the public service.

Kitu kingine napendekeza ni kwamba Bill of Rights. The Bill of Rights must be passed into law without exception. Hii ukiangalia ni kwamba kuna hivi vitu vinaandikwa katika Katiba halafu sheria nyingine inawekwa inatoa hiyo haki ya mtu.

These are mystifications in the Constitution and the current law, iwe removed in the new Constitution. Kitu kingine, the outgoing

Com. Salome Muigai: Hebu dakika moja, tafadhali excuse me, the people arranging chairs, please take notice that we are

trying to tape these proceedings live, so all the noise that gets on the way also gets taped. So lets try to keep background noises as minimal as possible. Tafadhali tujaribu kuweka kelele chini kwani haya maneno yote tunazungumza tunanasa kwa vyombo vya kunasa sauti na hizo kelele za kutoka nyuma pia zinasikika. Asanteni, endelea na una dakika moja

Gilbert Kimani Nyumu: Outgoing and all retiring Presidents should be guaranteed security on condition that he is not going to engage in active party politics. If I now come to the senior citizens, me being one I recommend that Section 112 of the Constitution, 124 and 125 of the Constitution be overhauled because this are the areas where the senior citizens, the retirees are denied economic justice. Along with that, the law associated with pension should be overhauled that is 189, 185, 195, 190 and so on. Na ni hayo tu mabwana Commissioner na bi Commissioner

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa kuweka wakati wako, nitawauliza wanatume, mna swali kwa Bwana Nyumu? Asante sana Bwana Nyumu na sasa mzungumuzaji wetu atakayefuata ni Robert S. Kiama

Robert S. Kiama:Asante sana Commissioners, tumefika kwa mualiko wenu. Ni vyema mumetupatia wakati mzuri. Ningelitaka kuuliza nisikizwe tu kwa mambo machache mafupi yanayohusu mambo ya retired civil service personnel. We have civil servants who have retired and they retired prior to the salary increases most of which came around 1980 upto 1983 I think so that the new salary scales....

Com. Salome Muigai: Please speak into the mic Mr. Kiama then it gets recorded

Robert A. Kiama: Okay

Com. Salome Muigai: Yes, thank you

Robert S. Kiama: The rates of pension are dependent on the salaries in terms of time, yes and of course the rates of paying. Then those who retired earlier were working in the Government at the old salary scale rates. The conversion that yields the pension pay per month for retirees is very seriously in disfavour of the old retirees who left prior to 1984,85,86. Consequently, we have alot of old people, me included and it has been very dissappointing to receive in what they call in the Americal language peanuts for so long, whereas those who have worked in the same grades after 1986 have enjoyed reasonably better pay in terms of pension than those who retired prior to the increases. I am asking that the retirees be accorded due consideration that the new Constitution does take the trouble and see the goodness in the staff who have done Government work which I like to equate, honorable commisioners to like a share in what ealier on in a company which is still performing and performing well. In addition, I do believe Kenyan Government has done very well but the benefits are not going to the retirees accordingly so the older fellows should receive respect and payment to suit.

I am asking also that the matters that pertain to pension for the families of the retired persons in this item called Widows and Children pension plan be reviewed accordingly. Because I will surprise you honorable Commissioners that I have witnessed somebody going to ask for assistance, because he is retired, his wife was very sick almost dying and he was asking whether that money that is in the pension fund can be used to cater for payments of bills for the sick wife. The answer was ridiculous, I am sorry to say because the response by the offices was quick that you must be dead before any payment is made. So it is inappropriate in society today, it is indeed inhuman. We would want to ask that these benefits be handed over perhaps to a more commercial oriented authority like the RBA, which should manage and yield dividends for the retirees accordingly which should cater for some of their needs in terms of sickness or any other problems. This should be paid to the retirees as per request or as per the defined program. Today, nobody knows what happens to the WSCP because it is not brought to their attention and nothing, I have never seen anything, I retired in 1978 and I have not seen anything any document sent to me to inform me. Thank you very much

Com. Salome Muigai: Thank you very much Mr. Kiama, you are very focused on the issue you wanted to talk about. Any questions? No question. Mzungumzaji wetu sasa ni Beatrice Cherono wa kutoka Sombentai Womens Group

Gilbert Bor: Madam Commissioner ningependa kutangazia wote kwamba ukishika microphone, utaje jina lako maana linashikwa na tape before you start the presentation

Beatrice Iris Cherono: Thank you Commissioners and the panel at large. Thank you for giving me this chance to present my proposals. My names are Beatrice Iris Cherono, I am going to present a proposal from Sobentai Women Group, Eldoret South Constituency. I will start first with the structure; I will address the Constitution directly before I start with the specific women issues. The first one is the structure and system of Government. We propose that the system of Government be adapted should be either Parliamentary or Presidential system. The President to be directly elected by the electorate, the President to be a member of a political party, the President to be the head of the state. A Prime Minister's post should be created, a Prime Minister to be appointed by the President from the majority. The Prime Minister to appoint Ministers, Prime Minister to be head of Government. We also propose that a Senate to be set up and.....

Com. Salome Muigai: Beatrice, if you try to read it at a supersonic speed, we will not be able to hear you and we will not be able to take notes because you are very fast.

Beatrice Iris Cherono: Okay.

Com. Salome Muigai: What I suggest that you do, is look at the things you can talk into, a few of them, yes and leave us to read the memorandum

When we go to the Judiciary, we need a Constitution that will give the Judiciary power to deal firmly with corruption and to give each and every person his or her rights. When we touch on human rights we say that we should have the right to clean water. People of Kenya really need good water wherever they are. We should also have right to developments. We should have developments wherever we are, good roads and so forth. We should have right to land, we should have right to live with alot of dignity as a human person, and also we should have freedom to settle everywhere in Kenya, freedom to do business anywhere in Kenya, freedom to work everywhere in Kenya. So when we touch on our financial aspect, we say that we shall also be told when the Government is acquiring a big loan, and when the loan is coming in and how it is used. We find ourselves paying alot of debts from our monetary institutions without knowing how they came in or how they were used.

Then in our civil service we say that if a civil servant retires, actually, he should be given his benefits immediately, but here is the case that we see that after retirement, you are again not given your benefits and maybe you will die even without a single cent after you have worked for a long time for the Government. We say about trust land, we should be very much transparent in issuing title deeds and a good law should be enacted to make somebody who has acquired a title deed be once and final, not being transfered here because of money. We are touching also on cultures, we need a constutitoin that will actually protect good cultures of our people and also to promote them. We also say that we need a Constitution that will enhance the good relationship between our country and the foreign countries to give us good investments in our country to create more job opportunities.

We feel that the towns are becoming very thickly populated, so we need a Constitution that will enable the Kenyans to have factories and industries in our rural areas, so that people don't come and actually be, a lot of people to be in town at one place. So we feel that the town is made by the industries. Wherever there are industries, people will automatically be there. So I am very pleased that the much we have written in this memorandum you will take time and read it. Thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you very much Mr. Omollo, sasa ningetaka kumuita Mzee Kibet Chepkwony. Mzee Kibet Chepkwony.

.....*End of tape 3 side A*

Joseph Chepkwony: *Kainenyun ko Joseph Kibet arap Chepkwony.*

Translator: Jina ni Joseph Kibet arap Chekwony

Joseph Chepkwony: *Ane ko a mengindet neba Langas.*

Translator: Yeye anaishi Langas

Joseph Chepkwony: *Ko olekiabunu siamenye Langas,*

Translator: Kabla ya kuja Langas alikuwa akiishi

Joseph Chepkwony: *Ko kiamenye Kaptalat.*

Translator: Kaptalat

Joseph Chepkwony: *Yan kilelen Kapkechui.*

Translator: Kwa jina ya sasa inaitwa Kapkechui

Joseph Chepkwony: *Ko kingebwan yu ke al.*

Translator: Alipokuja kununua hapa

Joseph Chepkwony: *ko mi ra chito ne isumbuanech ok one kikiale tugul*

Translator: Hadi wa sasa kuna mtu anawasumbua na walinunua hili shamba pamoja

Joseph Chepkwony: *Chichoton ko kile kaistegei konam tugukyik ak kowa.*

Translator: Huyo mtu alisema kwamba anataka kutoka, anahama na akachukua mali yake akaenda.

Joseph Chepkwony: *Koe kaistegei chichoton .*

Translator: Huyo mtu alisema ninahama

Joseph Chepkwony: *Ak kikilibanji tugukyik.*

Translator: Na alipewa vitu vyake

Joseph Chepkwony: *Angkoret anyun*

Translator: Shamba

Joseph Chepkwony: *Kotam aalde ne nyun.*

Translator: Hadi wa sasa yeye hajauza lake

Joseph Chepkwony: *Kiangen nyalida ne kiba ubeberu.*

Translator: Yeye alielewa shida alizokumbatia wakati wa ubeberu

Joseph Chepkwony: *Ubeberu ko kinyalilenech kirebenech tuga.*

Translator: Wabeberu waliwanyaganya mifugo

Joseph Chepkwony: *Anga kika kibauge kele kakopunjech emani,*

Translator: Na juzi tulipopata uhuru

Joseph Chepkwony: *Ko nyo arap malel koal koranaton kigi menye.*

Translator: (?) Akaja akanunua shamba walilokuwa wakiishi ndani

Joseph Chepkwony: *Noto kilen Kapkechui.*

Translator: Hilo shamba linaitwa Kapkechui

Joseph Chepkwony: *Kole mache ch I kiy nyin.*

Translator: Kasema basi kila mtu atafute jasho lake

Joseph Chepkwony: *Ko kigibwan yu keal, kikibwan bik somoku.*

Translator: Sisi watu watatu tulikuja tukanunua

Joseph Chepkwony: *Keal imbaranoton- Langas.*

Translator: Wakanunua hilo shamba

Joseph Chepkwony: *Agoi ingunon tom kenyoru Tittle.*

Translator: Basi hadi sasa hawajapata title deed, cheti cha kumiliki shamba hilo

Joseph Chepkwony: *Ko ngunon koimech bik, komache kole kimache rabisiek alak.*

Translator: Sasa wamesumbuliwa kwamba pesa zingine zinahitajika

Joseph Chepkwony: *Ama kingen ole bunu rabisiechoton.*

Translator: Na hawajui mahali watapata hizi pesa

Joseph Chepkwony: *Ak kenyalidosi.*

Translator: Na wako na shida sasa

Joseph Chepkwony: *Nyalidos lagokyok.*

Translator: Hata watoto wetu wana shida

Joseph Chepkwony: *komangen anyun ale amune asi komwa chito kole amache rabisiek ogo kigoib tugukyik.*

Translator: Na sijui ni kwa nini huyu mtu tena amerudi kusema kwamba anataka pesa na alikuwa amelipwa hapo mbele

Joseph Chepkwony: *Amwae ale kongoi matinye ng'al che tian.*

Translator: Anasema asante, hana mambo mengi.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee. Mzee Phillip Kiprono?

Phillip Kiprono: Naam. Mimi ni Phillip Kiprono kutoka side ya Langas. Asante sana tume kwa kuja kusikiza maoni. Kwangu ni kuendelea kama vile mnajua, mimi ni Mnandi, sikusoma na sikuelewa Kiswahili lakini nikiteleza, lazima kunyorosha kwakuandika. Jambo moja wananchi, ameumba dunia na mbingu lakini ameumba miti na mto, bahari chochote ambacho ameumba ni Mungu, lakini kwa nini kuharibu mazingara na Serikali yetu kuharibu mazingara? Na mazingara ni kitu ambacho wewe ukitoa leo usafi wako, utapata watu, na kwa nini kukata miti bila kupata mvua?

Baada ya hayo, kuna wasichana siku hizi wanaleta aibu nyumbani kwetu kutembea uchi kwa sababu wakivaa nguo ambayo imekunjana mpaka naona aibu. Basi, unajua kiumbe ya kabila yetu nyeusi ni kama mtu ameumba na kuja kabisa kunenepa, na msichana akivaa nguo ile suruali amevaa tight inakua aibu kubwa kwa sisi wazazi.

Baada ya hayo, sisi tunalemea kodi yetu kama hapa Uasin Gishu, kodi yetu imelemewa kwa sababu sijui pesa ya kodi inaelekea

wapi? Baada ya hayo, watoto kusoma hakuna. Mtu ambaye kama mzazi anatupa mtoto wake, kwa nini watoto wanachoma shule, unatoka wapi? Ingefaa kutenganisha watoto, upande wa Eldoret lazima watoto wao wasome halafu tunajua wenye kutoa taabu hii ni watoto kutoka wapi?

Kufuatana na hayo, shamba mtu anategemea mali yake, mali ya mtu si ya mtu mwingine kukuja kukalia na kudanganya, kupeleka na kumuambia pesa iko na ukipeleka mahindi mahali sokoni anaenda kutorosha au kuwacha hapa kwanza ili yule ataabike bila kusomesha mtoto. Kufuatana na hayo, Serikali sasa nataka kuendelea kuanzia degree kuwa majimbo na ikiendelea mpaka province kuwa majimbo, halafu kufika province lazima kujua kutekeleza mambo ambayo itapata faida kutoka kwa district yoyote ambayo province inatawala. Na huko province tutajua sisi wenyewe kama governor kuendelea mbele, mimi naona tangu kupata uhuru, je Rais lazima kutumikia miaka kumi au tano ikiona anafanya kitu kisichotosheleza binadamu ni lazima akae kuliko kusema na sitaki mtu.

Kufuatana na hayo, je kwa nini kuandika watu kama Eldoret (?). Imefika kuandika watu wa kufanya kazi na picha. Weka ndani ya nyumba na kuficha huko. Zamani nilikuwa naona vijana wamechagua wanaenda mlolongo, kuona kweli watoto wameenda. Mtoto (?) Kama location amepata kijana moja, (?) imepata vijana wawili ama ngapi? Sasa siku hizi wanaficha na kupitia njia ya magendo. Baada ya hayo.....

Com. Salome Muigai: Mzee una dakika nyingine moja

Phillip Kiprono: Eh?

Com. Salome Muigai: Una dakika nyingine moja

Phillip Kiprono: Basi moja ni kuomba kwa wananchi wasinyang'anye mtu haki yake, lazima kujua. Na maskini, mbona kiwete hawezi kupata usaidizi? Ya pili, mbona maskini amezingara, mbona wameleta pombe halafu inaleta ukimwi maana pombe ni hatari kwa usalama? Weka pombe mpaka saa kumi halafu watu hawawezi kuenda kupata ukimwi. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana mzee, sasa ningetaka kurudia list yetu ya kawaida na nimuite Daniel Rotich. Daniel Rotich?

Daniel Rotich: The Commissioners, ladies and gentlemen thank you. My name is Daniel Rotich and I am representing Kapserit Village Group. First, I will just try to go point by point. The group feels that Republic of Kenya should change from unitary Government,

Com. Salome Muigai: Just give me one moment. Ninaelezwa kuwa niliposema wazee waende nje ni kina *boiyo* peke yake

walienda nje. *Gogo* bado wako ndani, kama wewe ni mama mzee tafadhali jiandikishe. Nilitaka akina mama na akina baba

Daniel Rotich: Thank you, this village group is actually men and women and they feel that the Republic of Kenya should change from unitary Government to federal state. That each state to be headed by an elected governor and this could also replace the provinces and we will have the state instead. The district to be headed by district attorneys, that is the feeling, and preferably the attorneys from their respective community. Some of the Presidential powers should be transferred to the governors, and they feel that the key ministries like Foreign Affairs, Finance Security, Tourism, Judiciary, Auditor General to remain in the federal republic but ministries like Agriculture, Social Services, and Local Government to remain under the governor.

On law pertaining to debts and corruption, we feel that stealing or embezzling of the public money, the public officers or the civil servants should be made to pay back the money or imprisoned, or both, instead of being transferred to another institution to mess it up as the case has been. The issue of trust land, the group felt that the land should be protected and preserved in the Constitution and if need be, later on if the Government feels like sub-dividing that land, the indigenous groups should be given the priority and the elders of that community should have a bigger say in that division.

Land control boards should be chaired by indigenous elders not the courts as we have been seeing. On finances, this group felt that the federal republic shall be required to consider population needs when it comes to the consolidated funds, sharing of the consolidated funds. For the Executive powers, the group also felt that the President should be at least a degree holder, that is on education. He should be over 40 years of age or over, and at least have served as an MP for two consecutive terms prior to being elected to be the President. They also felt that the councillors should at least be 'O' level education, should have an 'O' level education. On succession, the group felt that the incoming President should assume office three months after the Presidential elections, and the Constitution should make provision for a former President in terms of security, welfare, and immunity from legal powers.

Com. Salome Muigai: And now you have one more minute.

Daniel Rotich: Thank you. On the rights of vulnerable groups, the group felt that a widow should have the right to choose who to marry instead of being inherited as is practised in some communities. If she remarries and decided to come back she should not come back with other children. However, if she leaves, she leaves the children in that original home. The state should also provide for homes for the elderly and the vulnerable groups in terms of health and security. Finally, because of time, the public officers or civil servants should be required to declare their assets. Thank you very much.

Com. Salome Muigai: Thank you, now can we have Reverend James Kosgei. Reverend James Kosgei?

James Kosgei: Yes. Jina ni Reverend James Kosgei, natoka sehemu za Karafalls sehemu za juu. Yale niko nayo ni machache. Jambo la kwanza ni President atakaye ongoza nchi ya Kenya: President awe na terms mbili za miaka tano kama atachaguliwa, awe na terms mbili za miaka kumi. Hitimu yake, umri aweze kuanzia miaka 40 na mwisho ni 75. Awe amewahi kwenda Bunge, pia asipatikane kuwa na makosa ambayo inahusika na corruption wakati mwingine awe hajashitakiwa kuhusu corruption. Kwa kupigiwa kura, awe amepata aslimia tatu katika mikoa zaidi ya tano au kama provinces za Kenya ni nane awe amepata aslimia tatu au 70% kwa mikoa kama tano ndio aweze kuongoza nchi.

President asiwe na sehemu yake ya Bunge kwa sababu akiwa na sehemu yake ya Bunge kila mara hatashughulikia Kenya nzima, atashughulikia sehemu yake. Huyu President asiwe above the law, asiwe juu ya sheria zote, aweze kushitakiwa kama amefanya makosa baada ya kuhitimu miaka zake hizo tano, aweze kushitakiwa.

Councillors; Councillor cheo chake ikiwezekana awe ana 'O' level na zaidi. Chairman wa county council ichaguliwe na wananchi. Mayor pia achaguliwe moja kwa moja na mwananchi. Jambo lingine ambalo nahitaji nigusie ni kuhusu elimu. Elimu ya primary hasa wazazi waende waweze kujenga mashule lakini elimu ya primary iwe 100% imegharamiwa na Serikali, na shule ziwe equipped, ziwe na vitu ndani yake. Kwa hivyo hiyo ni kusema mtoto asome. Afya.

Com. Salome Muigai: Dakika moja Bwana Kasisi

James Kosgei: Pole. Afya iweze kufikiriwa na iwekwe na nafasi nzuri sana kwa afya katika Kenya. Kuo na kuolewa, mume ikiwezekana, mume au mke ikiwezekana waweze kurithi, mwenzake akikufa hakuna mtu atakayeingilia kati yao. Iwe mjane au si mjane, mtu wowote asiingie katikati bali awe akirithi mwenzake awe akirithi mali ya mwenzake. Kama ni kuo mke zaidi ya mmoja, wote waolewe kirasmi, kisheria wawe wakiolewa kirasmi. Hii itabidi kila moja, kila mama apate haki ya mume wake. Mwisho, katika hali ya kuandikisha usia, kwa mfano kama Kalenjin kama Nandi, customary law ifuatwe au ifanywe upya kwa Katiba iliyoko, kwa sababu Nandi customary law hakuna mtu atakayechukua mali ya mjane ila ni mwenyewe, mke ndiye atakaye chukua. Nafikiria kwa ufupi ni hayo nimekuwa nayo.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Kasisi. Sasa ningetaka kuipa hii nafasi kwa Bwana P. K. Waweru..

Peter Kabiru: Commissioners na wazee wenzangu ningependa ku-summarize points zangu kwa dakika moja tu. Kwanza kabisa

Com. Salome Muigai: Anza na jina lako tafadhali.

Peter Kabiru: Jina langu ni Peter Kabiru Waweru. Tuna watoto wengi sana wanarandaranda mtaani, Constitution yetu ilinde hawa watu. Ya pili, uBunge, watu wapewe Wabunge kulingana na nambari ya watu sio kulingana na area-kama Eldoret hii

tungekuwa na Wabunge wanne watano hivi. Point yangu ya tatu ni kwamba hii central administration ya kuwa na DC ya kuwa na PC, Permanent Secretary, governor hivi, hiyo ni maneno ya Lord Lugard ilitokezea karne ile nyingine kwa sababu alitaka kukula nchi hii. Viongozi wote wachaguliwe, hiyo system ya ma-DC, ya nini ikwishe.

Ya mwisho, rhythm ya election ya nchi hii isikue changed na Constitution iwe ni writtern Constitution sio hii ya kusema leo hivi, kesho hivi. Tulianguka sana wakati Mzee Kenyatta alikufa na hatukupewa nafasi ya kuchagua kiongozi. Sasa Mzee Moi amekuwa mzee na wanataka tusichague kiongozi tena. Rhythm ya elections isikuwe changed na mtu yeyote. Mahali tumeangukia sisi watu wa Kenya, wakubwa wakienda huko wanasema ni wakubwa, nani aliandika hawa kazi, si ni raia? Kwa nini tulipe kodi ya kulipa DC, tulipe kodi ya kulipa Chief, tulipe kodi ya Mbunge, hii ni system mbili. Sisi tunaumia sana huku mgogoni kubeba mizigo miwili.

Com. Salome Muigai: Bwana Waweru,

Peter Kabiru: Asante

Com. Salome Muigai: You are addressing the Commission

Peter Kabiru: Asante sana Commissioner

Com. Salome Muigai: Asante

Peter Kabiru: Tunataka mzigo wa mwananchi ipunguzwe, tunabebe mizigo mizito sana. Kodi tunalipa, tunalipa system mbili tunafuata mzungu na mzungu alitaka kukula sisi ovyo. Asante sana

Com. Salome Muigai: Asante sana sasa ningetaka kumpa mzee mmoja Salome Phillip. Salome Phillip? Mama mmoja mzee anaitwa Salome Phillip.

Salome Phillip: *Chamge tugul.Kongoi missing en nafasi kokonan siang'alal ra.*

Translator: Anasema anashukuru kwa nafasi ambayo mumempa nipate kuongea

Salome Phillip: *Kigurenon Salome Philip.*

Translator: Anasema majina ni Salome Phillip

Salome Phillip: *Aba location neba Kapseret.*

Translator: Anatoka Kapseret

Salome Phillip: *Atinye kenyisiek Sabini ak Tisap.*

Translator: Ana miaka 77

Salome Phillip: *Anan kasir angwan, mangen isine komie.*

Translator: Hana uhakika lakini huenda iko hata zaidi ya hiyo.

Salome Phillip: *Amun masoman.*

Translator: Kwa sababu hakusoma

Salome Phillip: *Namwae missing kongoi en Serikalini asobwan okaswech rirekyo.*

Translator: Anasema anashukuru sana kwa sababu mumekuja hapa kusikia malilio yetu

Salome Phillip: *Kamwa ale missing ne kakechagua che bendi Bunge, ak ke bendi nyalilida si maker bik che kigue kole une, tepta ano.*

Translator: Anasema amesikia uchungu hadi akaja hapa kwa sababu tunachagua Wabunge, tukisha wachagua wakifika kule wanasahau wale watu waliowachagua.

Salome Phillip: *Ki kue iman koteben ng'echeret ne ngowek kowiskee.*

Translator: Akienda kule anapata kiti kikubwa ambacho kinazunguka na kuviringika

Salome Phillip: *Amatakobwat kole ng'o ne kikwaan siateben ng'echeraniton.*

Translator: Lakini hajui ni nani aliyemchagua kuja kwa hicho kiti.

Salome Phillip: *Kalyan si kekonech keswek che ma keswek?*

Translator: Kuna shida pia ya mbegu, tunatengenezewa mbegu ambazo sio mbegu

Salome Phillip: *Kaige yon kakinech kerichek che kakinde chokaa, siki lekenen kerichek ab bek.*

Translator: Wakati tunapewa madawa ya mimea tunapewa chokaa ambayo imepakwa rangi tu na tunadanganywa.

Salome Phillip: *Kitinye ngwanindo missing.*

Translator: Tuna uchungu sana

Salome Phillip: *Amakase bik che ba Bunge.*

Translator: Na Wabunge hawatusaidii kwa vyovyote vile

Salome Phillip: *kimwae kele saisai, ye kakomwa Nandi kole ingotep Nandi kou ye kinye komotwa.*

Translator: Anasema mila zipate kuhifathiwa vile ilikuwa tangu zamani

Salome Phillip: *Mache kotep Nandi kou ye kiu.*

Translator: Mila za Wanandi zipate kubaki vile zilivyokuwa

Salome Phillip: *Si ingo michepyoso konyin, Kou ye kigemwa en Nandi kele ingotep chepyosok kotebie kounaton.*

Translator: Tangu zamani mama alikuwa na jukumu lake na alikuwa akifuata kazi yake na jukumu lake ndani ya nyumba.

Salome Phillip: *Okot inguni ko Baisyechuchoket ko makergei ak lagochuchoget amun makikachi sheria ne kiyame.*

Translator: Anasema hadi wa sasa kuna mivurugano ndani ya nyumba kwa sababu zile sheria za kitamaduni zimetolewa. Rika yao wali.....

Salome Phillip: *Igere lakwet ne kamang', ne katalelen iyoo anan karget kole daddy,fathee anan mathee.*

Translator: Anasema vijana siku hizi badala ya kusema baba au mama wanasema 'daddy', 'fathee' au 'mathee'

Salome Phillip: *Kokibut ng'atutik che makikas komie.*

Translator: Anasema sababu ya jambo kama hili litokee ilikuwa kupuuza kimila

Salome Phillip:*Ara kakimwa Nandi kele kotep ng'aliot ne unatan ne kagekonok okwek omite gaa ireyu oye mobut okot akenge.*

Translator: Anasema mambo ambayo tumewapa ninyi Commission musifute hata moja, muhifadhi na mututekelezee shida zetu.

Salome Phillip: *Ara mamache amwa che tian.*

Translator: Anasema hana mengi

Salome Phillip:*Agase ko ngwan en ng'alechutan.Kongoi.*

Translator: Anasema anasikia uchungu kwa mambo hayo, asante.

Com. Salome Muigai: Halafu mama mwingine wa pili ni Leonida Kambia. Baada ya huyo mama nitampa nafasi Christopher Mitei kwa hivyo ukae tayari na Luka Kuto.

Leonida Kambia: Nashukuru sana kamati ya tume kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu kuhusu Katiba. Mimi kwa majina naitwa Leonida Kambia, natoka mtaa wa Hill School na ni location ya Pioneer. Katika uchaguzi wetu kufuatana na hii

Katiba iliyoko, tulikuta ya kwamba mengi hayakuongezwa na ni mambo kama vile mnaona tukiangalia hiyo Katiba haina utangulizi, kujua inalinda nani na haimlindi nani. Wanasema mwanaume peke yake hawakumbuki mwanaume anakaa na mwanamke. Kwa hivyo hapo tuliona ni kosa. Tukifuatilia tena tunakuta ya kwamba hiyo Katiba haikuruhusu wamama kugombea viti vya Bunge. Ni huruma tu ambayo waliokuweco kwa utawala walianza kuonelea kwamba wamama wameanza kujitokeza na kuwapa nafasi ili waweze kuingia katika siasa. Ndio mwaka wa 1974 waliweza kuweka tu wamama wanne peke yake kwa Bunge na tunaona ya kwamba kwa sababu sisi wote tunaenda shule, tunaelimishwa kisawa na tuna uhuru katika nchi yetu, tungependa vile elimu iko sawa tena uwakilishi wa uongozi uwe sawa kwa sababu mama tena ana lake la kuchangia pahali panainama.

Tukiangalia tuliona ya kwamba haikumkumbuka mama kuwa raia mkamilifu, kwa sababu akiolewa na mgeni anaambiwa hama nchi yako enda ukaishi mahali mume wako anatoka. Na ilhali yule mume ana nafasi ya kununua shamba Kenya na aishi hapa na huyo mtoto wa Kenya . Kwa hivyo tuliona ya kwamba tumebaguliwa na kwa hivyo wajaribu kurekebisha hapo. Mjaribu kurekebisha hapo. Tuliona ya kwamba tumedanganyika kwa upande wa ndoa. Wenzetu wanatudanganya tumeolewa

Com. Salome Muigai: Tafadhali ningetaka kuomba pale nyuma tuwe na utulivu ndio tumsikie mama

Leonida Kambia: Tulikuja kugundua ya kwamba tumedanganywa muda mrefu na wakati huu ni wakati wa kila mmoja kuchangia katika maendeleo. Tumedanganywa zaidi katika ndoa, mara nyingi ndoa tunaambiwa tumeolewa na mtu, unakaa miaka ishirini, arobaini hata unakufa kabla ya kujua ya kwamba umeolewa, hauna certificate ya marriage, hauna yaani utambulizi kwa huo ukoo. Wakati mume wako anakufa, urithi unaenda tu kwa watu wa ukoo wa hapo. Hatutambuliwi kurithi mali ya waume zetu na hiyo tunaona ya kwamba ni dhuluma kwa wanawake.

Kwa hivyo tulipendelea ya kwamba ikiwa mtu anaamua ya kwamba anataka kuoa, mtoto msichana ajichunguze na aone ya kwamba ako miaka 24 na kuendelea, aolewe na mvulana naye awe na miaka zaidi ya 30 aowe. Na kuhadharisha ndoa zao ikiwa ni ile wanaita come-we-stay, kuanzia mwaka moja wawe wamewasilisha matakwa ya kuwasilisha ndoa yao, ili kila mmoja aishi akijua ako na haki ya kuishi katika sehemu anayoishi. Tena tulichambua tukasema ya kwamba katika urithi wa mali ya boma inatakikana tuandikishe mali yetu yote kwa majina mawili. Registration of properties, tuandikishe majina ya mama na baba ama bibi na bwana kwa mali ya boma yote ili kila mama awe na haki. Tulisema ya kwamba katika familia, mzee anataka kuuza sehemu ya mali ya boma, mama ashirikishwe kujua ya kwamba mali inauzwa na apewe sehemu ya mauzo isiwe ni kwa mfuko ya mzee peke yake, hapana.

Tuliona pia tulisahauliwa wakati wa mwanaume kutaka haja zake. Mwanaume ana haki ya kuoa vile anapenda kwa sababu hatujui ni nini kinamsukuma lakini tulisema ya kwamba wakati anataka kuowa mwanamke wa pili, wakae na bibi wake wa kwanza kwa sababu walianza kwa carton chini, sasa wakae wazungumze ya kwamba ninahaja kwa sababu ninaona mali imekuwa mingi na itaharibika. Kwa hivyo nataka mke mwingine, wakae na jamii, hiyo jamii impe ruhusa tumeona kweli una

mali ya kutosha kulinda wanawake wawili. Agawe hiyo mali ampe mwanamke wa kwanza mali yake na hiyo mali inabaki anaweza kuoia nayo bibi mwingine lakini atunze tena watoto wa bibi wa kwanza. Na akitaka bibi wa tatu tena azungumze na bibi wa pili ili agawe mali yake. Wakati atafilisika, ajue kikomo ya kuoia imefika. Tumesema ya kwamba tunataka kuzuia mambo ya watoto wa nje ya ndoa. Hawa watoto inatakikana washugulikiwe kwa njia yake. Ikiwa ni mzee ambaye amekuwa na tamaa ya kutafuta mtoto nje, atambulike kwa huyo mtoto kuwa baba yake na atunze huyo mtoto mpaka amalize shule hadi university, asimutupie mama tu.

Vile vile tulisema ya kwamba tusiambiwe ya kuwa wanawake ni watoto, hilo jina wafute kabisa kwa mawazo yao, ya kwamba mwanamke tena si dhaifu sana ambaye hawezi changia maendeleo. Tupewe nafasi yetu tufanye maendeleo bega kwa bega na waume zetu. Ni hayo tu, Mungu awabariki.

.....*End of Tape 3*

Com. Salome Muigai: Asante sana mama, ningetaka kuomba hali ya kunyamaza na kupeana heshima za kusikilizana. Ikiwa wewe ulipozungumza watu wale wengine walinyamaza wakakusikiza na wakati mtu mwingine pia anazungumza sasa wewe hutaki kusikiza. Hiyo sio hali ya kutengeneza Katiba. Katiba ni wakati wa kuzungumza sote pamoja na kupeana kila mtu heshima zake ili sote tuchangie nchi nzima, sindio? Kwa hivyo wakati mtu mmoja anapozungumza ningeomba wengine tunyamaze. Jambo la pili ni kuwa nimewaeleza mara kwa mara kuwa tunanasa sauti. Tukienda Nairobi na hizo kelele hatutasikia vile watu wa kikao cha Bunge cha Eldoret ya kusini walivyosema. Kwa hivyo tafadhali habari ya kuzungumza wakati mtu mwingine anapozungumza, tupungue kabisa. Na sasa ningetaka kumuita Christopher Mitei.

Christopher Mitei: Commissioners, utangulizi uwepo katika Katiba mpya ya Kenya, ukianzishwa na maneno 'We the people of Kenya....' kuonyesha kwamba Katiba ni ya wananchi na ya kwamba maono ya nchi, maadili na filofia kama sovereignty, secular, democratic, be a enshrined in the Constitution together with the philosophy of justice, liberty, equality and fraternity. Also katika utangulizi ama Preamble, honor for all those who suffered for justice and freedom in our land and respect for those who have worked to build and develop our country.

Pia kanuni za sera, kanuni za kuongoza sera za dola ama directive principles of state policy ziandikwe pia katika Katiba mpya ili iwe kielelezo pia kwa Wabunge wetu ambao wanafanya mambo mengi katika Parliament bila muongozo. Basi, supremacy ya Constitution pia iwepo kwamba when we ammend our Constitution procedures na principles za the independent Constitution ziwekwe pamoja. Tuwe na sehemu mbili katika Katiba mpya, special entrenched provision ambayo tukitaka kubadilishi tuwe na idadi ya 75% ama referendum kwa wananchi wahusishwe, halafu ordinary provisions iwe Wabunge wenyewe wanaweza kupitisha kwa simple majority.

Tuangalie sehemu za vyama vya kisiasa, the Constitution should regulate the formation and management, and the conduct of political parties. We need two to three political parties. Pia, ofisi ya mkuu wa, ama leader of opposition, should be entrenched

in the Constitution with the necessary facilities and manpower. Structure and system of Government, vile tumekuwa na Serikali ya umoja, unitary Government, wametulet down, hebu pia tujaribu hii ya majimbo ama tunasema federalism, tuone kama itaweza kutusaidia wakati huu kwa vile tunajua unitary Government is service delivery is quite poor.

We want to try this federalism to see because the Government is so close to the people, tukae nao. Katika Bunge, tuwe na two houses, upper house na lower house. Upper house tuwe na wakilishi wawili katika kila mikoa na zile Bunge za majimbo pia zikuwepo. Pia, key positions in the Government should be vetted by the Parliament, and the people of Kenya should be given power to recall non-performing MPs. Pia coalition Government ikuwepo, Serikali ya mseto, Katiba ifafanue ya kwamba ikiwa chama fulani kinataka kuunda Serikali, lazima wawe na nusu ya viti katika Bunge na wasipojaza waende wafanye vikundi wakutane na waunde Serikali, wakishindwa tukuje tena kwa kura. Haya ningesema pia maneno ya salaries za Wabunge.

Com. Salome Muigai: Excuse me, una dakika moja Mr. Mitei kwani una memo to give us, so you have one minute to summarize.

Christopher Mitei: Okay, mishahara ya Wabunge wakipitishi ziwe kwa the next Parliament, sio wenye wako sasa na Judiciary: I concur with the opinion of those experts who came to assist the commission wakiwa na Chairman Bwana Kayamba wa South Africa. Halafu pia tuwe na mambo ya electoral Commission, tarehe ya uchaguzi iwekwe katika Katiba ili isiwe siri ya mtu mmoja. Basic rights na fundamental rights under fundamental duties zikuwepo. Halafu land, agricultural land, consent ya community at least wakuwe na sehemu yao. Environment, waweke sheria ya kila mtu akiwa na shamba apande miti fulani.

Nikimalizia, community wapatiwe sehemu maalum kuchunga misitu. Mwisho, nimesema fundamental duties. Naamini mutasoma kwa vile hakuna nafasi. Currency ya Kenya isiwe na picha ya Rais yeyote, tuweke maneno ya maybe milima yetu, wanyama wetu, tusiwe na picha za watu, na flag ya Kenya pia iwekwe katika Katiba ni hayo yote. Asanteni sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Mitei. Sasa ningetaka kumpa hii nafasi Bwana William Kurgat, Mzee William Kurgat. Mzee William Kurgat....

William Kurgat: Asante sana. kwa majina mimi ni William Kurgat kutoka upande wa Kipkenyo. Nina machache, kwa sababu mengi, nimekuwa nimejitayarisha lakini mengi yamesemwa na wananchi, kwa hivyo singalitaka kurudia tena, isipokuwa nina mambo mawili. Mambo haya ambayo nitasema ni mambo ya mahakama, mambo ya kortini. Mambo ya kortini ni kwamba watu wanashitakiana kortini ama wanashtakiwa na wanaweza kuchukua muda mrefu sana.

Kabla sijasonga ni kwamba kulikuwa na watu watatu ambao walinunua shamba na walikosana kwa shares. Hawa watu watatu walienda mahakamani na wakachukua miaka kumi na nane. Kufikia miaka kumi na nane, tayari watu wawili wameaga dunia na akabakia tu mtu mmoja. Sasa watoto wa wale watu wawili ambao waliaga dunia wakitaka kuanza kesi, ilikuwa ni ngumu sana

maana hawakujua vile shamba ilinunuliwa, kwa sababu ilinunuliwa kama walikuwa watoto wachanga, walikuwa hawajajua.

Kwa hivyo hata sasa ninazungumza hapa, hiyo shamba bado haijamalizika kortini. Ninasema tume ya uchunguzi, tafadhali tuweke kiwango cha kesi, kwa sababu kesi inaweza kuchukua miaka ishirini na watu wanaweza kupoteza haki yao. Wale waliaga dunia na yule amebaki, tayari watoto hawa wa marehemu wawili wamepoteza haki ya baba zao. Kwa hivyo ni uchungu, hata nilisikia mama mwingine alisema hapa anaongea kwa uchungu. Hata mimi pia naongea kwa uchungu. Wengine ambao wamefika hapa tayari wana mambo kama hayo labda, kwa hivyo ningesema ya kwamba kesi ianzie nyumbani kwa location. Ikiwa ni mashamba, ianzie kwa location mahali pale, wazee wachaguliwe ambao ni waaminifu, waanze kesi ya mashamba huku ama kesi yoyote inayohusu watu wale wanakaa mahali pale. Hilo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili ni mambo ya elimu. Elimu kwa wakati huu imekuwa ngumu sana, ni kama hospitali, kwa sababu tayari watoto wa form four wakati huu wako nyumbani na wana matarajio ya kufanya mitihani. Kwa hivyo ingawa wako kwa shule, hawatapita mitihani hio kwa sababu wamefukuzwa shuleni walete karo. Kwa hivyo ninapendekeza ya kwamba elimu ianzie standard one bila kulipa mpaka wamalize form four. Na wakati hawa watoto wanasoma wakianza standard one mpaka wamemaliza form four, watakuwa tayari kufungua account yao ili kujitayarisha. Nilisema mpaka wamalize standard eight. Tayari wamemaliza standard eight, watakuwa wamefungua account hapo mbeleni kuweka pesa ya kujitayarisha kwa elimu ya juu. Kwa hivyo nikimaliza ya kwamba, nursery school iwe ni ya wazazi. Sina mengi ya kuongeza isipokuwa tu nilitaka kuongeza ya kwamba sheria isiwe tu kuna mtu mwingine hawezi kuenda kortini. Kama tumetengeneza sheria ya kuhukumu mtu, inahukumu hata Rais mwenyewe. Kwa hivyo mimi sina mengi ila ninasema ya kwamba sisi sote twende kortini.

Nikiongeza kidogo kwa sababu nimezungumza kwa muda mfupi, ni jambo hili la corruption. Wengi wanazungumza, hata ukiwa kwa gari unasikia watu wanazungumza mambo ya corruption. Mimi ningetaka kusema wale wangemaliza hii corruption, wao wenyewe ni (?). Kwa hivyo (?) hawezi patia isipokuwa wale ambao wamewekwa kuangalia sheria, wao wenyewe wamekuwa watakatifu kabisa na wanaweza kuzima haya maneno ya corruption. Kwa hivyo tume ya uchunguzi, ningesema nitamalizia hapo na asante kwa kuweka nafasi hii nzuri kila mtu aweze kuzungumza.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana William Kurgat, tafadhali, Bwana Joseph Maiyo yuko?

Joseph Maiyo: Ndio

Com. Salome Muigai: Joseph Maiyo, karibu mzee. Na baada ya Joseph Maiyo tutapata Bwana Sospeter Mwangi, kwa hivyo jitayarishe pahali ulipo.

Joseph Maiyo: Joseph Maiyo kutoka hapa Tuiyo location ya Kapseret. Tunauliza mambo ya (?). Wazungu walitusumbua kutoka zamani, wakanyakua huko Kapsabet halafu hao wanatufukuza sisi (?), halafu juzi wanaamuka, wanasema rudi nunua

shamba. Sisi tulinunua na sasa inakuwa majimbo ya leo, hii nchi ya Nandi.

Tena, tunataka maji iletwe Kapseret kusaidia Serikali, na pia sisi na kazi ya maji kule nyumbani. Maneno ya cereal board, kwa mahindi, tunazunguka kila mwaka na hatuoni namna gani. Serikali itaangalia namna gani, sisi tunaomba Serikali iangalie cereal board, kuweka mahindi mbili mbili namna hii, KCC imepotea, kila mahali imepotea na Serikali iangalie namna hiyo. Hii ifanye namna hiyo na maneno mengi haitoshi, inatosha sasa nimewaambia. *Kongoi.*

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee kwanza kwa mawazo yako hayo mafupi. Mzee Sospeter Mwangi. Mzee Sospeter? Mzee Sospeter?

Sospeter Mwangi: (?)

Com. Salome Muigai: Jina lako ni Sospeter?

Sospeter Mwangi: Eh, Mwangi

Com. Salome Muigai: Mwangi?

Sospeter Mwangi: Ndiyo

Com. Salome Muigai: Basi hilo ni jina lako

Sospeter Mwangi: Sijui kama mimi nitajua kuongea (?) sijui kama mimi najua kuongea na (?)

Com. Salome Muigai: Kwanza mzee uongee na hiki kidude kikiwa karibu na mdomo wako

Sospeter Mwangi: Ehe

Com. Salome Muigai: Ndio tuweze kunasa sauti yako

Sospeter Mwangi: Oh.

Com. Salome Muigai: Karibu, angalia yangu

Sospeter Mwangi: Majina yangu ni Sospeter Mwangi na mimi naishi hapa miaka mingi. Nilikuja hapa 1925, upande wa Maji

Mazuri. Na sasa mimi nimekuja hivi mpaka Kipsinendet, hapa Eldoret. Na mimi ni mmoja wa wale walifukuza mzungu na nilifukuza mzungu ndio tukae vizuri, tule vizuri, lakini sasa mimi sioni. Sasa kitu kile mimi nasimama hapa, na musikie maneno yangu, ni tukae vizuri tuungane, tuwe kitu kimoja. Tuweze, raia aweze kujua tutaishi namna gani kuliko, sasa mnakimbilia maneno mengine. Chukueni hawa wajumbe na mkubwa wetu anataka ku-retire. Sasa ata-retire namna gani na sisi bado kukaa vizuri? Vile mimi ninasema, mchague yule mtu anaweza kuongoza sisi na msichague mtu tajiri, na msichague mtu mnono namna hii, hapana. Hapana chagua huyo, chagueni yule mtu ambaye yuko na akili halafu aongoze Kenya mzima.

Kitu moja mimi nimesikia hapa leo, nimesikia mwingine amesema anataka majimbo, Kenya ni ndogo sana na tukiwa na majimbo, sisi wote tutakufa tuwaachie wazungu Kenya hii. Na wazungu wanataka kurudi hapa na nyinyi mnataka kuwarudisha hapa. Kama ni majimbo, mimi nitakua njaa, wewe uko na mali na huyu yuko na mali, na mimi sina mali. Sasa mimi nitakufa njaa na wewe unakula nyumbani. Hapo ndipo mimi nakataa majimbo, maanake sisi tutakwisha wote, hakuna mtu atabaki, maana mwingine ana nguvu na mwingine hana nguvu. Sasa vile mimi nataka, ni (?) kitu kimoja vile Kenyatta alisema, tuungane. Wewe huwezi kunifukuza na mimi siwezi kukufukuza, tutakuwa kama ndugu na dada halafu tukae vizuri. Hiyo majimbo nyinyi mnataka sasa tukae ati huyu anasema shule, huyu anasema nini, chagueni hawa wakubwa wote. Kama tumewachagua wakubwa wote tunaona yule mtu atatuongoza, tukae chini tumuambie vile sisi tunataka. Lakini kama bado hatujachagua mtu, sisi hatuna hali nzuri. Na mujue mimi Kiswahili yangu ni ya mama Njeri, kila mtu ajitambulie.

Sasa mungoje wachaguane. Kama bado kuchagua, kitu kimoja, hakuna (?) mingi na hakuna kidogo, (?) kitu moja na wachague yule mtu mzuri, hapana shauri ni tajiri na hapana shauri ya kunona, hiyo mimi nimekataa. Na mimi sina mengi ni hayo tu peke yake

Speaker: *Thie haria muthee*

Sospeter Mwangi: *Ni wega .*

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee, hicho Kiswahili cha baba Njeri pia kimejieleza na asante sana kwa kuzungumza maneno machache. Luka Kuto. Luka Kuto?

Luka Kuto: My names are Luka Kuto, I am a resident at Race Course. My proposal to the Commission is that the Preamble must be people owned. Constitutional supremacy; Parliament must not be allowed to decide on Constitutional matters alone. People must have a right to say anything that touches on the Constitution.

Political parties; we must have a body that the Constitution must regulate. Political parties must be limited to 2. Executive; Executives must be qualified people and have academic proven records. The President must be 40 years to ascend to that office and the limit age is 65. He/she must be married and with a stable family, sound morals, must declare his or her wealth.

Local Government; Mayors and Councillor must be elected by people. Qualification is 'O' level, must have sound morals, declare wealth and married with stable families. Basic rights, I am proposing to the Commission that people with 85 years of age must be exempted from taxation. Also, Constitution must be made in such a way that it must be taught in school and any learning institution.

Education; our education in Kenya is not of any use to us at the moment. I am proposing that our Government must provide room for all professionals so that they can assist the wananchi, because the wananchi are paying alot of taxes to these people so that they can acquire their education. That is the much I had, thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you very much Mr. Kuto that was precise. Mr. Francis Abdaka? Abdaka, Francis Abdaka Abdasa yuko? David Simbolei.

David Simbolei: Commissioners na wananchi wote, mimi pia nitazungumuza Kiswahili changu pia ni kama cha mzee aliyemaliza kwamba nitazungumza lugha yangu pia ya (*Nandi word*). Basi, langu la kwanza ninataka..... Jina langu ni David Simbolei, natoka location ya Sirmat. Yangu ya kwanza nitazungumza juu ya afya. Mahospitali yetu hapa Uasin Gishu district yana shida sana. Ningependa Serikali ichukue jukumu hilo maanake inaonekana hata stakabadhi ya wananchi wa hapa kwa ajili ya wagonjwa: mgonjwa anaweza kutibiwa kwa siku fulani na baadaye waki-discharge ama akifariki ile bill yake iko juu kabisa. Inakuwa ni kama 50,000 ama karibu 100,000 mpaka inaweza kushinda wale jamaa. Kwa hivyo wanauliza walete stakabadhi yake ya shamba waweke kule ili waongojee pesa.

Pili, yangu pia ninataka kuzungumza juu ya masomo juu ya elimu. Kwa sababu, ningependa masomo iwe bure kutoka primary hadi form four. (?) Ya haya, sisi tunaweza kupata masomo hata tunaweza kuwapoteza wale watoto ambao hawana mitihani saa hii kwa sababu hakuna elimu. Sasa watoto wanatembea kule na mnaweza kuona wale wanaitwa chokora, wanaweza kuchukua kinyezi ya mtu ili wapate pesa. Wanaweza kumuekea mwingi ama wanaweza kuuliza mtu mzima namna hii, usipo mpa pesa anaweza kukutupia hiki kinyezi. Kwa hivyo hii inaleta aibu nchini mwetu. Tafadhali Serikali ichukue jukumu la elimu mpaka hawa watoto wapate kusoma.

La tatu ninachangia pia upande wa ukulima. Wakulima wanateseka sana hata ikiwa ni kulima, nikipata mahindi na chakula chochote cha mashambani, unakosa hata mahali pa kuuza vizuri. Ni vizuri hii soko huru (?) ndio wakulima wanaweza kupata mahali watauza mapato yao. Unaona hata maziwa, hata nikiwa mkulima nifuge ng'ombe wa aina gani, nikikamua maziwa kiasi gani, ninakosa hata mahali pa kuuza maanake soko huru inatawala. Ukifika town fulani unakuta maziwa inatoka ng'ambo, unakuta mahindi inatoka ng'ambo, kunatoka kila kitu. Hata mayai siku hizi zinatoka ng'ambo. Mayai yetu sisi tungeuza shilingi tano unarudi mpaka shilingi mbili. Kwa hivyo ni vizuri Serikali iangalie mkulima vizuri

Basi, mambo ya uchumi sasa. Uchumi wetu unaanguka kwa ajili ukulima wetu umeharibika. Uchumi sasa uko chini hata hawa wananchi wa hapa wanakosa hata kusomesha watoto, wanakosa hata pesa na unaona watu wanakuwa maskini. Ukiangalia watu wa hapa Uasin Gishu wanakuwa maskini sana na wanakosa kujisaidia hata kwa kila namna. Sasa ni harambee tu, wanaita tu harambee mpaka hata harambee inakosa kusaidia watu kwa ajili ya elimu hata.

Upande wa Katiba, Katiba hii iandikwe, ilinganishwe na kila jamii. Yaani kila jamii lazima iwe na Katiba yao ambayo inalinda desturi yao kwa sababu hatuwezi, ama mimi kama Mnandi saa hii, mimi ni mtu ambaye desturi yetu wanaume wanatairi, wanaume wanaoa wanawake. Sio kwamba ati mwanamke amtawale mwanaume. Vile vile tungependa kuchangia hii Katiba pia ilinde mipaka ya kila jamii kwa sababu ikilindwa namna hii watu wataishi vizuri. Lakini kwa ukweli, hata sisi tukiweka ile (?) ya Kenyatta wakati ule, ilikuwa inasema kila mtu ardhi yake. Alisema hivyo kabisa, tukiweka hiyo tutasikia saa hii inasema kila mtu ardhi yake ili wananchi waishi vizuri.

Mali ambayo kila mtu ameshatafuta kwa sababu hawa watu, kila mtu ameshatafuta mali yake. Yuko na shamba lake, ako na pesa zake, ako na kila kitu lakini angepewa uhuru huyu mtu agawe mali yake vile yeye anataka. Hatutaki mahali inasemekana ati anakuja kutawaliwa na watu wengine, lazima tutawaliwe na huyu mtu mmoja. Kama nataka kuwapa watoto wangu, ninaangalia vile mtoto ananipenda, mwingine ananiletea kitu fulani ya kufurahisha, mimi nataka kuchagua nisema huyu nitampa kiasi hiki, huyu atachukua kiasi hiki na huyu anachukua kiasi kama hiki.

Vile vile, ninataka kuchangia pia kortini. Kortini ningepende iwe na uhuru wake, uhuru wake kamili wa kuweza kukata kesi yoyote. Isingiliwe tena pengine na wanasiasa. Tuseme wakati mmoja court ikiendelea ya mtu fulani na fulani, wanaweza kupiga simu kwamba kesi hiyo ikatwe namna hii halafu inaumiza mwingine. Vile vile ninataka kuingia upande wa uchaguzi. Uchaguzi (?) wananchi uhuru wa kuchagua yule mtu wanataka.

Com. Salome Muigai: Na una dakika moja mzee.

David Simbolei: Asante. Nimemaliza. Basi ningependa tumpe huru wananchi wale wanachagua watu, wachague yule mtu wanataka, usije kuingilia kusema ati sio huyu ni huyu. Hiyo tena ni kunyanyasa wananchi, tena hiyo kura ihesabiwe hapo hapo msije kusema ati inakwenda kuhesabiwa kule halafu baadaye mnaleta maneno ya rigging. Mwisho, sisi tukiwa Wanandi, zamani tulikuwa tunachagua kiongozi wetu kwa mlolongo, hata Chief. Sisi tulikuwa tunachagua Chief kutoka jamii ile ambayo ilikuwa inaongoza watu tangu zamani. Asante sana, yangu ni hayo.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee. Mzee David Chelget. Mzee David Chelget

David Chelget: Jina langu ni David Kiptawa Chelget, natoka location ya Kapseret. Jambo la kwanza, nashukuru Mungu ambaye ni muumbaji wa watu wote na nchi yote, pia nyinyi watu wa tume ya Commission. Neno langu nasema kuhusu, mimi ni

Mnandi kwanza. Nasema kuhusu nchi ya Wanandi. Hapa Kapseret ni nchi wa Nandi maana kabla wazungu hawajaingia, kabla kifo cha Koitalel Samoi, Wanandi walikuwa hapa Kapseret. Kwa hivyo naomba tume hii ichunguze mpaka ya nchi ya Wanandi. Nchi ya Wanandi inatoka Lomotit na kufuata mpaka yake mto inaitwa Kipchoria, tukagawa na Wajaluo, tukaingia kwa Waluhya, tukafika Webuye, tukafuata mgo unaitwa Moiben, tukaenda mpaka Koibatek tunakutana na Lomotit, hapa ni nchi wa Nandi. Baada ya hayo, nchi ya Wanandi hatutaki mtu yeyote kuingilia ndani. Wanandi wenyewe wanastahili kuchagua viongozi wao ambao wanajua mila zao, maana kiongozi yeyote ambaye anaongoza watu na hajui mila ya hao watu anaharibu hao watu.

Pili, katika nchi ya Wanandi kuna shamba la wenyewe katika shamba la Nandi. Kila nyumba ama kila ukoo wana shamba yao. Haitakikani mtu yeyote kuingia ndani yao, hao wenyewe wanagawana mali yao na shamba yao bila kufuatana na watoto wao. Hakuna mtu mwingine anatoka nje kuingilia. La tatu, mambo ya viongozi kuchaguliwa, wanachaguliwa viongozi ikiwa mjumbe, ikiwa councilor kufuatana na wale wanaojua kuongoza watu. Si yule anayenunua. Anayenunua ndio mwenye kuharibi, tunakata yule anayejua kuongoza ambaye tena anachaguliwa na watu, si yule anayenunua watu.

La nne, katika town kuna municipal na watu wa municipal wamezoea kuzongesha mipaka bila kuuliza wenye mashamba. Wanashirikiana members wa county council na wa municipal wakasongesha mpaka, mpaka watu wanaanza kuumia. Kwa hivyo municipal ikome kusongesha mipaka. Mipaka hao ni hiyo hiyo tu. Wajenge manyuma yao gorofa, hakuna kusongesha. Watu wa county council wakome kudai rent watu kwa nyumba za watu. Mtu kukaa ndani ya nyumba yake, mwingine anamfanyia hesabu ya kulipa rent, haitakikani. Kuuza mtu pamoja na watoto wake, mtu kama yuko nyumba yake analala, mwingine anadai yeye na si shamba lake.

Baada ya hayo, mambo ya mazao, mapato, chakula: tunaishi shamba yetu na kulima chakula chetu tulishe watoto wetu na tulishe watu wetu, nchi yetu. Kuuza tunauza mahindi, ngano na maziwa. Tuna KMC hata angalao wamelala wataamuka. Tunataka kuuza hiyo mali yetu, sisi wenyewe tunataka kujisimamia. Tukichagua wakurugenzi sisi wenyewe tunachagua, si kuchaguliwa na mtu yeyote. Wenye mali wachague wakurugenzi wao, kama ni watu wa KFA, members wa KFA wachague. Kama ni wa KCC watu wa KCC wachague, kama ni watu wa KMC watu wa KMC wachague. Na kazi yetu katika mashamba yetu tunataka kuuza hiyo maziwa, mahindi, nyama ya ng'ombe zetu na kondoo zetu na kuku zetu na mboga zetu. (?) nje. Sisi wenyewe tunataka kusimamia, si mwingine na tunataka tu Serikali ilinde, amani tu ambaye Mungu alitupa sisi. Amani inatoka kwa Mungu, Serikali inalinda, hiyo ndio tunataka.

Jambo la mwisho, viongozi wasitawale wananchi, wananchi wanatawala viongozi. Kama iko mambo ya kupeana kama ma-plot, si mwanasiasa yeyote ikiwa Mbunge ama councilor ambaye anapeana hiyo mali. Lazima achague committee kutoka kwa wananchi wale anajua kweli ni nani anastahili kupatiwa hicho kitu ili asipatie rafiki yake ama asijigawanyie mali yake peke yake. Hakuna kiongozi yeyote anayeweza kujaribu kuchukua mali ya wenyeji.

Mambo ya elimu: ile kodi yetu yote ambayo tunalipa kwa hao watu ikiwa central Government warudishe ifanyiwe kazi yetu ya kielimu na mambo ya hospitali na barabara. Mjumbe aangalie kodi yetu imerudishwa kufanyiwa hii kazi. Pia Councillor wachunguze yale mapato wanapata imerudishwa kufanyiwa wananchi kazi si kuchukua iwe mali yao, kujitajirisha wenyewe. Ni hayo tu.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee.

David Chelget: Mungu asifiwe!

Com. Salome Muigai: Mr. Kipkosgei Chumo.

Kipkosgei Chumo: Hamjambo wananchi. Kile kitu kililete mimi hapa, jina langu naitwa Kipkosgei Chumo kutoka Sirmat Location. Chumo ndio jina langu hilo. Asante sana ma-officers ambao wamelete maneno ya sheria leo hapa tuchunguze. Neno langu la kwanza ni kuhusu retirement. Retire huku inaonekana hata wazee wale wameenda retire kuanzia 1980s mpaka wa leo hawako kwa sababu ya shida. Hao watu walipata shida, ikiwa mimi ni mmoja nilienda retire 1995 mpaka wa leo sijaona hiyo pesa na nilisikia hiyo. Namba ya kwanza niliona tu watu wa retire wawe na society yao. Tunapata wapi pesa ya society hiyo? Serikali yenyewe inatajikana retire, pension iwe kwa DC wa district ya mahali ambapo mtu yuko. Na hiyo nyumba iangaliwe sana wale watu wako ndani wavutwe wote na iwekwe sheria mpya.

La pili, hao watu kwanza wafungue account, kama ni National Bank kama ni wapi, iwe mtu wa retire apate pesa yake kama kawaida, mshahara wote na awe akiongeza hiyo pesa. Pesa ile ambayo tunapewa sasa watu wa retire pension, haitosho. Shilingi elfu moja inatosha hata mtoto kulipa school fees? Na mimi ni Mkenya na nilifanya kazi kubwa katika Serikali? Longezwe hiyo pesa ifike hata elfu kumi na huyo mtu alindwe, kila binadamu ambaye yuko Kenya alindwe kama ameenda retire. Kuja mpaka nyumbani kwake kuangalia anakaa namna gani, mlevi kila siku au anahesabu tarehe namna gani.

La tatu ni kuhusu mambo ya askari. Tuna shida sana kwa upande wa askari, ikiwa ni polisi, ikiwa ni wa wapi, wanatunyanyasa sisi wananchi sana. Siku hizi hata ukienda kuuliza askari iko kitu hapa imeharibika. Anakuambia, una shilingi mia mbili ndio niende huko? Hiyo kitu indolewe kabisa. Kuhusu mambo ya askari vijana, mtu anaandikwa kama ni army ama jeshi fulani katika Kenya. Inamaanisha training na kufika miaka mbili tatu unaona mtu yuko nyumbani. Kwani hiyo pesa ili-train huyo kijana, si ni ya Serikali? Si ni ya wananchi? kwa nini huyu mtu hapana (?) na discipline mpaka amalize miaka yake ile aliweka sign?

Yangu, kuhusu mambo ya chang'aa huko reserve, Serikali ya sasa iangalie mwananchi kule reserve. Mimi nin mzee wa mtaa na mimi ninaona hii chang'aa inasumbua watu kwa ajili ya umaskini. Aangalie apatiwe loan na iwekwe sheria, ikiwa mtu anafanya kazi ya chang'aa huko reserve na amepewa loan, pakuwe na sheria ya kufunga yeye sababu amesaidiwa. Yangu ni hayo.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Mzee Hassan Choge. Mzee Hassan Choge

Hassan Choge: Hamjamboni?

Audience: Hatujambo.

Hassan Choge: Yangu ni maneno mawili matatu. Yangu ni kuhusu hospitali. Kuna shida mimi naona kwa hospitali. Mimi ni Hassan Chogo kutoka (?) Kapseret location. Basi shida ile mimi naona ni mambo ya hospitali. Kuna hospitali hii ambayo ni ya Kenya. Wakati wa kwanza ilisema sisi tutoe kodi ili tutibiwe bure lakini mpaka saa hii karatasi ile ya kuandika ili upate hata tonge ya kumeza unaweza kulipa shilingi thelathini. Na sasa kama mtu analeta mtu mgonjwa

.....*End of side A tape 4*

Hassan Choge: Kutoka kila kitu kile sisi tunanunua wanataka kodi, hawawezi kutusaidia sisi hata kwa (?) ambao sisi tunalipa kodi?

Ya pili ni mambo ya kokwet elder. Kokwet elder ni kama kifagio ya Assistant Chief na Chief, sio watu. Hao wanapata mshahara, kweli wamebarikiwa kupata mshahara lakini kwa nini kokwet elders hawapati mshahara na yeye anafanya kazi mingi kuliko hata assitant Chief, hata Chief mwenyewe? Kazi yake ni kuitwa usiku wote, ng'ombe inakula mahindi, watu wanapigana, kuja kwa shamba. Yeye kazi ni kusimamia shamba na kuona halafu atapelekea Assistant Chief, halafu Assistant Chief ndio anapeleka ofisini kuja (?).

Na mimi naona hapo afadhali msaidie hawa wazee wa kokwet wapate kitu kidogo. Tunaomba nyinyi mpeleke Serikali kuwaambia wazee wa kokwet wana jambo muhimu. Hata mimi naona kuna watu wengine hapo wanaitwa, wanapewa proposal ya kuzungumza mambo ya kesi ya mashamba, wanaitwa panel. Panel haina kazi, wanakuja kufuata wazee wa kokwet kwa sababu hata kama panel inakuja, inakuja kwa vijiji, wanauliza watu wa kokwet wako wapi na watu wa kijiji wako wapi tuulize? Halafu watarokota ile maneno yote ndio wanataka kutuumiza. Lakini ingefaa hata mzee wa kokwet afanye hii ya panel kwa sababu yeye anajua kazi hii yote.

Ya tatu ni mambo ya mashamba. Naonelea sisi Wanandi ama mimi mwenyewe hata naonelea ya kwanza sisi Wanandi mila zetu tulipwe mashamba zetu. Ikija kurithi, lazimatuwe community na mzee wangu tuandike mashamba iwe watu, watu wawili wakitaka shamba. Mimi nikipita, mama anashika, mama akipita mimi ningali bado nashika tugawie watoto, sitaki kupea watoto.

Kwa sababu nikipea watoto, watoto watauza na sisi tutakwenda zikwa kwa municipal. Hakuna kitu watafanya na kulewa.

Basi ya kwanza hiyo sasa ndio maneno yangu nilikuwa nayo. Mimi sina mengi, nasema asante na Mungu awabariki.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee kwa mambo yake na kwa kutumia masaa yako vizuri. Mr. David Cheluget, amesha zungumza? Jonathan Nyaoke alizungumza?

Audience: Ndio

Com. Salome Muigai: Kwa kundi ya wazee na Marko Tarus, wazee walikuja pamoja. Paul Ngand?

Paul Ngando: Ngando.

Com. Salome Muigai: Ni Ngando?

Paul Ngando: Ngando

Com. Salome Muigai: ‘O’ iliachwa, wameandika Ngand. Ngando karibu.

Paul Ngandu: Commissioners na wananchi wenzangu, asanteni sana. Yangu si mengi ila ni pendekezo kidogo kidogo. Kwanza ningesema kwa upande wa uongozi. Ningependa tuwe na Rais, majina ni Paul Ngandu (?). Tuwe na Rais, awe mtu mwenye sifa nzuri na umri usiopungua miaka 45 na usiozidi miaka 70. Na Rais awe na kwake, ameowa, amefanya harusi kanisani hata kama ni ya kitamaduni, iwe imetambulika. Rais awe kazini kwa vipindi viwili yaani miaka mitano kila kipindi kimoja, hizo ni miaka kumi. Makamu wa Rais achaguliwe na raia si kuteuliwa na Rais. Rais asiwe na mamlaka ya kutawala Bunge apendavyo. Rais awe chini ya sheria za nchi, hivyo akivunja sheria atashtakiwa.

Uajiri; mkuu wa sheria awe akiajiriwa na kamati ya kuajiri wala si kuteuliwa na Rais. Awe amehitimu kwa kazi hiyo na asipendeleee upande wowote. Jaji mkuu awe akiajiriwa na wala si kuteuliwa na Rais. Elimu; tungependelea kwa watoto wetu kwa kuwa sasa ndio wanatangatanga sana. Wengine wazazi wao hawana cha kulipia elimu. Wawe na elimu ya bure inayogharamiwa na Serikali na ya lazima, kutoka darasa la kwanza mpaka la nane na hapo tuwe na masomo ya kutoka form one mpaka form six halafu ndio miaka minne ya university.

Afya; gharama za hospitali ziwe zikigharamiwa na Serikali kwa kuwa, kusema kweli hata kama sasa tuko hapa Uasin Gishu, naona hatuna hospitali ya Serikali. Ni lazima tunaenda hospitali za pesa na wengine tunapata matatizo sana kwa kuwa pesa hakuna na watu wanafariki kwa kukosa mahali pa kutibiwa. Hapa Uasin Gishu hatuna hospitali.

Lingine, madaktari wanao ajiriwa na Serikali waangali na wapewe mshahara wa kutosha, wasije wakaweka hospitali zao za kibinafsi. Kwa upande wa mashamba, Mwanakenya wowote anaweza kuishi popote bora atii sheria za nchi na watu walio na

uwezo mwingi wasikubaliwe kuwa na zaidi ya acre 100 ambazo zinakaa bure. Wawe wakiweze kujenga viwanda ili vijana wapate mahali pa kufanya kazi kwa kuwa hata vijana wengi hawana kazi.

Katika upande wa familia, urithi ningeonelea usibaguliwe. Iwe ni mtoto wa kiume, mtoto wa kike, wote wawe wakigawiwa mali, wapewe nafasi ya kurithi mali. Kwa upande wa Bunge, Wabunge wawe wakichaguliwa kwa kuwakilisha idadi ya watu sawa na sio kwa kuwa vile mahali ni pakubwa na watu ni wachache. Ya pili, kuchaguliwa kwa Wabunge maalum iondolewe, kuwe hakuna Wabunge maalum. Yangu si mengi, ni hayo tu, asanteni.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mr. Ngandu. Sasa tungetaka kumuuliza Mr. Mathews Kipretwa.

Matsela Kipretwa: Kwa majina naitwa Matsela Kipretwa. Ninasimama hapa nikiwakilisha kikundi kidogo cha kanisa ya Africa Inland Church. Kanisa letu la Africa Inland Church ni kanisa ambalo halifanyi faida yoyote, non-profit making institution. Kwa hivyo ningeomba Serikali iondolewe rent kwa maploti zao za kanisa kwa sababu hawa hawafanyi faida yoyote. Tunaonelea tena kama kanisa, kwamba Serikali inatambua viongozi wa makanisa kwa maombi za sherehe kubwa kubwa kama Bunge, kabla Bunge halijafunguliwa unaona wanahitaji viongozi wa makanisa wanakuja kufungua kwa maombi. Wanakuja tena kwa national days, unaona ma-pastors au viongozi wanaitwa wanakuja kuomba. Lakini baada ya Serikali kutambua viongozi wa makanisa, hakuna kitu ambacho watapata kama mshahara.

Ningeomba Serikali kwa sababu inawatambua hawa viongozi, wana wajibu kubwa katika Bunge, katika national days, wapatiwe mshahara kidogo kama (?). Hata wale wengine wadogo kama ma-pastors kwa sababu wanafanya kazi kusaidia Serikali, wapatiwe kitu kidogo kwa sababu watu wakifa, kwanza kama mimi nikifa, ninahitaji pastor kuja kunizika. Hata kila mtu hapa, akifariki unaona wanataka pastor aje lakini hakuna kitu ambacho pastor atapata na yeye anafanya kazi mzuri kabisa kwa wananchi lakini hakuna kitu ambaye anapatiwa. Hata kupeana watoto, hata kuomba kwa kanisa. Ukitaka kufunga ndoa, unatafuta pastor anakuja kufunganisha nyinyi ndoa lakini hakuna kitu wanapata kwa Serikali na wamefanyi Serikali kazi nzuri. Sasa maoni yangu

Com. Salome Muigai: Hiyo point tumeichukua, tafadhali ende kwa nyingine kama una nyingine.

Matsela Kipretwa: Ninayo nyingine. Katika kanisa letu tunaweka posters, tunatangaza kuweka mbao yetu ya matangazo yetu. Unaona mwingine anakuja kubandika matangazo yake juu ya mbao yako ambayo umetangaza mambo yako. Sasa ningesema hiyo sheria ingewekwa ili watu wasiweke matangazo yao kwa mbao za wengine. Katika kanisa letu tunaye Education Secretary mmoja katika district mzima hasa ya Uasin Gishu. Ningeomba Serikali kama ingeongeza Education Secretaries mpaka ifike kiwango cha zonal level, ndio kazi ya pastoral programs katika mashule yetu iendelee kwa sababu hilo ni jambo nzuri. Watoto hawataenda kupata madawa ya kulevya kama wamepata pastoral program ambayo inaendelea vizuri.

Jambo lingine ni kuchafulia watu majina. Sijui kama kuna sheria kama mtu anachafua jina lako? Ningesema, kuchafuliana majina, kama wewe una jina nzuri halafu mtu anakuja kukuchokoza na kukuharibia jina lako. Ingewekwa sheria kali kabisa ya kulipa hata sijui maelfu ngapi, ingewekwa sheria kama hiyo. Tena ningekuwa na.....

Com. Salome Muigai: Sasa malizia la mwisho tafadhali.

Matsela Kipretwa: La mwisho ni trespass. Ningeomba tena sheria ambayo inakuja izidi iendelee kwa trespass. Unajua hata kwa nyumba ya mtu kama unaingia kuna sitting room, kuna rooms zingine, lakini utaona watu wengine wanaweza kuja na badala ya kukuaa kwa sitting room, anaweza kuendelea. Sasa trespass ingekuwa iko kwa mambo kama hiyo halafu watu wasipite kiwango kingine. Trespass iwekwe. Jambo lingine ni, Mkenya halisi, kuna swali lilikuwa linasema Mkenya halisi atatambuliwa namna gani? Ningesema atatambuliwa kwa birth, atatambuliwa kwa majina, atatambuliwa kwa utamaduni wao kama meno, masikio, circumsicion, atatambuliwa namna hiyo kwa kusema huyu ni Mkenya kabisa, vitu kama hizo zimekubaliwa.

Com. Salome Muigai: Asante sana

Matsela Kipretwa: Ya mwisho kabisa ni raslimali. Ningependelea kusema raslimali kama mchanga, samaki etc iwe raslimali ya watu wa hapo hapo kabisa kuliko mtu mwingine ambaye anatoka mbali kabisa na anakuja kunyakua raslimali ya district fulani au ya location fulani na kuwa mali yake. Hiyo ni raslimali ya watu wengine. Watu wengine wanakuja kuchukua mchanga wa mtu, wanakuja kuchota samaki za watu na ni raslimali ya watu wa hapo. Asante sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Kuna swali moja kwako.

Com. Ratanya: Bwana Mathews, nina maswali kama mawili hivi

Matsela Kipretwa: Yah

Com. Ratanya: Ya kwanza umesema mambo ya kuharibiana majina. Hiyo pengine inaitwa lower (?) ita defamation. Kuharibiana majina kama mtu anakutukana na kuendelea.

Matsela Kipretwa: Mnh

Com. Ratanya: Na tena kuna trespass. Umesema kuwe na sheria kama hizo. Kama sasa tunasheria hizo katika sheria zetu sasa. Sasa unaona ubaya gani ama ni wapi unataka turekebishe kwa hizo sheria mbili pale hazitoshi? Hiyo ya kuharibiana majina na hiyo ya trespass? Kwa sababu iko, sasa unataka irekebishwe kiupya iwe namna gani kama hiyo haitoshi? Ya pili,

utajibu yote pamoja. Ya pili umeguza mambo ya culture and customary laws. Ukasema utamaduni wetu kama kutairi kuendelea. Sasa hapo tunaendelea na kusema mambo ya kutairi, kuna hata mambo ya kutairi wanawake hiyo debate inaendelea. Sasa wewe kulingana na maoni yako ya ki-kanisa ama wewe mwenyewe, unaonelea tuendelea kutairi wanaume na wasichana? Ni maoni yako hayo.

Matsela Kipretwa: Maoni yangu hapa kwa Mkenya halisi kabisa, Mkenya halisi anatambuliwa namna gani? Mimi nasema kwanza anatambuliwa kwa birth ya ukoo wao kabisa ndio awe Mkenya asili. Tena kwa majina. Majina kama uwe Mkenya kamili, kuna majina ambaye inajulikana hapa Kenya, ukiitwa Kimani unajua huyo ni Mkenya, ukiitwa Kipruto unajua huyo ni Mkalenjin, ukiitwa nani, namna hiyo. Nilikuwa nasema namna hiyo kwa maoni yangu.

Com. Salome Muigai: Hiyo imeshaeleweka Bwana, nafikiri hiyo tumeshaelewa. Endelea kwa hiyo nyingine

Matsela Kipretwa: Nilisema kwa utamaduni tena unajua watu wengine wanatoa meno, wanangoa meno hizi na sasa utajua huyo mtu ni Mkenya fulani. Wengine wanatoboa maskio, ukiona mtu ametoboa maskio unajua huyu ni kabila fulani kwa sababu anatoboa maskio kulingana na style yao. Hiyo ndio nilikuwa nataka niseme, Mkenya halisi.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa maoni yako.

Matsela Kipretwa: Niendelea kwa trespass?

Com. Salome Muigai: Kidogo, kwa ufupi.

Matsela Kipretwa: Ningetaka trespass hasa kwa manyumba zingine, hata kwa compound, ploti ya mtu. Unaona watu siku hizi badala ya kutumia lane ama mahali ambapo pametengenezwa, unakuta tu mtu anakuja kukata shamba yake, anafinya seng'enge anaenda. Iko sheria lakini bado haijakazwa kabisa kusema hii ni trespass na anaweza kushikwa

Com. Ratanya: Kwa hivyo ni mkazo

Matsela Kipretwa: Ndio ni mkazo

Com. Ratanya: Ni mkazo (?)

Matsela Kipretwa: Basi ni mkazo. Hata kuchafuliana jina ni mkazo. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa maoni yako Bwana Mathews. Albina Aluda.

Albina Aluda: Kwa majina naitwa Albina Aluda. Mimi nakaa hapa Eldoret Langas.

Com. Salome Muigai: Tafadhali mpaka watu wakuwe tayari kukusikiza.

Albina Aluda: Kwa majina naitwa Albina Aluda, mimi nakaa hapa Langas. Nitasema tu machache kwa sababu mengi yamesemwa na hii inahusu watoto. Niko hapa kwa niaba ya teenage mothers and children. Ya kwanza ni basic rights kama afya, maji, chakula na elimu. Naona kila mtoto anatakikana apate free and compulsory education. Gender parity in decision-making should become a basic right. Both gender have a right to equal representation in decision-making. Ninasema hata tukiwa nyumbani, si ati mzee ndio ana decide ati tunaenda kufanya hili, ni vizuri tuamue pamoja ndio litaendelea vizuri.

Mambo ya utamaduni, culture – mzee ameongea kidogo. Tunataka hii Constitution kama ni kutairi wasichana, ikuwe kwa Constitution na kama si kutairi wasichana ikuwe Constitution, si culture ati hawa wanatairi na hawa wasitairi. Kwa sababu sisi tungependa mambo ya kutairi wasichana isikuwe na ipitishwe kama Constitution. Si eti Waluhya wanatairi wasichana na Wanandi hawatairi because sasa hiyo ni culture lakini ikiwa Constitution ni uniform. So tungependa iwe hivyo. Kwa Parliament, tunataka wamama wakuwe, hata kama inaweza kuwa one third ya wamama. Tukienda kwa mambo ya local Government, hatutaki ati kama wanachagua Mayor au councilor wanaenda kujificha Tanzania wanachaguana huko. Wachaguliwe na watu kwa sababu mimi nikitaka kuwa councilor mzee wangu hatapenda niende Tanzania kujificha na wazee wengine. Wachaguliwe na watu, si kwa sababu niko na pesa nipeane na nichaguliwe na watu ambao hawanitaki,

That is local Government. Mechanism for accountability needs to be put in place to ensure democracy and transparent local Government. The principle of at least one third of representatives (?) at any one time to be entrenched into the Constitution to ensure gender equality in the local Government. Ninaenda haraka shauri ya saa. Mambo ya geographical constituencies. Lazima tuwe na boundaris kwa sababu mtu akiwa na constituency kubwa hata hajui nini inafanyika kwa constituency yake. Haka kama ingekuwa mambo ya Chief vile mtu alisema, ni vizuri hata Chief ajue how many households kuliko tu kusema tuko na Chief na hajui nini inafanyika. Mambo ya law, law should provide the provision for security for all (?). Security, si eti wengine wanasikia mzuri na wengine wanaumia.

Tukija mambo ya girl-child, hata nyinyi Commissioners' mumeona hapa, wamama tuko wangapi. Tuko wachache sana, about one eighth na sasa tunasema lazima tuendeshe maendeleo pamoja. Na hiyo maendeleo Constitution ndio itasaidia sisi because iko wamama wako na elimu, wako na maendeleo. Hata mtu anaweza kuwa hajaenda shule lakini anaweza kuongoza familia yake kulingana na kile kipawa Mungu amempa. Lakini kama ni mama hicho kipawa kinafinywa. Tena, wenye wako na vibeti ni wazee na wenye wanafanya kazi ni wamama. Sasa hiyo mambo, nataka kama ni vibeti, tujue ni nini iko kwa hiyo kibeti kwa sababu mimi nachunga ng'ombe, nakamua, nalima mahindi na sijui bank ya mzee wangu iko wapi. Hiyo nataka muangalie hiyo maneno in the Constitution.

Maneno ya administration, limit to election expenditure. Hatutaki tu ati kwa sababu mimi Mbunge niko na pesa mingi kuliko yule Mbunge mwingine sasa naanza kutoa pesa. Hii pesa ikuwe limited. Kama wanajua ni elfu ngapi Mbunge atatumia kwa siasa, ikuwe hiyo kwa sababu wengine wanatumia pesa lakini they are not the right candidates. Sasa hiyo lazima iwe kwa Constitution. (?), Hiyo hatutaki kujua itakuwa siku gani, lakini ni vizuri kufanya kazi kwa utaratibu.

Lakini sasa kumaliza kwa sababu ya saa, mimi niko hapa kwa niaba ya wamama na girl-child. Sasa tukianza kutoka kwa watoto, tujue John na Mary wako equal, hata tukienda Parliament itakuwa hivyo. Na hivi vipawa vyote tuko navyo, ni vizuri kuzipa nafasi kuliko kunyima. Kama watoto wasichana. Unaona mzee anapeleka kijana na msichana amefanya vizuri, wanasema enda oleka. Sisi pia tunataka umri wa kuoleka. Kama utapeleka mtoto wako kama ako ten years, uwe disciplined by the Constitution that will be passed, ndio kila mtu aende shule na kila mtu awe na equality yake. Lakini wamama tunataka from the grassroot, tuwe equal, tupewe equal chances. Nimesema pengine tunaanze ndio nilisema one third, tupe wazee two thirds lakini isikuwe kama hapa one eighth, hii ni mbaya sana. Wamama hata walipenda kuja lakini wazee walisema enda chungu ng'ombe mimi ndio ninaenda na wamama wangepika pia watoe maoni yao. Hiyo ni kweli, asanteni sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana mama, kabla haujaondoka hapo ningetaka kukuuliza swali moja. Umesama habari ya umri wa kuolewa. Ungependekesa umri upi?

Albina Aluda: Kulingana na sheria ya Kenya, wanasema mtu anapata kipande akiwa na miaka kumi na nane. Si vizuri mtu aoleke na hana kipande. Hata angalau apate kipande ndio umuoe, ningesema hivyo.

Com. Salome Muigai: Kwa hivyo unasema miaka kumi na minane?

Albina Aluda: Kumi na minane and above.

Com. Salome Muigai: Okay

Albina Aluda: Yes

Com. Salome Muigai: Sasa kwani mama amejitetea vilivyo na sijawaita wakina mama wengi, ningetaka kumuita Josephine Kutuny.

Josephine Kutuny: *Achame akaak tugul en kainet ab Jeiso ale ochamege tugul*

Translator: Anawasalimu wote, hamjambo

Audience: Hatujambo

Josephine Kutuny: *Awekyini kongoi Jehova*

Translator: Anashukuru Mungu

Josephine Kutuny: *Amun kikokonech nyikanatet.*

Translator: Kwa sababu ya kutupa nguvu

Josephine Kutuny: *Komiyon ko chepyoso.*

Translator: Akiwa mama pia naye akiwa hapo mbele

Josephine Kutuny: *Ko kikoitech Jehova kele ki bik.*

Translator: Inaonesha hata Mungu amewahesabu kuwa watu

Josephine Kutuny: *Awekyini kongoi Mungu amun no ton.*

Translator: Anashukuru Mungu kwa sababu hiyo

Josephine Kutuny: *Makase Kiswahili.*

Translator: Yeye, lugha ya Kiswahili ni taabu kwake

Josephine Kutuny: *akamache imwa kouyekamwa.*

Translator: Ananiambia niseme vile amesema

Josephine Kutuny: *Ng'alekyuk I, kainenyun kekurenon Josphine chepyoset ab Kutuny.*

Translator: Naitwa Josephine Kutuny

Josephine Kutuny: *Amun en echek koyekageit rika ini nyun*

Translator: Kulingana na mila, rika hii yake

Josephine Kutuny: *ko me kekuren neba arap.*

Translator: Haitwi bibi wa fulani

Josephine Kutuny: *Amache okas noton lagok si mabet no kurengei. Chepyoset kotom koyamak*

Translator: Anaambia hawa wasiende mpaka waka trespass.

Josephine Kutuny: *Kikuren neba arap che uchon.*

Translator: Rika hii ndio inaitwa bibi wa fulani

Josephine Kutuny: *Echek kekuren chepyoset.*

Translator: Yeye anaitwa gogo wa nyumba fulani

Josephine Kutuny: *Kang'et en yu,*

Translator: Anatoka hapa

Josephine Kutuny: *Amun kitinye tabu kamastab chepyosok.*

Translator: Kwa sababu wamama wana shida

Josephine Kutuny: *Kitinye tabu amun ng o kakotunin boiyot,*

Translator: Wana shida kwa sababu wakisha olewa

Josephine Kutuny: *Itebie en yoton kityo.*

Translator: Wanakaa hapo tu

Josephine Kutuny: *ak irib tuguken yoton.*

Translator: Na kuongoja vitu tu waletewe

Josephine Kutuny: *Ingoit anyun raini kokomenge kitun imbarenik.*

Translator: Ikiwa kwanza kwa mfano kama wakati huu mashamba yamekuwa madogo

Josephine Kutuny: *Ko makingen petut agetugul ne ruwei chito.*

Translator: Haijulikani mtu atakapo lala au kufa

Josephine Kutuny: *Makingen ingondoi chepyoset, ingondoi boiyot.*

Translator: Haijulikani kama ni mke au mume ataongoza kwa kifo

Josephine Kutuny: *ko mi malik yutan.*

Translator: Kuna mali hapa

Josephine Kutuny: *Che kikicheng' ak boiyot nyun.*

Translator: Ambayo mume na mke walitafuta pamoja.

Josephine Kutuny: *Ke cheng' malik ko ye kakobwa malik.*

Translator: Walifanya bidii na wakati sasa mali imepatikana

Josephine Kutuny: *Bahati mbaya kagoru boiyot.*

Translator: Kumbe kwa bahati mbaya mume akafa

Josephine Kutuny: *Ak ye kagoru boiyot I,*

Translator: Wakati mume sasa ameaga

Josephine Kutuny: *Keguren chepyoset makii.*

Translator: Huyu mama hatambuliwi kama kitu

Josephine Kutuny: *Kele malik koribe lagok*

Translator: Anasema sasa mali ni ya watoto

Josephine Kutuny: *Oko lagok komakas uchungu ole kikichengdai milk ak boiyot.*

Translator: Na watoto hawakujua pilika zilizopitiwa na wazazi kupata mali haya

Josephine Kutuny: *Konyor malik choton ak kong'emang'em.*

Translator: Hao watoto wanapewa haya mali na wanaanza kuharibu

Josephine Kutuny: *ak ngot ami anyun chepyoset amako boiyot, ama malik.*

Translator: Na mama bado yuko hai, anaanza kuteseka, bwana hayuko na mali haziko

Josephine Kutuny: *Okertai ono anyun Serikalit bik che uchoton oko bik che kicheng'e malik ko bichu oeng'.*

Translator: Unaona je kitendo kama hicho na hao watu wawili walitafuta mali?

Josephine Kutuny: *Nyalu keratyin chepyoset ak boiyot.*

Translator: Unaonesha sasa ni lazima bibi na mume waandikwe katika chochote

Josephine Kutuny: *Amun kikocheng' maalikchwak en kagilet ab kei.*

Translator: Kwa sababu walitafuta hiyo mali kwa bidii

Josephine Kutuny: *Ingo sibkowa chepyoset,*

Translator: Akienda kabla ya mume

Josephine Kutuny: *Koribe malik boiyot kot ko pyechi kou ye kamakyin.*

Translator: Mume atabaki alinde mali mpaka awape watoto vile anavyotaka

Josephine Kutuny: *Ango sipkowa boiyot,*

Translator: Kama mume ataenda mbele

Josephine Kutuny: *Kong'etu chepyoset amun kait neba boiyot.*

Translator: Yeye naye atabaki kwa sababu ni naibu wa mume

.....*End of tape 4*

Josephine Kutuny: *Ako rib malikyik.*

Translator: Kulinda na kuchunga mali hiyo

Josephine Kutuny: *Asi kopyechi lagok kou ye makyingei.*

Translator: Naye pia atagawanyia hao watoto mali hiyo vile anavyotaka

Josephine Kutuny: *Asi mang'em tuguk lagok.*

Translator: Ndio watoto wasipate uwezo kuharibu na kuchezea mali hiyo

Josephine Kutuny: *Ako kiriwe hasara icheng'e.*

Translator: Na wewe umeenda hasara kutafuta hiyo mali

Josephine Kutuny: *Merue kemoi ak bet.*

Translator: Haulali usiku na mchana

Josephine Kutuny: *Chepyosok.*

Translator: Wamama

Josephine Kutuny: *Che kiyosen.*

Translator: Wao wazee

Josephine Kutuny: *Koki en keny kinkobendi boisyek luget.*

Translator: Zamani wakati wazee wanatoka kutafuta mali

Josephine Kutuny: *Kogii bore bek chepyoset*

Translator: Mama alikuwa akikongoa mahindi

Josephine Kutuny: *Ak konde sotet.*

Translator: Na kuweka wimbi ndani ya kibuyu

Josephine Kutuny: *Akityo kowa boiyot luget.*

Translator: Na mzee sasa anaenda kutafuta mali

Josephine Kutuny: *Koiib tuguk.*

Translator: Anaenda kuleta mali

Josephine Kutuny: *Sasai*

Translator: Sasa wakati huu

Josephine Kutuny: *Ko kikong 'etio boisiek yani choton ko lagokyok.*

Translator: Sasa hao watoto wetu ambao wanaitwa wazee

Josephine Kutuny: *Kobendi,*

Translator: Wanaenda

Josephine Kutuny: *Kago yamis chepyoset wendi kasit en Nairobi.*

Translator: Wakati mke amemuaga ameenda kazi upande wa Nairobi

Josephine Kutuny: *ingomi oloton I,*

Translator: Anapofika kule

Josephine Kutuny: *Makobwati olin ba gaa.*

Translator: Anasahau nyumbani

Josephine Kutuny: *kotoi ingunon kokagele che chik tuguk.*

Translator: Ananza sasa kwa sababu mali imesemekana

Josephine Kutuny: *Komuchi koalda tuguk en olatan.*

Translator: Anaanza kuuza mali kule

Josephine Kutuny: *Akityo kogai tabu Serikali amun imuche konyoko kanapta tugul komi lagoi.*

Translator: Na anaanza kupea Serikali taabu kwa sababu anauza shamba watoto wakiwa kule

Josephine Kutuny: *Chepyosok*

Translator: Wamama

Josephine Kutuny: *Kimache anyun i*

Translator: Tunataka

Josephine Kutuny: *Olenjinewech Serikali*

Translator: Muelezee Serikali

Josephine Kutuny: *Chichon ale imbaret ama iro mama*

Translator: Yule mtu anayenunua shamba bila kuona mama

Josephine Kutuny: *Kakwal tugul kobata lagok*

Translator: Ajue kwamba amenunua hiyo shamba pamoja na watoto.

Josephine Kutuny: *Amun bendi ano?*

Translator: Kwa sababu hao watoto wanaenda wapi?

Josephine Kutuny: *Nerube noton.*

Translator: Linalofuata hili

Josephine Kutuny: *Ketinye lagok.*

Translator: Tuna watoto

Josephine Kutuny: *Kitinye werik ak tibik.*

Translator: Tuna wasichana na wavulana

Josephine Kutuny: *Kigesich komie.*

Translator: Tumewazaa vizuri

Josephine Kutuny: *Kikisomesan*

Translator: Tumewaelimisha

Josephine Kutuny: *Kikong'et koroita ake ne kagile kiguren Ne nekerute.*

Translator: Kuna jambo ambalo limefika sasa ambalo linaitwa, pool ama nini?

Josephine Kutuny: *ak kebendi video*

Translator: Kuna pool na video

Josephine Kutuny: *kobaanyun lagochu kaalji sandet video koip kobakoger.*

Translator: Wanajikaza wanunue hiyo video sasa halafu wanaenda kuangalia

Josephine Kutuny: *Ip kosich lakwet chepto lakwet.*

Translator: Halafu hapo msichana sasa anaenda kuzaa mtoto

Josephine Kutuny: *OKo ye kakosich lakwet I,*

Translator: Baada ya kuzaa mtoto

Josephine Kutuny: *Ko toi sandeet kole mang'enin.*

Translator: Huyu mvulana anamgeuka

Josephine Kutuny: *Kindai ano lagochatan.*

Translator: Hao watoto tutaweka wapi?

Josephine Kutuny: *Amache*

Translator: Anakata

Josephine Kutuny: *Kerat sandanaton ak cheboton amun mami kiy ne kikachin amri.t*

Translator: Wale wote wanaozaa nje ya ndoa wafungwe.

Josephine Kutuny: *King'emi kokitibik,*

Translator: Hao wakiwa wasichana zamani

Josephine Kutuny: *Moker is ole koik aibu.*

Translator: Msione kama ni aibu.

Josephine Kutuny: *Kokikimi kogi tibik che kitonondosi .*

Translator: Wao walipokuwa wasichana walikuwa wasichana wakisimama

Josephine Kutuny: *Kikimite ole kimakingen okot kele kilache ingoriet.*

Translator: Hawakujua kwamba kuna mavazi ya (?)

Josephine Kutuny: *Lakini makinyoru oko chepto akenge ne kibun.*

Translator: Lakini hakuna mtoto hata mmoja aliruka na kuzaa mtoto kabla ya wakati.

Josephine Kutuny: *Kikemete lagok kosigot lagok kou sesenik.*

Translator: Watoto tumewaachilia kuzaa ovyo ovyo kama mbwa.

Josephine Kutuny: *Murenichu,*

Translator: Hawa wanaomba wavulana,

Josephine Kutuny: *Taimuti mogor iman boiyot ne yos muren i.*

Translator: Unaweza kweli kumpeleka mvulana, mzee kama huyu kuenda mahali pa (?)

Josephine Kutuny: *Kolyan sikosib kosich lakwet kotom koit kiwango neba kiyon.*

Translator: Mbona tunazaa watoto kama miaka au ruhusa hawajapata rasmi

Com. Salome Muigai: (?) mama sasa amalizie

Josephine Kutuny: *Neerube noton*

Translator: Linalofuata hilo,

Josephine Kutuny: *amun kago wonan sait.*

Translator: Kwa sababu ya masaa

Josephine Kutuny: *Amache amwa ale*

Translator: Anataka kusema

Josephine Kutuny: *Ake ko kap D.C.*

Translator: Maneno ya DC

Josephine Kutuny: *Kap D.C ko ole kirwakyin ne ngei.*

Translator: Hapo ndipo maneno inafanyika

Josephine Kutuny: *Amune si ketinye kanisosiek lakini ikwae lagok kap D.C kotunis lagok kotun mamilioni cheba kwanyik.*

Translator: Anasema tuna makanisa lakini wengi wametoroka kutoka kuoia ndoa za kanisa, wanakimbia kwa ile ya DC.

Josephine Kutuny: *Kalyan D.C si merwakyi kirwagutikyik kometa chutan ba kanisa, koyai kanisosieek.*

Translator: Mbona ofisi hiyo basi isiruhusu watu wafanye ndoa zao na yeye afanye zingine kwa sababu huko ndio watu wanafanyia ukora.

Josephine Kutuny: *Asikobit kosabcho lagok.*

Translator: Ndio watoto wapate kupona.

Josephine Kutuny: *Kounaton I*

Translator: Kwa hayo

Josephine Kutuny: *alenjinok kongoi.*

Translator: Nasema asante

Josephine Kutuny: *Orib mila neba bik.*

Translator: Chunga mila ya watu.

Josephine Kutuny: *memuche ingo kobais, agot ingunon emet ab lima ak emet ab Nandi kongo tiendos Nandi kolel.*

Translator: Anasema mila ni tofauti, ukienda Western Kenya na hapa Wanandi, Wanandi wakiimba, wanaimba wakifanya hivi,

Josephine Kutuny: *Lakini ingo tiendos lumek koburbureni ke.*

Translator: Nao wale wa Western wanaimba wakivingirisha mwili wote

Translator: (?) kule (?) wanaimba tofauti hivyo

Josephine Kutuny: *Ongetien tiendo ne nyon.*

Translator: Anasema tuimbe wimbo ulio wetu

Josephine Kutuny: *ingo berurok Jehova.*

Translator: Mungu awabariki.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mama Josephine Kutuny. Sasa ningetaka kumuita Mzee Daniel Samwei. Mzee Daniel Samwei?

Daniel Samwei: *Kit ne amwae en yu amwae kongoi missing.*

Translator: Anasema anarudisha shukrani sana

Daniel Samwei: *Kaine nyun kekurenon Daniel arap Samoei.*

Translator: Kwa majina anaitwa Daniel arap Samwei

Daniel Samwei: *Abunu Kamagut.*

Translator: Anatoka sehemu za Kamagut

Daniel Samwei: *location.*

Translator: Location ya Kamagut

Daniel Samwei: *Ko kit ne tai en yu ne iimech ko imbarenik.*

Translator: Jambo la kwanza linalotuudhi sana na kutusumbua ni mashamba.

Daniel Samwei: *Oko imbaret ko kit ne kiosaben, long'et tugul no, ngomami imbaret koma mi kiy.*

Translator: ambayo ndio nguzo ya kuishi

Daniel Samwei: *Kit ne ya en imbaret ko kirwaget.*

Translator: Kinachotusumbua kwa mashamba ni kesi.

Daniel Samwei: *Mache kobetyi kirwakindet kobek kirwaget ab imbaret chief anan ko D.C ak koyam.*

Translator: Kesi za mashamba zinatakikana kuishia utawala wa mikoa ambao ni DC na kurudi, isiende juu

Daniel Samwei: *Amun imbaret ingwa kotkoit okilyot ko tabu.*

Translator: Kwa sababu kesi ya shamba ukifikisha kwa wakili itakuwa ni taabu

Daniel Samwei: *Amun okilini komache rabisiek.*

Translator: Kwa sababu mawakili kazi yao ni pesa.

Daniel Samwei: *amangen baornatanaton okot imbaranaton ko mang'en.*

Translator: Na hawajui uhakika wa shamba hilo.

Daniel Samwei: *Ingelejin kitaunenkei ano imbarani komaingen.*

Translator: Wajikaribu kuulizwa historia ya hiyo shamba hata hawajui

Daniel Samwei: *Amun boiyot kok ak kirwakindet kongen komie.*

Translator: Lakini mzee wa mitaa na Chief ndio wanaoelewa kesi za mashamba zaidi

Daniel Samwei: *Amun ne nywan imbaret oko che chwak bik mi ak bik katakora.*

Translator: Kwa sababu shamba ni yao na hao watu ni wao na wako na hao watu kila wakati.

Daniel Samwei: *Kaigai Serikali oker laininoton ba kap ogilini.*

Translator: Tafadhali msiruhusu kesi zetu zifanywe na mawakili na mahakama na kuenda juu, zirudi kwa wazee wa mitaa na Chief

Daniel Samwei: *Okot akinye ne kerwachi ng'omayamin en yoton koi chorin.*

Translator: Naye wewe unayefanya kesi, iwapo hautaridhika na kesi ya akina Chief na DC, wewe ni mwizi.

Daniel Samwei: *Nerube yoton amwae agoba malik.*

Translator: Linalofuata sasa nitaongea kuhusu raslimali au mali

Daniel Samwei: *Kinge mi emani ketieng'e KCC amakinge ye kiit*

Translator: Hapo mbeleni tulikuwa na KCC lakini hatujui ilikoelekea

Daniel Samwei: *Kinge tinye KCC kokitinye sabet. Kigisomeshan lagokyok komie.*

Translator: Tulipokuwa na KCC hatukuwa na shida, tulisomesha watoto wetu bila shida.

Daniel Samwei: *Lakini ingunon korandarandan lagokyok kopetyo amun tuguk che kisomeshanen komami.*

Translator: Lakini sasa watoto wetu wanatangatanga, kurandaranda lakini ni kwa sababu hatuna pesa za kuwasomesha.

Daniel Samwei: *Amun ki KCC ko kilengut ne kikikonoren rabisiek.*

Translator: Kwa sababu KCC ilikuwa ikituhifadhiwa pesa

Daniel Samwei: *Ki kila arawet iibu rabisiek che matinye matata.*

Translator: Ilikuwa kila mwezi unaenda unatoa pesa zako bila matata

Daniel Samwei: *konyokowa lakweng'ung'ukul bila taabu..*

Translator: Ndio hapo watoto wanakunywa wanaenda shule bila taabu.

Daniel Samwei: *ngo shida ne kitinye newo ko neba KCC kabisa.*

Translator: Shida sasa tulionayo ni KCC.

Daniel Samwei: *Ne ba oeng' ko KFA.*

Translator: La pili ni KFA

Daniel Samwei: *KIkome KFA nemakingen kele kiurusan KFA ak keyae bek, kiib ne bek.*

Translator: Nashindwa KFA imeisha na tunalima, mahindi ikapotea, ni nini ilichukua KFA?

Daniel Samwei: *Ne nda maeni okot kenyit akenge ke bete amun ma mi chaget ne kimi bek.*

Translator: Hata sasa Mungu anatusaidia kwa sababu kukitokea ukame kidogo tu wa mwaka mmoja tutakufa. Hatuna mahali pa kuhifadhia, hatuna mahindi iliyo katika hazina.

Daniel Samwei: *ye maitinye chi to chaget ne ikonoren tuguk kuk kotai chito.*

Translator: Ikiwa kweli umefika wakati hauna store ya kuhifadhi vyakula, kweli wewe bado ni mtu?

Daniel Samwei: *Maipuch i?*

Translator: Si wewe ni mtu tu.

Daniel Samwei: *ko tuguk ab kop chi age che mache kotisyin ko chi age ko cheba ne?*

Translator: Kusema ukweli vitu vya mtu ambaye mwengine anataka kuengemea au kunyemelea ni vya nini?

Daniel Samwei: *Ki tugukyo ko imbaret ak kerib teta tuguk oeng'.*

Translator: Sisi tunataka tuchungiwe shamba na mifugo.

Daniel Samwei: *Matakingen missing biashara. Biashara ne nyon ko kealde tuguk chuton ak kealde chego.*

Translator: Sisi hatuwezi biashara sana lakini mambo yanayohusika na hizi, mimea na mifugo ndio yetu.

Daniel Samwei: *Kingen kele yon kaialde tete ko kakwa lakwet sukul.*

Translator: Basi tunajua kwamba ukisha uza ng'ombe, tayari mtoto ameenda shule.

Daniel Samwei: *Ko tuguk che uchoton che kikon taabu.*

Translator: Vitu hivo ndio vimeleta taabu.

Daniel Samwei: *Kebebetab Serikali koiman komache kotebi kirwakindedt komie.*

Translator: Anasema kwa upande wa Serikali Chief anastahili kukaa vizuri

Daniel Samwei: *ko miak assistant chief ak boiyot kok.*

Translator: Wakiwa pamoja na Assistant Chief na mzee wa mitaa.

Daniel Samwei: *koribaksei Koret amun mi ak bik chwak ak kongen History che chwak cheba picha ton.*

Translator: Nchi itaridhika vizuri, watu watatawaliwa vizuri kwa sababu hawa watu wako na watu.

Daniel Samwei: *Ko Mbunge ke kwae bik tugul.*

Translator: Mbunge ni mtu anayechaguliwa na watu wote

Daniel Samwei: *ko ingosich chi bahati yake ko ka kwae bik.*

Translator: Mtu akifaulu au apite kwa bahati yake ni kuwa amechaguliwa na watu.

Daniel Samwei: *Amun makilenjin chi meten ni ng'unget.*

Translator: Kwa sababu hakuna mtu anaambiwa wacha, mtu huamurishwa na kura.

Daniel Samwei: *Amuani kurayat chito noon ne kakikoito kowa Serikali.*

Translator: Kura ndio muamuzi wa mwisho kwa kiti hicho cha uBunge.

Daniel Samwei: *Konai bik icheken kole yamechweri eb kapanum ana mayamech konai kokwanoton kakwae.*

Translator: Nasema kwamba ni watu wenyewe wataamua huyu mtu wa nyumba fulani atawatosha au hawatoshi.

Daniel Samwei: *Mikit age ne kakimwa kele Prime Minister.*

Translator: Kuna jambo ambalo limetajwa la Prime Minister, Waziri Mkuu

Daniel Samwei: *ko chichoton anyun ke chame amun ye kakonyor Kap chitugul kirkinnywan akomuch korib emenywan koribakse emet ab chi.*

Translator: Anasema iwapo Serikali ya majimbo itakubaliwa kila mtu awe na uwezo wa kulinda raslimali zake, yeye anaunga mkono kwa dhati ofisi ya Waziri Mkuu

Daniel Samwei: *ko choton che chuk amun emani ketelejin, kigiribe kong'eten taunet.*

Translator: Anasema hayo ndio yake na inajulikana kwamba nchi hii ilikuwa ikichungwa na kulindwa tangu zamani.

Daniel Samwei: *Ng'emangung' ko kimengech ko mi boisiek chok ak chumbek ak kikiribe emet ak kiribok agoi ra.*

Translator: Wakati alikuwa mchanga alikuwa (?) akiona wazungu na wazee wakilinda nchi na hadi sasa bado inalindwa.

Daniel Samwei: *Ko choc he chuk kongoi.*

Translator: Hayo ndio yake, asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee Samwei. Sasa namuita mama Emiliana Chebor. Mama Emiliana Chebor na atafuatwa na Rael Tirop, kwa hivyo naye ajiweke tayari. Rael Cherop bado yuko?

Rael Cherop: Niko

Com. Salome Muigai: Emiliana Chebor kwanza, sorry halafu Rael Cherop.

Speaker: (?)

Speaker: (?)

Speaker: Nilipeana jina na mimi nasikia naitwa (?)

Com. Salome Muigai: Tafadhali mzee tumeandikisha majina, hata hayo majina ya wazee tumechaguachagua ndio wazee wasiwekwe sana. Vumilia kidogo.

Emiliana Chebor: Commissioners na wananchi wenzangu, nawasalimia kwa jina la Yesu nikisema hamjambo nyote?

Audience: Hatujambo.

Emiliana Chebor: Basi mimi hapa ninaunga mkono sehemu ya watu wa pension ambao wame-retire. Mimi ni mmoja wao.

Mimi Emiliana Chebor kutoka location ya Kapseret, Tuiya Farm. Maneno yangu ni haya, ninazungumza juu ya retirement kwa wale wame-retire ambao ni watumishi wa Serikali hapo awali na tuna mshahara mdogo. Naunga mkono mmoja ambaye pia amezungumza. Kuna mmoja anapata 150 kwa mwezi na mimi pia nikiwa hapa hivi napata 500 kwa mwezi na nili-retire nikiwa na miaka 27 nikapewa retire niende nyumbani kupumzika. Nili-retire 1980 December. Na huu mshahara ni mdogo, tunalia kwa sababu ya mahitaji yote. Tuna watoto, tuna wajukuu na wote wanatuangalia kwa sababu sisi ni nguzo ya nyumba tukiwa wazazi. Tunaomba mtusaidie kwa hio njia ili itimike vizuri, na mtu awe anajisikia vizuri nyumbani, awe anaweza kula kama mwingine, asihangaike mpaka akafanya yale hayampendezi. Mimi nilikuwa ungraded nurse, najua kazi ya hospitali na nikipatikana nikifanya machafu kama kutengeneza pombe na mambo mengine, watu watashangaa. Watasema kwa nini mama anaelewa na anafanya vitu kama hivi? Kwa hivyo tunaomba msaada kupitia mikono yenu iende kwa Serikali.

Kuna siku Wabunge walizungumza kwa Bunge 1994, wakasema watu walio na mshahara chini ya pension, inafaa waongezewe iwe shilingi elfu mbili. Walisema na wakapitisha wenyewe na tangu siku hio mpaka wa leo, hatujaona kitu, tuko tu kama zamani. Ile nusu ya mshahara wako ambao walisema ni benefit unapata half salary na chochote kile, tuliandikwa na wazungu wa ubeberu time. Mshahara ilikuwa kidogo na tukaongezwa ongezwwa hivyo mpaka mahali tulifikia.

Mambo ya retirement, wengi wanakuwa wana-retire wakiwa na miaka 50 wanaume na wanawake ni miaka 45, lakini inategemea uwezo wa mtu mwenyewe akiwa na nguvu ya kuendesha kazi vizuri na Serikali inaona bado anafanya, afanye. Hakuna mtu atalazimishwa aende pengine huko nyumbani hakuna kitu. Lakini lazima ajifikirie ya kwamba akitoka hapo, hapo si nyumbani, kuna nyumbani ambapo ataenda aketi na atapata shida zaidi.

Namba tatu, mimi nazungumuza juu ya watoto wa kuzaliwa na wasichana ambao hawajaoleka na mtu. Na hawa watoto, namuongezea huyu mama lakini pia nilikuwa na wazo hilo. Wenyewe wana tabia mbaya kwa sababu sisi wote tumepitia hiyo njia ya utoto mpaka tukawa watu wazima na kulikuwa na sheria. Msichana akiwa bado ni msichana asipate mimba. Na ana mchumba, wanacheza, wanaenda pamoja sigirai na wanafanya vyovyote lakini hakuna njio hiyo. Mpaka awe virgin akiolewa na mume wake. Walikuwa hawazai watoto nje na hiyo sheria ni sisi wazazi tumetupa, watoto wetu hatuwapeleki kwa ile sheria tulikuwa nayo ya zamani. Tumesema wamesoma, wamekuwa civilized wanajua chochote, lakini civilization yao inakuwa kuambatana na uchafu. Halafu wanazaa watoto nje ya ndoa, hawajaoleka. Mtu na baba yake hata hajui ile walikuwa wakisema heshima kwa msichana wangu, awe mwanamwali, aolewe akiwa mwanamwali. Na mumewe pia alikuwa akisema, yule mchumba wake, msichana wangu awe ni mwanamwali nikimuoa. Lakini saa hii wanaanza hata yule hajui mambo gani inaendelea katika dunia hiyo.

Tuwasaidie kwa sababu hawa watoto wanaozaliwa na wasichana ndio baadaye wanakuwa chokora kwa sababu mama yule hajui kutunza. Amezaa, anatupa yule mume alimpatia mimba, hana haja pia. Wote wako njia nyingine na hawa watoto wamebaki nyumbani bila chakula na dakika ya mwisho, hawa watoto wako barabarani kuomba na kufanya chochote halafu wanakuwa chokora. Na hatutaki kuona na macho, ati ndio kitu muhimu kweli tunaona watoto wetu wakiendelea, wajukuu

wetu na vitukuu vyetu, tunawaona hivyo. Na hatuna njia, sababu msichana wangu kama amesoma na ajitafutie kazi na ajitunze apate mume, mume ndio maisha mazuri. Kwa sababu gani Mungu aliumba mwanaume, akakaa kidogo na baada ya hiyo akatoa ubavu wa mkono wa kushoto na akamuumba mwanamke? Na huyu mwanamke lazima atunze hiyo heshima yake ndio aweke kwa bwana wakae pamoja. Sasa ninazungumza juu ya hawa watoto. Sisi wote tuone ni kitu gani tutawafanya watoto wa kuzaliwa nje ya ndoa kabla hawajaoleka. Tuwatengenezee pahali na wasome na watunzwe vizuri halafu waendeleo vizuri kama wengine.

Sehemu ya mne yangu inasema mambo ya town....

Com. Salome Muigai: Mama tafadhali sasa tuanze kuenda mwisho mwisho.

Emiliana Chebor: Ndio. Sababu tunajenga kweli vijiji kama Eldoret, Nakuru na popote na hapo ndio utakuta watu wengi wanakuja kukusanyika huko na kutunza ukora ambao watoto wengi watavuta bhang na kila kitu kwa sababu ya kujua kwa wengine. Yangu ni hayo tu na Mungu awabariki.

Com. Salome Muigai: Asante mama, kuna mmoja wa wana tume angependa kukuuliza swali moja kwa hivyo tafadhali ngoja. Mama, tunaswali kwako kwa hivyo subiri.

Emiliana Chebor: Asante

Com. Riunga: Asante sana mama, ungetuambia ile shida ya hawa watoto wanazaliwa nje ya ndoa. Je, uko na mapendekezo gani ili tutatue hili tatizo kubwa ambalo limetuingilia sisi wazazi?

Emiliana Chebor: Mimi kwa sehemu kidogo na akili kidogo nitasema tu ingefanywa sehemu kama pahali pa kutunza hawa watoto, wawe wakiishi huko na sisi pamoja na Serikali. Watoto hawa wapatiwe chakula na masomo mazuri. Kwa sababu wakikaa hivyo hivyo machokoraa na vitu vingine si vizuri.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa maoni yako mama. Tunakushuru. Rael Tirop na baada ya Rael tutakuwa na Dansoi Lwane. Is that your name?

Speaker: (?)

Com. Salome Muigai: Daudi? Daudi Lwane basi utakuwa wa pili kutoka hapo. Mama Rael Tirop yuko?

Speaker: (?)

Com. Salome Muigai: Rael Tirop. Kama ametoka basi tumsikie Daudi. Tafadhali mpelekee Daudi, its okay you can sit where you are, utaletewa mic mahali uko.

Daudi Lwane: Mimi nashukuru kwa vile tumekutana hapa sisi wote, tuweze kutoa maoni. Shukrani kubwa zangu mimi narudishia Commissioners wote ambao wako hapa pamoja na wageni wengine wote. Maoni yangu mimi, jina ni Daudi Lwane na maoni yangu mimi, ninasikitika kuona vijana wenzangu umri wa hii miaka niko nayo wamekuwa hawana kazi. Ie kukosa kazi imefanya wameanza kuingilia mambo mengine mengi, hata wameanza kuiba vitu kwa watu. Ningeomba Serikali kama ina uwezo, isaidie vijana kama wenzangu wa umri kama wangu. Kama Serikali ingekuwa na njia ya kuwafungulia viwanda mahali wawe wanaandikwa kazi hapo, wanapata mkate wao halafu mambo ya wakora nafikiri inaweza kupotea kidogo.

Maoni ya pili: nafikiri ni kwa Serikali yetu ambayo iko saa hizi. Upande mwingine unaweza kupata mtu ameenda kuripoti police station, anaambiwa pesa ya mafuta ya gari na mambo mengine mengi, mtu haweziujua kama atasaidiwa. Unaenda kusaidiwa na bado tena wewe ndio unatakikana kusaidiana huko kwa police station. Sasa hapo ninaomba Serikali kama Katiba inaweza kuwa.....sorry. Yaani Katiba mpya vile itakuwa, wawe wanaangalia mambo mengi kama hayo vijijini.

Mimi hutembea saa zingine town na naona watu wamekaa chini na wana shida mbali mbali. Wameketi tu pale na hakuna vile wanaweza kusaidiwa ama kusaidika na hakuna mtu mmoja ama mwingine ambaye anaweza kuwashugulikia, kuwauliza ama kuwasaidia vile wanaweza ishi. Kama wanaweza jengewa mahali na Serikali waishi hapo na wawe wanalishwa na Serikali. Mambo mengine mengi hata watoto wa mtaani wameteseka, wanaketi hapo na unaweza kuta watoto wanarandaranda mtaani kila mahali. Serikali kama ingeweza kuwa na vile inaweza fungua kitu kama shule, wawe wanachukua kila mtoto hana pesa ama yule ambaye mzazi wake hawezi kumlipia karo ya shule, waweze kupewa masomo kusaidiwa bure.

La mwisho ni kuhusu vile ambayo magari yanabeba watu. Unaweza pata wakati mwingine watu hawa, aliye kwenye gari haoni yule aliye barabarani. Halafu shida ni kwamba waweza pata gari linapita na labda kumenyesha ama kuna vumbi na badala gari lipite kwa barabara, unaweza pata gari limepita likakanyanga maji chafu ama vumbi na linapiga yule mtu ambaye anatembea kando ya barabara bila dereva kuona. So maoni yangu ni kwamba ni afadhali kama kungekuwa na vile hao watu wanaweza chunguzwa na Serikali. Pia watu ambao wanatembea kwa miguu na baiskeli wawe wakisaidiwa pande zingine. Hivo ndivyo maoni yangu yalivyo. (*clapping*)

Com. Riunga: Asante sana David. Sasa tutamuita Mzee Alfred Bor. Mzee yuko?

Alfred Bor: Niko

Com. Riunga: Karibu mzee

Alfred Bor: Asante. Mimi nitaongea Kiswahili ingawaje si kizuri sana

Com. Riunga: Hiyo ni sawa.

Alfred Bor: Basi, yangu mimi nasema hamjambo wananchi

Audience: Hatujambo

Alfred Bor: Jambo tena

Audience: Hatujambo

William Bett: Commissioners, kwa majina naitwa Willam Bett kutoka sehemu ya Sirmat. Sitachukua muda mwingi lakini nitataja maneno machache. La kwanza ni kwamba Constitution ambayo inaundwa sasa iandikwe kwa lugha ambayo inaeleweka, isiwe ikiandikwa na lugha ya mawakili ambapo wananchi hawawezi kuelewa.

La pili ni kwamba, tarehe ya uchaguzi itajwe kwa Constitution ili wananchi wawe wakijua term ikiisha, ni wakati gani uchaguzi utafanywa. La tatu ni safe guarding of the Constitution. Hii ni kwamba ingefaa asilimia ya kurekebisha Katiba iongezwe kutoka 65 ambapo iko wakati huu hadi 75. Kukiwa kutakuwa na marekebisho yoyote, kuwe na opinion vote kwa ile sheria ambayo inatakiwa kurekebishwa. Kwa hayo machache, asante

Com. Salome Muigai: Asante sana na ni machache kweli. Asante sana. Angeline Macharia.

Angeline Macharia: Basi kwa majina ni Angeline Macharia kama mlivyosikia na nina mambo machache tu ambayo ningependa kuguzia. Kwanza kabisa ningependa wakina mama waweze kupewa fursa katika nyadhifa za uongozi kuanzia mashinani. Tuweze kuwa na hata wamama wa mitaa, kuwe na Assistant Chief, Chief, DC na kuendelea katika nyadhifa za uongozi. Pia Mayor achaguliwe na raia kama vile mwenzangu alivyonena hapo awali. Kwa wale wajumbe wetu, ma-councillor pamoja na Wabunge, iwapo wata-prove kuwa hawatekelezi wajibu wao ipasavyo, basi mwananchi apewe mamlaka ya kupiga kura ya kutokuwa na imani kwao na mwingine awekwe mahali pao.

Ningependekeza pia Presidential elections iweze kufanywa independently, isiweze kufanywa pamoja na zile elections za civil seats pamoja na zile za Bunge. Pia kwa hali ya employment rights, kuna wakati mwingine nimeshuhudia cases ambapo iwapo mke ameolewa na mume ambaye anajiona kwamba yeye pengine ako economically powerful, anamlazimisha mkewe kuachishwa kazi. Kwa hivyo ningependekeza kwamba afanye hivyo kwa hiari yake mwenyewe bali isiwe kwa kushurutishwa.

Kuna shughuli nyingine ambayo ni environmental rights. Nimesikia wengi wakisema kwamba zile fundamental rights zao zilindwe na tunasahau mazingira yetu. Nafikiri wale ambao wanaishi mjini kama mimi mtaniunga mkono kwa vili tumeadhiri sana mazingira yetu. Uukitembea mjini ma-councilor pamoja na wale wengine ambao wanafanya council, wanashindwa ni vipi wataweza kukabiliana na uchafu. Kwa hivyo ningependekeza kwamba environment iweze kuwa na right pia ya kuchungwa na wananchi wa mahali pale.

Mwisho ningesema kwa mambo ya rape na ninafahamu kwambo ipo. Ningependekeza kwamba itiliwe mkazo zaidi kwamba kuwe na severe punishment kwa mke ama mume ambaye atamnajisi mwenzake. Ni hayo tu, asanteni.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bi. Macharia na sasa ningetaka kumuita Bi. Emma Kipyegon. Bi. Emma Kipyegon bado yuko nasi? Kama hayuko, David Sato? David Sato.

David Sato: Kwa majina mimi ni David Kirwa Sato, councilor Kapseret. Yangu yatakuwa ni machache sana. Tunataka Serikali ya majimbo, tuwe na Chairman wa county council na awe governor wa hilo jimbo. Mayor achaguliwe na Uasin Gishu mzima na isiwe ma-Councillor peke yao. Chairman ama Mayor asiwe ni mtu mwenye ako na ward, awe ni mtu ambaye atagombea kuwa Mayor au kuwa Chairman, asiwe na ward yoyote. County council au municipal isikubali tena kuwa na mambo ya central Government. Tunataka council ijisimamie peke yao. Kama ni kuamua mambo yao wakishapitisha, iwe imetosha hapo, hawatauliza mambo mengine.

Lingine ni kwamba kwa sababu hapa Kenya tuna shida sana sisi wakulima, na moja ni kwamba ukifika wakati tuna chakula

kama mahindi, tunaambiwa bei ya mahindi imeshuka chini na ni kwa sababu hii tunapata tajiri mmoja ama kikundi cha watu wanatumana mahindi kule nje. Langu ni kwamba Parliament yenyewe, kama hakuna chakula nchini, Parliament yenyewe ijadiliane na ione ni chakula kiasi gani tunataka ku-order kutoka kule nje. Hao wenyewe wapitishie na chakule kitoke nje, kwa sababu tuna chakula kingi na bado wanatoa chakula kule nje. Hivi majuzi wakati tulikuwa tunavuna ng'ano nilikuwa Mombasa na milioni meli mbili zimejaa ng'ano na upande huu tukitaka kuuza wananunua kwa bei kidogo. Kwa hivyo ninaonelea Parliament ipitishie ya kwamba chakula zitoke nje. Lingine ni kwamba.....

Com. Salome Muigai: Bwana Diwani sasa tupe la mwisho, tulikata tukaacha 3 minutes.

David Sato: Yah. Tuna mambo kama bar. Nilikuwa naonelea ma-bar zifunguliwe saa kumi na moja na zifungwe saa tano. Watu wafanye kazi kuanzia morning mpaka saa kumi na moja waende kunywa pombe. Hiyo tu ndio maoni yangu nilionelea, tukazie hapo. Nafikiri kama Madam ungeniruhusu, ningengeza ya kwamba uchaguzi uwekwe siku yake binafsi, isiwe ni ile Rais mwenyewe anasema itakuwa siku fulani. Saa hii kama mimi ningekuwa ninajua siku fulani nitashika kiti ama nitaanguka. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Diwani. Moses Chelule.

Moses Chelule: Honourable Commissioners, kwa majina naitwa Moses Chelule.

- Nitaanza kwa kueleza aina ya Serikali ninayotaka itutawale. Ningelipenda Serikali ya shirikisho, yaani majimbo.
- Pili, tunataka Serikali ambayo inakuwa na Senate ambayo itawakilishwa na watu wawili wawili kutoka kwa kila kabila.
- Tatu, tunataka majeshi yote iundwe ki-Katiba.
- La nne tunataka vyama vya siasa viwe vichache kama viwili au vitatu. Tungelipenda Serikali iundwe kama ile ya sehemu zingine kama Europe ambapo mtu hawezi kupewa wakati, anaweza kutawala bora bado anapendwa na wachaguzi.
- Tungelipenda Serikali yetu iwe na Bunge mbili, upper house na lower house ili iwe kamilifu. Mamlaka ya Serikali yetu iwe chini Bunge.
- Mahakama iwe huru.
- Tena tungelipenda tuwe na tribunal courts kutoka kule nyumbani maana huko ndiko kuna kazi nyingi.
- Serikali za mitaa ziwe na mamlaka kamili hasa kufuatana na shamba na mambo mengine mengi, kama ya ardhi.
- Raia awe na kinga ya kimsingi yaani awe na haki yake kule nyumbani.
- Ardhi na mali ya asili irudi kwa local Government yaani Serikali za mitaa.
- Title deeds ziwe freehold wala si leasehold kama vile inavyo kuwa hapa Uasin Gishu. Mali ya asili, mwenye shamba awe na haki kama mali yake maanake Serikali huwa inasema futi tatu ni ya mtu binafsi lakini zile zingine zinakuwa ni za Serikali. Tungeliomba yote iwe ni ya mwenyewe mali.

Com. Salome Muigai: La mwisho Bwana Chelule

Moses Chelule: Uhusiano wa Serikali ubaki katika Serikali kuu.

- Na mwisho ningelipenda wazee wa mitaa wapewe marupurupu. Asante sana Commissioners.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee. Mr. Alex Beigut.

Alex Beigut: Thank you. The first thing I would like to say is

Speaker: Your name?

Alex Beigut: My name is Alex Beigut. The truth is that the present Constitution has not been a failure that we say it has been but I think it is the application that has been the failure. However, because we have more or less agreed that we want to review the Constitution, let me give a few suggestions. The biggest failure in the present Constitution I think is Parliament. It has not done the work that it is supposed to do in checking the powers of the Executive and in ensuring that public funds are properly used. Therefore, I would like us in this exercise to focus on the checks and balances of Government so that it can deliver services to the wananchi.

We should retain the unitary system of Government; we should retain the Executive President. However, I think we should limit or reduce the Parliamentary term and the Presidential term to 4 years. The President should be able to hold office for only two terms. Members of Parliament should not be appointed to cabinet position. The Executive should be able to find its own cabinet members from outside parliament. I think that has been the biggest failure of our present Constitution because a cabinet position is a bribe and you cannot expect Parliament to check the President if they are looking towards these bribes.

Parliament cannot decide their own salaries. There should be another body that can decide the wages or remuneration of parliament. In the event that we do this Constitutional review, we must not limit the time in which we are to discuss this Constitution. It could be a terrible mistake, even if it has to spill over to the next 10 years, let's do a Constitution that will last for the next 200 years. So I think that once we are through with the paper work of the Constitution, we should not even allow one Parliament to decide on the fate on the Constitution, but it should be reviewed by 2 consecutive Parliaments, that is for example the 9th Parliament and the 10th Parliament before this Constitution can be taken into effect.

A referendum at the end of this exercise is a must, is necessary, and we should be able to approve it by at least a majority of more than 51%. Parliament should also be able to approve Presidential appointments in parastatals or Government bodies and judges. There should be public hearings for appointment of judges so that we can be sure that the judges that hold position are

people of intergrity. These hearings should be public.

We should scrap the provincial administration and replace it with district administration, but we should re-organize the district administration into a more manageable number of districts between 15 and 20.

Com. Salome Muigai: Can you give us your last suggestion?

Alex Beigut: Government departments must be reduced and Government size must be circumscribed by the Constitution. I think the maximum number of Government employees should be around 50,000. Finally, representation must be proportional, that is if the constituencies must be equal in population, or voting in Parliament must be done on a weighted basis, so that if I have gone to Parliament with 2,000 votes, my vote is not equal to that of a member of Parliament who has come in with 100,000 votes. Thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you very much. Is Rael Martim here? Rael Martim?

Speaker: Aliongea

Com. Salome Muigai: Alishaongea tayari?

Speaker: Ndio

Com. Salome Muigai: Okay, now (?) Patricia Sawe. Karibu

Patricia Sawe: My names are Patricia Sawe; I come from within the municipality that is Mwanzo. My views are both men and women with disabilities should be given assistance by the government, e.g. by being given loans to do business so that they can help their families. Another point is that women should be given 35% of job opportunities e.g. in Parliament and civic. We should also have women Managing Directors in organizations and also like Vice Chancellors in public universities and Principals in teachers' colleges.

Girls from poor families who have passed their KCSE examination for example should be assisted by the Government to join public universities so that they can get better jobs in future. Any woman who has been married in customary law should be given a certificate so that it helps them incase they want to do anything. Both girls and boys should be given right of ownership of their parents' property such that girls are not discriminated upon.

Land ownership, I think has been said many times, it should be joint so that the husband should avoid selling the land and leave

the children suffering. On the agricultural issue, sector rather, it should be scrutinized seriously because the common man is suffering. That is all I have.

Com. Salome Muigai: Thank you maam. Philip Kiprono? Philip Kiprono. Lawrence Chirchir, Lawrence Chirchir? Elijah Kimei? Elijah Kimei? Chumo Maina, oh, Elijah is here, okay. Ulikuwa umeongea?

Speaker: (?)

Com. Salome Muigai: Bado. Basi ni nafasi yako una dakika tatu. Tupe pointi tatu za muhimu.

Elijah Kimei: *Kainenyun ko Elijah arap Kem ei.*

Translator: Kwa majina ni Elijah arap Kimei

Elijah Kimei: *Abunu Kapseret location.*

Translator: Anatoka upande wa Kapseret

Elijah Kimei: *Sub location ko Lemok.*

Translator: Lemok kata ndogo

Elijah Kimei: *Ko amwae kongoi missing en betut ne kokikonech kebwan nyo ke mwa agoba kaimutik che kigere komi.*

Translator: Anashukuru sana kwa siku hii njema ya kuchangia maoni yake

Elijah Kimei: *K o ne tai amwae agoba meng'atosiek ana kiwattet.*

Translator: Kwanza anataanza na mipaka

Elijah Kimei: *Noton ko majimbo.*

Translator: Hiyo anataka Serikali ya majimbo

Elijah Kimei: *Si mamichi ne mangen kole maba kutit ab bichotet yuniton, komengisie kokergei ak bik..*

Translator: Anasema kwamba iwapo kuna mtu atapatikana akiishi katikati ya makabila mengine, aishi pamoja na hao watu

Elijah Kimei: *Anan mabakoyai kiy ne mateben bichuniton.*

Translator: Lakini hana uwezo wa kufanya kitu chochote bila kuafikia na wakaazi.

Elijah Kimei: *meng'isie kosipkeny akamun imbarenyin.*

Translator: Ataishi kwa sababu shamba ni lake

Elijah Kimei: *Ak yemach kokoita kokachin bichoton.*

Translator: Lakini iwapo anataka kupeana atapea wakaaji wa hapo.

Elijah Kimei: *Ng'aliot age neba oeng'*

Translator: Jambo la pili

Elijah Kimei: *kosomanosiek en lagok.*

Translator: Ni mambo ya elimu.

Elijah Kimei: *Ateleli koini aba Kaniset ab SDA.*

Translator: Yeye akisimama hivi, ni mshiriki wa dhehebu la ki-adventista SDA

Elijah Kimei: *Akere ko nyalidos lagokyok en somanet.*

Translator: Anaona kwamba watoto wao wanateseka kielimu

Elijah Kimei: *Ingoit betut ne ataimunye Jumamos*

Translator: Ikifika wakati wao wa kuabudu ambao ni Sabato yao siku ya Jumamosi

Elijah Kimei: *kelenji obwan sioyai testi ra.*

Translator: Wanaambiwa kwamba muje shule kwa sababu mitihani inafanyika.

Elijah Kimei: *. Koyeyesio kowa*

Translator: Wakikataa kuenda

Elijah Kimei: *. Ib kewon mutai*

Translator: Wanafukuzwa siku ifuatayo.

Elijah Kimei: *. Noton komakatiagnatet neba saet*

Translator: Huo sio uhuru wa kuabudu.

Elijah Kimei: *Asome ale kinde en ng'atutik konyor betunyan ne imunyei.*

Translator: Anasema kwamba muweke ndani ya Katiba siku hiyo yao ya Sabato ipate kutambuliwa na Katiba siku yao ni siku ya jumamosi.

Elijah Kimei: *Ingo mi boisiet ab Serikali, komunyvko sabato kora.*

Translator: Kama ameajiriwa na Serikali, apumzike siku hiyo.

Elijah Kimei: *ingo asikarindet ii komuny kora.*

Translator: Kama ni askari apumzike siku hiyo

Elijah Kimei: *Iya kokami kiy ne kawo missing.*

Translator: Labda kama kuna jambo la dharura.

Elijah Kimei: *mie kesiki chichoton kamunget.*

Translator: Anasema kwamba huyu anastahili kuandikiwa mambo yake

Elijah Kimei: *Amun kikere lagokyok betut yon kait*

Translator: Tunaona watoto wetu wanapofika

Elijah Kimei: *Ingo mi sekondari.*

Translator: Kama ako katika shule ya upili

Elijah Kimei: *kelenjin obaisien Jumamos.*

Translator: Anaambia afanye kazi siku ya Jumamosi

Elijah Kimei: *Oko jumapili melen kele somani.*

Translator: Na Jumapili pia hawasomi

Elijah Kimei: *Katabaisye Jumapili koyai boisionikwak amun mutai kobwane sukul.*

Translator: Hawangelazimishwa, wangewachiliwa wafanye kazi hiyo Jumapili

Com. Salome Muigai: Tumepata jambo hilo la Sabato. Endelea kwa jambo lingine.

Elijah Kimei: *Ngaliot age ne miten*

Translator: Jambo lingine

Elijah Kimei: *Kokwaet ab kirwagik.*

Translator: Ni uchaguzi wa Chief

Elijah Kimei: *Mie ingekwae sub- chieft*

Translator: Anasema kwamba anataka wachague sub-Chief na wakati sub-Chief anachaguliwa

Elijah Kimei: *Anan ko chief*

Translator: Au wakati Chief anachaguliwa

Elijah Kimei: *Ko tilu bik.t*

Translator: Iwe inapitia mikononi mwa wananchi

Elijah Kimei: *Ko kagi birchi kura bik.*

Translator: Watu wampangie laini apigiwe kura.

Elijah Kimei: *Ke nai ke le chichi koyame koik kirwakindet.*

Translator: Itambulike vizuri kwamba yeye anastahili kuwa kiongozi.

Elijah Kimei: *Makimache cho kilelen koyai interview.*

Translator: Hatutaki maneno ya kuenda kufanyiwa interview kule kwa ofisi ya DC

Elijah Kimei: *Akityo sikwam rabinik akityo koalen chito baunatet*

Translator: Halafu watu wanaenda na pesa kwenda kumnunulia mtu uongozi.

Elijah Kimei: *koik chit one maiyani bik.*

Translator: Mtu atapita ambaye hatakikani na watu.

Elijah Kimei: *Ko nateben bik kolelen makimache kouni , komache kole kimaosiron.*

Translator: Lakini watu wanapojaribu kumuuliza vile anatekeleza wajibu wake, anaanza kuambia watu sio nyinyi mliniajiri.

Elijah Kimei: *Kole kimaokwayon.*

Translator: Anasema sio nyinyi mliniteuwa

Elijah Kimei: *kikwaan Serikali.*

Translator: Ni Serikali imenileta hapa

Com. Salome Muigai: Tupe la mwisho

Elijah Kimei: *Ko aker en yoton ale,*

Translator: Hapo ameona kwamba

Elijah Kimei: *Mie kowa ng'atutik asikobit ingeyae boisio aketugul ii, kingen ole kabunu ng'atutiet.*

Translator: Kila kitu kiingie ndani ya Katiba ndio chochote kitakachofanyika kiwe kwamba ni Katiba ndio imesema

Elijah Kimei: *ko kongoi ingobachit yoton.*

Translator: Anasema asante, yake imefika hapo.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Zipporah Maru? Zipporah Maru. Chumo Maina?

Speaker: Aliongea

Com. Salome Muigai: Aliongea. Japheth Samwei? Japheth. Gabriel Tarus.

Gabriel Tarus: Majina ni vile umesema, Gabriel Tarus. Commissioners na wenzangu, mimi nimesimama hapa kwa niaba ya wakulima. Mengi yametajwa lakini nataka kujumulisha yote nikisema kwa upande wa wakulima na shida zao. Ya kwanza kwa sababu wakulima wana-fall ndani ya uongozi wa nchi hii, nitasema kidogo yale ambayo pia hata wao wangependa wapate. Na nitasoma tu speedily.

We need a majimbo Government of the district, kumaanisha kwamba majimbo yako ya aina nyingi lakini kwetu sisi ni vile mumekuja, mahali tuko sasa tungependa tusikizwe kama wananchi wa upande huu. Mengi yamesemwa juu ya mahali pa kuishi lakini mzee mmoja ameongea juu ya watu kuishi pamoja na wananchi wengine. Ni watu ambao wataishi kama wageni na wako na nafasi yao wakitaka kutoka wanaweza kuuzia wananchi shamba. Kwa ufupi ninataka kusema tu Mungu alijua vile alifanya kwa sababu tulijikuta tumeumbwa na tumezaliwa upande wa Nandi. Kwa hivyo ninataka mchukue tu maneno haya kama yanatoka kwa matamshi ya Wanandi wa hapa. Hivyo ndivyo tunataka kwa upande wa majimbo.

District governor to be elected by the people of the district. Mayor kama vile wengine wamesema, Mayors to be elected by all the electors of the district. The Constitution to be the supreme law, and nobody, even the President of Kenya to be answerable to the Constitution. MPs to be full-time MPs, and Ministers should not be MPs. MPs to open offices in constituencies with a secretary and assistants paid by the Government. Hivi ni kusema kwamba tungependa wawe na ofisi karibu ili vile mwenzangu amesema, tukiona mambo yake haikuji kabisa, hatupati services za yule MP ama hata councilor, tuna uwezo wa kumuita na tuseme hatuna confidence naye na tum-replace.

Only 3 political parties to be allowed. The Government to provide money to every political party. Leader of the official opposition party to be paid and given security by the Government. The Constitution to give priority to agriculture as the backbone of our country. Tunaona kama sisi wakulima tumechukuliwa hivi hivi ili kwamba tunapigania kuona kwamba kweli Mungu alifikiria sisi na tunapata mvua mzuri na tuna rotuba nzuri ambayo tungestahili ama tuilizwe kwa nini hatuja produce. Na wakati tunajikaza mpaka tuna-produce, wakati inapokuwa tayari nyingine tayari inashuka, iko Mombasa kwa meli, tunashangaa huo uwezo unatoka wapi? Kwa hivyo tunauliza Commission hii ipeane maneno yetu.

The importation of agricultural produce before the local one has been cleared itoke kabisa. No importation of agricultural produce before the local one has been cleared. Indigenous Kenyans and farmers or their organizations such as UGNC, mahali ninatoka kama Chairman wao, to deal with agricultural inputs such as fertilizers, seeds, chemicals na hizo zingine. Hii itawapatia nafasi nzuri ya kuchagua ni kitu gani kizuri kwao, kama vile mzee mwingine amelalamika juu ya kuuziwa chemicals ambazo ni mbovu hazifanyi kazi. Sisi tukipewa hio nafasi ya kuangalia, tutaangalia ni gani ambayo ni mzuri kwa wakulima wetu. Na pia.....

Com. Salome Muigai: Tupe point yako ya mwisho.

Gabriel Tarus: Point ya mwisho. Nilikuwa na point nyingi lakini chukueni hiyo.....

Com. Salome Muigai: Tupe memorandum ukishamaliza

Gabriel Tarus: Basi. Mimi nataka kusema kidogo tu juu ya court. Kortini tumekuwa na madalali ama hawa watu ambao tunawaita court brokers ambao mara nyingi kama mtu anadaiwa anaenda anapewa hiyo nafasi ya kwenda ku-harass. Zile pesa anaenda kuchukua kule anapata nafasi nzuri ya kuchukua hata pesa zaidi ya ile mali anadaiwa na mambo yake inaishia hapo kwa sababu anaenda kuuza mali ya yule na haiwezi kufika mahali ambapo ilitarajiwa iende. Kwa hivyo hayo mambo ya madalali ama court brokers iangaliwe vizuri sana sheria zao.

Niko na mengi lakini kwa sababu ya nafasi, nitafikisha hapo. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Tarus. Sasa ningetaka kumuita Bi Linet Otwor. Bi. Linet Otwor? Sabina Wairimu?

Sabina Wairimu: Asante. Kwa majina naitwa Sabina Wairimu na yangu ningetaka kuguza juu ya Judiciary. Haya maneno yamezungumzwa na watu wengi na mimi nimeona mengi. Suggestion yangu ni Judiciary iwe independent. Haya maneno ya kuwa na kesi kortini, watu wengine wamehongwa, mnatafuta file inakosa, hiyo ingizwe kwa Constitution, Judiciary iwe independent. Kitu kingine juu ya Judiciary, kesi zinachukua miaka mingi, justice denied. Unaenda kortini mwaka twende

mwaka rudi na kesi hiyo haikwishi kwa kuwa mtu ambaye mnaenda kesi naye ana pesa za kuhonga, na amehongana mpaka wewe utaishi kwa hiyo kesi maisha yako. Mimi ni mmoja wao. Niko na kesi ya miaka kumi na mbili sasa, na tunataka hiyo maneno yaangaliwe.

Ndani ya Constitution, tungetaka tuingiziwe maneno ya environment. Ukiangalia estates zetu ni kitu cha kushangaza sana. Unakuta kwa estate, makaratasi ya green, blue, black, white, ni kama decoration. Tungetaka ipitishwe ndani ya Constitution ili yule atakaye haribu environment awe ako na fine atatoa ili tuweke nchi yetu kama nchi zingine za nje. Wengine tumetembea na hakuna kitu walifanyiwa isipokuwa wewe uwe concerned, mwingine awe concerned. Tunaweza kufanya hii nchi yetu...

Com. Salome Muigai: Zungumzia kwa mic Bi. Wairimu tafadhali.

Sabina Wairimu: Okay.

Com. Salome Muigai: Zungumzia kwa mic.

Sabina Wairimu: Tunaweza fanya hii nchi yetu iwe maridadi zaidi kila mtu akichunga laini yake. Kitu kingine ni haya maneno ya wakina mama na bwana zao. Yes, sikatai watu wanaweza kuachana. Lakini watu wakiwachana, hatuoni kwa nini mnavurutana kortini kwa sababu ya mali, na hiyo mali mlitafuta nyinyi wote wawili? Mtu mmoja akue ako na pesa ya kuhongana kortini mpaka unasumbuliwa, ile kazi unafanya, huna pesa, una tumia kwa ma-advocate. Tunataka Constitution...

Com. Salome Muigai: Unapendekeza nini?

Sabina Wairimu: Tunapendekeza iwe kitu kama mumeachana iwe kitu straightforward, mtu apatiwe haki yake na mwingine aende na haki yake. Na nikisema hiyo ni maneno nime-experience. Lingine ni juu ya public transport katika nchi hii. Imekuwa kitu cha maajabu. Sikumbuki ni mwaka gani lakini tulikuwa na accidents mingi sana na Serikali ikatufanyia msaada mkubwa wakasema overloading ikwishe na tukaambiwa imekuwa law. Ilifanywa kuwa law kwa wakati mfupi na haya maneno yamerudi tena. Unaweza kuona katika bus watu wamesimama, watu kama 50 katikati ya bus na ukiingia ndani uliambiwa kuna kiti. Wakati umeingia ndani unakuwa kama mahabusu. Tunataka Serikali, ndani ya Constitution wapitishie kwamba hakuna overloading, kila mtu akae vizuri kwa maana unalipa. Wakati mwingine ninajiuliza, accident ikifanyika na zinafanyika, mimi naona kama watu wengi wanakufa kwa sababu ya msongomano huo wa bus na unalipishwa sawa. Tunaona polisi kwa barabara na unaona conductor ametoka, amepeana kitu na bus inaendelea. Sasa wengine tunashindwa, kwa nini hili jambo haliwezi kuzuiliwa kabisa kama vile tuliambiwa?

Kitu kingine, ndani ya Constitution yetu, ningetaka labda tuwekewe, maneno ya sigara. Si kila mtu anataka kuvuta sigara, na wale ambao wanavuta sigara katika nchi hii yetu hawana fikira za wale watu wengine. Kama unavuta sigara, uvute sigara peke

yako lakini usifanye mwingine anuse hiyo harufu ya sigara kama hataki. Kuwe kama wakati unaingia kwa ndege, kuna section ya wenye wana-smoke na iko section ya wale wengine ambao hawa-smoke. Nchi hii, kama unavuta sigara, unaweza kuwa unakula na mtu na baada ya kula anawakisha sigara. Hajali kama hakuna mtu mwingine ambaye hataki hiyo harufu.

Com. Salome Muigai: Hiyo point tumeshachukua.

Sabina Wairimu: Umechukua?

Com. Salome Muigai: Ndio. Tafadhali nenda kwa nyingine kama unayo na iwe ya mwisho mwisho.

Sabina Wairimu: Asante. Hii nyingine ni ya wanawake. Sisi kama wakina mama, tuliambiwa kumepitishwa law ya sexual harassment. Tungetaka ndani ya constitution hiyo, hii sexual harassment iwekwe maanani na iwe ni sheria kabisa, ili mtu akinitusi mimi kama mama, uwe unaweza kwenda polisi ama kwa sheria na huyu mtu achukuliwe hatua, akomeshwe, hayo maneno awachane nayo. Nimesana hiyo kama, hebu nipeana kidogo tu. Juzi nilikuwa nasukuma gari kama imekataa kwenda. Nilikuwa nasukuma na wanaume wengine na wakati mwanaume mmoja aliona ni mama anapeleka gari aliniuliza, "mama, kama hauna petrol, si niuingie petrol station uweke gari mafuta?" Mimi nikajiuliza, kama alikuwa mwanaume mwenzake, kweli hata angefungua mdomo? Tunataka hiyo sexual harassment ijulikane na kila mtu vile ilipitishwe kuwa law, wanaume wasitutishe hivyo kwa kuwa wameona ni skirt wearer, hatutaki.

Com. Salome Muigai: Neno la mwisho? Sitaki kukutisha ukiwa skirt wearer.

Sabina Wairimu: Kitu kingine, ndani ya Constitution yetu tungetaka, kama sasa tunaenda kwa uchaguzi. Wakati tunachagua wabunge, ningeliza ndani ya Constitution, hawa Wabunge wakati wanachaguliwa, hatutaki wakora. Wengine ni watu wameiba mali ya uma, wengine walikuwa wakora wa aina fulani. Tungetaka mtu achunguzwe vizuri ili tujue wale tunapatia hiyo kazi ni watu waaminifu, mtu ambaye hatatuletea aibu hata kidogo. Asante

Com. Salome Muigai: Asante sana. Job Sitienei. Job Sitienei. Phillip Sirma?

Phillip Sirma: Jina langu ni Phillip Sirma kutoka Kapseret. Tume, neno la kwanza ambalo nataka kusema ni, kwa sababu mimi ni mkulima na tunapata taabu sana kwa sababu ya vitu vyetu ambavyo tunauza. Kwa mfano kama mahindi, tunavuna mahindi, ngano, maziwa na vitu vingine kutoka shambani lakini Serikali inangoja wakati huu kama vitu viko kwa shamba kama mahindi, ngano na maziwa, wanaleta mahindi nyingine ama ngano nyingine ama maziwa, kutoka nchi zingine. Kwa hivyo mukomeshe hiyo ndio sisi wakulima tupate soko mahali pa kuuza vitu vyetu.

Kitu kingine, Wakenya wote wapate matibabu ya bure kwa hospitali. Wazee wote wa umri wa miaka 70 na zaidi walindwe na

Serikali kwa matibabu na kutunza haki yao. Watoto wote wapate elimu ya bure kama wazazi hawajiwezi, kupata pesa ama chakula, makao, haki ya kupata kazi. Wakenya wote wapate habari zozote kutoka kwa Serikali, kama ni matangazo. Kutangaza kila kitu kijulikane, kama hizi sheria ambazo tunatunga saa hii, ikiwezekana, zikifika Nairobi na zikisha jadiliwa, watangaze Kenya nzima ndio kila mtu asikie ya kwamba hivyo vitu vimekubalika. Mkenya wowote aweze kuwa na shamba kiasi apendacho, apate haki bila kiwango.

Com. Salome Muigai: Bwana Sirma, tafadhali usitusomee kila kitu, tuelezee tu yale ya muhimu na sisi tukitupa hiyo memorandum, tunakuhakikishia ya kwamba itasomwa.

Phillip Sirma: Mimi nasema tu mtu akiwa na shamba yake ambayo amenunua na mali yake, ilindwe isimsumbue huyu mtu kusema itakatwa shamba lake ama itafahyiwa hivi kwa sababu mali ni mali. Shamba ni kama mtu ambaye anafanya biashara kama duka na kadhalika. Kwa hivyo hiyo ni haki ya huyo mtu, awe na hiyo mali na Katiba ni lazima ilinde huyo mtu na mali yake.

Wageni wasio Wakenya na wasiwe na ruhusa ya kumilika shamba. Itakuwa lease peke yake, yaani mtu mgeni kama Muhindi, Mzungu na kadhalika, akiwa na.....

.....*End of tape 6 side A*

Phillip Sirma: Asiwe kama mwananchi wa Kenya.

Com. Salome Muigai: Jambo la mwisho (?)

Phillip Sirma: Jambo la mwisho, Serikali iwe ya majimbo kwa sababu tukiweka majimbo ni rahisi kila jimbo kutatua mambo yao kwa jimbo lao. Asanteni.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Bi. Emily Kurgat. Bi. Emily Kurgat? Moira Chepkok? Moira Chepkok? Kina mama wameshaenda nyumbani wote? Tony Kirwa? Na utafuatwa na Dave Chepsiror.

Tony Kirwa: Kwa majina naitwa Tony Kirwa. Nitaanza na Katiba yenyewe. Ningeomba kuwa Katiba ya Kenya sasa itengenezwe vizuri kuliko vile ilivyo sasa. Ukiona nakala ya juu ya Katiba ya Kenya, haijatengenezwa vizuri, kwa hivyo tunataka kusema katika ile cover ya juu ya Katiba, tuseme we invoke God's name, in God's name tunaweka juu. Katikati ya hiyo tuweke emblem ya Kenya, court of arms in colors. Halafu bendera ya Kenya lazima iwe kwa Katiba katika cover ya juu na tunasema juu ya Katiba kuwa hii ni Katiba ya Kenya. This is the Constitution of the federal democratic Republic of Kenya. Unapofungua cover ya pili baada ya page ya kwanza, lazima tuweke wimbo wa taifa, kwa sababu wimbo wa taifu haupo katika

Katiba ya Kenya. Lazima uweko kwa lugha ya Kiswahili, lazima uweko kwa lugha ya Kiingereza na katika lugha zingine ambazo zinazungumzwa katika Kenya.

Page ambayo itafuata tutaweka Preamble, tuseme sisi tunasimamia nini katika nchi hii, historia yetu. Katiba ya Kenya, ningetaka kusema pia, although we need a federal structure of Government, we are going for the plural collegiate kama ya Switzerland. Ili katika kila jimbo, Parliament ya kila jimbo ichague mtu mmoja wa kuenda ku-form federal council Nairobi, ili kila jimbo la Kenya lina mtu wao ambaye ni Chief Executive. Kama ni kula itakuwa ni wakati wao kula kwa sababu Katiba ya sasa inasema President wa Western akienda tunasema watu wa Western wameenda kukula sasa. Tunasema Wakikuyu walikula, Wakalenjin wanakula sasa, it is our turn to eat. So the best way to cover that is to make sure that every region has a representative in the federal council. Halafu wao wazee au wamama wakikutana huko, wanachagua mtu mmoja tu kwa mwaka mzima ambaye atakaa State House, na huyu mtu hatakuwa na nguvu zaidi kuliko hawa watu wengine ambao wametoka katika kila jimbo. Hawa watu, kama tutakuwa na majimbo saba katika Kenya, na mimi nina-propose kuwa Rift Valley kwa vile ni kubwa sana, igawanywe iwe mbili, tuwe na North Rift na South Rift. Na Nairobi iwe kama Washington DC, ni ya nchi nzima sio ya jimbo fulani tu peke yake.

Wale ambao wamechaguliwa kutoka kila jimbo, hawa ndio watashikilia the key ministries za nchi na wale mawaziri wengine si lazima wakuwe wajumbe. Wale wazee watakaa pamoja wachague ni Minister gani tutaweka, wakiweka maanani majimbo ambayo yako katika Kenya na maneno ya wamama pia ya special interest to be catered for, maybe disability na kadhalika. Na tuwe na two houses, senate na lower house. Senate, kila wilaya itatoa watu wawili kuenda senate, moja wa hawa wawili atakuwa ni mama. Katika kila jimbo kutakuwa na Parliament ya jimbo fulani, kama ni North Rift itakuwa na jimbo la hapa na Parliament yake itakuwa hapa Eldoret. Hiyo Parliament, watu watachagua watu kutoka divisions, tuchague mjumbe ambaye ataenda hapo kutoka division. Hawa wajumbe wakikaa ndani ya jimbo, wachague mtu mmoja anaitwa Chief Minister ambaye atakuwa mkubwa kama Rais huko Nairobi. Na hiyo jimbo, Serikali ya central Government itakuwa na macho yao katika region kwa mtu ambaye ataitwa Regional Administrator, ambaye si lazima atoke hilo jimbo, atakuwa ametoka katika jimbo lingine

Katika Katiba yangu pia nina-propose provision for independent candidates.

Com. Salome Muigai: Na dakika tatu ni chache kabisa kueleza Constitution nzima, kwa hivyo ungeeleza jambo la mwisho basi.

Tony Kirwa: Asante. Tutakuwa pia na referendum katika Katiba ndio maneno yote lazima ipelekewe watu waongee juu yake. Fundamental rights, lazima kuwe na fundamental duty na lazima pia kuma mambo ambayo wananchi lazima waseme. Nataka kusema kuwa terms ya mjumbe irudishwe kuwa miaka nne na pia two terms. Mjumbe lazima aende two terms peke yake. Kama anataka kuendelea tena lazima arudi kwanza halafu tena aende baadaye. Kama mtu atapiga kura akiwa na miaka 18,

inaonekana anaweza kuwa mjumbe pia. Huwezi sema miaka 18 mtu anapiga kura halafu miaka 21 anakua mjumbe. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Sarah Wepukhulu? Sarah Wepukhulu? Na utafuatwa na Ruth Kinavi. Is Ruth here?

Ruth: Yes I am here

Com. Salome Muigai: Oh, you have one group? Okay. So you will give us your name.

Ruth Kinavi: Good afternoon Commissioners and the members of the public. My names are Ruth Kinavi; I represent FOCUS, which stands for Fellowship of Christian Union Associate Members. We are drawn from professionals, various professionals who are Christians here in Eldoret. Otherwise, FOCUS is a fellowship actually for Christian Union amongst universities, and colleges, and high schools. We have a memorandum, which we have drawn of 16 pages, however I would like to just highlight certain aspects that the other members would like the rest of the public to hear.

For the Constitution, we propose that the Constitution of Kenya, is basically as it is but with certain aspect that we have highlighted: like we proposed that we have a Preamble. The (?) and establishes, and gives the vision of the nation as well as declares the will of the people. Other than that, we feel that the Constitution is supreme and should not be easily amended. In regard to the structure of the Executive, talking of the President and the Ministers, and cabinet, FOCUS associate members feel that we actually opt for an elaborate structure. Like my colleague who has just been here has stated, but we feel that we should actually have a President and Vice President who are running mates from one party. After that, they should be actually be in a position. They should not come from any constituency. Other than that, the Ministers should also be partyless. So even as we are thinking of the President and Vice President being ex officio members to the Parliament that means that they should not have any constituency. Based on their profession, that is where we draw our rationale from, that these are professionals actually working towards the good of the public.

With regards to the bill of rights, I would like to just highlight one or two points that FOCUS has actually looked at, especially in this last year on the right to abortion and capital punishment. We have felt that, giving it a Christian perspective, we should deny the right to abortion and as well abolish capital punishment.

With regards to citizenship, we feel that non-Kenyan men can actually acquire citizenship if he marries a Kenyan woman, however we propose a five year period first to ensure that it is not easy to acquire Kenya citizenship. Secondly, to ensure that there is some contribution made to our economy within that period of time.

Com. Salome Muigai: You have one more minute maam.

Ruth Kinavi: With regard to public assets, we feel that this should be accessible to public scrutiny especially before exploitation or being bequeathed to private entrepreneurs, to ensure that the public knows what is being exploited and what is available to the country. I believe that would be a highlight, it is just a small highlight. Otherwise, our memorandum is 16 pages, which we shall hand in. Thank you.

Com. Salome Muigai: I have a question for you. Any question from the rest of us? I have a question for you. You said that abortion should not be legal.

Ruth Kinavi: Legalized

Com. Salome Muigai: Should not be legalized. In the present Constitution its only 50% of the abortion that is not legalized because the man can say he made a baby and he is not interested. **Com. Salome Muigai:** That is abortion of 50% of the foetus, of the baby. So are you talking of the remaining 50% or are you revisiting the whole issue and saying that we need to look at it anew?

Ruth Kinavi: Okay, I will also call upon my.....

Com. Salome Muigai: No you cannot because you are not a Chairmadam, am sorry

Ruth Kinavi: Oh, sorry

Com. Salome Muigai: But could you please, in your discussion

Ruth Kinavi: Yes?

Com. Salome Muigai: How did you look at it, did you look at it as abortion, as the foetus carried by the woman, or did you look at the whole thing and said that a baby has been born or made by a father and a mother, and we are talking about the totality of that abortion and their full responsibility?

Ruth Kinavi: Not to sound ignorant to what was actually discussed because at the time we were having these series of discussions, I only happened to attend the final and that was not much. So we have the other members who I came with. Can I call upon them Madam Chairman? Chairperson rather?

Com. Salome Muigai: Yes for that one

Ruth Kinavi: Yes please

Com. Salome Muigai: And since you (?) like me, I am rigging this

Ruth Kinavi: I am sorry, I should also have introduced them

Com. Salome Muigai: No, that is okay

Ruth Kinavi: Because we came as a team

Com. Salome Muigai: Okay

Ruth Kinavi: I am sorry madam.

Speaker: Thank you for the opportunity. I think the part that we are referring to is the physical abortion, because we realize that most of the people who are debating about abortion happen to be men and they are talking about taking care of the woman. It is like they want the woman to abort so that she is taken care of. But you see that the guilty conscience that the woman carries around, the men are not aware. So the part that we are talking about of whether the father denied the child, that means the father has aborted the child that is what I understand. That one we leave to the fathers to know what to do about it. If they want to be irresponsible, we leave it for them. But now, for the person who is carrying the baby for her to go to hospital and have the child removed, or go to some back streets and have the child removed, that is what we are saying no to. Because we believe life is God given and some of the people whom we are aborting could be the Presidents we are looking for.

Com. Salome Muigai: Thank you very much. Thank you very much FOCUS. David Chepsiror. Mary Njambi?

Speaker: (?)

Mary Njambi: Wenzangu hamjambo.

Audience: Hatujambo

Mary Njambi: Mimi naitwa Mary Njambi kutoka Eldoret town. Kwa uongozi wa Rais, Rais ako na mamlaka sana na inatakiwa awe chini ya wananchi, anaamua kwa maana anasema na kufanya na haitakiwi hivyo. Tena tunataka Rais awe mtu ambaye yuko na familia, hatutaki mtu ambaye yuko peke yake, tunataka ajue masilahi ya wamama wakati wanakaa pamoja.

Ndoa; wazee wanatuoaji sisi na tunakaa na wao pamoja na hakuna kitu ambacho wako nacho kwa nyumba zao wakati wako peke yao. Wakati tunakaa pamoja tunapata mali na anasema mali ni yake peke yake. Tunataka tuwe equal kwa maana tunafanya kazi pamoja, tuwe equal sisi wamama na wazee.

Masomo ya wakati huu si mzuri sana na haisaidii watoto wetu kwa maana ina maneno mengi wanabeba, na wasaidiwe sana maneno ya kusoma. Kwa maana wanachoka sana fikira na wengine ni wadogo sana. Masomo irudi kama ya zamani ile tulikuwa tunasoma.

Mimi ni mkulima hapa Eldoret. Tunafanya kazi ngumu sana ya kulima na wakati tunauza chakula chetu, inakuwa si rahisi sana na tunaumia sana. Shida inakuwa nyumbani na wamama ndio wanaona shida wakati wako nyumbani. Tunataka hiyo maneno ya wakulima iangaliwe sana kwa maana Serikali hii inawekwa ndio isaidie wakulima sana na isaidie wananchi. Asante sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana mama kwa kulinda wakati. Christopher Sumbeiyo.

Christopher Sumbeiyo: My name is councilor Christopher Sumbeiyo, councilor from Pioneer and (?). I am told only 3 minutes, so I have a memorandum of 10 pages and I am not going to read all, I just want to highlight some few points. Starting by political parties, I want to say that I propose that we should have a maximum of 3 political parties, and the office of the leader of opposition shall be entrenched in a Constitution with necessary facilities, privileges and manpower.

About the structure and system of Government, I propose we adopt the federal system of Government in which the Executive and Legislative authorities split between the central union Government and regional. That is district Government for effective service delivery and bring the Government close to the people. When I talk of majimbo, I mean the district not the current provincial now. The Executive powers to be vested in a President of the republic. The Vice President be chosen at the same time as the President's running mate and to hold office for the same term. I am just skipping because it is a memorandum, I talk of the Legislature. Each district to have one seat for an elected senator, each district of Kenya to have one seat for a woman MP. Nominated members of the House of Representatives shall represent the civic interest, such as people with disability, others from maybe cereal farmers, tea, coffee, horticulture, dairy and even jua kali and others.

I am trying to go speedily because I have been told it is only 3 minutes.

Com. Salome Muigai: It was.

Christopher Sumbeiyo: Yah. Two minutes, so I don't know where to go now. Let me come to the Vice President. I want to say that the Vice President as I said shall be elected the same time with the President, and he shall act as the President in case of the President's death or resignation or removal or otherwise.

The cabinet; I propose that the number of ministries and Ministers should be regulated by the Constitution to only 15. The office of the Attorney General and the Solicitor General should be separated. I go to local Government where I come from, I can't forget that one. Cap 265 law of Kenya should be amended to give more powers to the local authorities to run and control and manage their affairs. Mayors of municipalities and cities where the capital of regional Government is sited will be elected directly by the people of that region. I mean when I talk of the region, I mean the district. Chairmen of local authorities within regional to be elected directly by residents of that locality. A local authority in a region to be autonomous, I mean now that all powers to be empowered to a local authority. Let me see what else I will touch.

Com. Salome Muigai: And that will be the last touch

Christopher Sumbeiyu: Okay. Let me talk of electoral system and process. The electoral Commission should be given more powers to effectively manage the electoral process in Kenya. All political parties to carry out nominations for the civic, regional and Parliamentary candidates on the same day, not to give time for others to defect. We should (?). The outgoing President, Parliament, regional legislative assembly and civic authorities to remain in office until the last day before their successor's have gone in. In other words, they should be (?). I don't know if I still have more time madam?

Com. Salome Muigai: No Mr. Diwani you don't but thank you (?)

Christopher Sumbeiyu: Otherwise I am going to leave my memorandum (?)

Com. Salome Muigai: Yes, please do, please do

Christopher Sumbeiyu: Thank you madam

Com. Salome Muigai: Somebody has a question for you.

Com. Riunga: Councilor, sijui labda kama hiyo ime(?) katika memorandum lakini ningetaka unifafanulie. Umependekeza kwamba tuwe na Serikali za wilaya

Christopher Sumbeiyu: Ndio

Com. Riunga: Sasa, hizo Serikali zitatoa pesa ya kujigaramia wapi au unapendekeza pesa zitatoka wapi?

Christopher Sumbeiyu: Ile collection ambayo inafanywa katika every wilaya itumike katika wilaya hiyo na ikiwa pengine

haitaweza kugharamia gharama zote, then ile central Government inaweza kusaidia.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Njuguna Ngugi?

Njuguna Ngugi: Kwa majina ni kama vile mnavyosikia nikiitwa Njuguna Ngugi na niko na machache ya kusaidia hii Commission. Ya kwanza nitasema kuhusu, Commission iangalie upande wa barabara maana kuna watu ambao, kunaweza kuwa kuna shamba fulani hapa na upande ule uuzwe na njia ile wanaweze kutokea karibu iko kwa hiyo shamba. Nadhani hapo mungeangalia muone, musaidie wananchi kupata njia ile ya karibu kupita. Pia, mashamba mengi yameshafanywa survey na hiyo njia ile ilitolewa, kweli imerudi imefinywa imeisha na Serikali iko na wazee wa mtaa wako. Kwa hivyo hilo jambo muangalie.

